ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad **Kaimu Katibu wa Baraza la Wawalishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

WIMBO WA TAIFA

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 18 Januari, 2012

(Kikao Kimeanza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya Taarifa naomba nikukaribisheni tena katika Mkutano wetu huu wa Sita wa Baraza la Nane. Nafikiri sote tupo wazima. Na mimi mwenzenu nashukuru sijambo. Nadhani nduguzangu wamefanya nafasi kuwa ndogo wakafikiri afya yangu imepungua sana kiasi cha kuwa nitahitaji nafasi ndogo. Lakini kwa kweli nipo fiti naneno ya vijana na namshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Tano wa Baraza la Nane la Wawakilishi lililofanyika kuanzia tarehe 12 Oktoba mwaka 2011 hadi tarehe 26 Oktoba mwaka 2011, Baraza lilipitisha Miswada mitatu ya Sheria kama ifuatavyo.

1) Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa Ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao Mengine ya Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

3) Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti Bora Ndani Yake.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 90(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2011, naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo mitatu imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naomba kuwasilisha.

Hiyo ni taarifa ya kwamza ambayo waheshimiwa Wajumbe naomba muipokee kwa sababu hiyo ni kazi ambayo mmeifanya katika mkutano uliopita.

Taarifa ya pili Waheshimiwa Wajumbe tumeona tuitoe rasmi kwa sababu jana iliulizwa kwamba kuna mwenzetu mmoja haonekani. Kwa hiyo inafaa tutoe taarifa rasmi kwenu Waheshimiwa Wajumbe, lakini pia na wananchi na wao waelewe kwamba kumetokea jambo fulani.

Hii ni taarifa ya Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim aliyekuwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kupata uteuzi mwengine. Tuna heshima kubwa kutoa taarif a kwamba ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim ambaye alikuwa Katiba wa Baraza la Wawakilishi amepata uteuzi mwengine. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amemteuwa ndugu Ibrahim kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Ndugu Ibrahim aliapishwa kuwa DPP siku ya Jumapili tarehe 15/01/2012 na kuhitimisha kipindi cha takriban miaka 20 katika utumishi wake wa Baraza la Wawakilishi tangu kuajiriwa kwake tarehe 20/08/1992. Kabla ya uteuzi ndugu Ibrahim alikuwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa miaka mitano, aliteuliwa mara ya kwanza Januari 2007 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati huo Dokta Amani Abeid Karume. Ndugu Ibrahim aliteuliwa tena kuendelea na wadhifa huo na Mhe. Dokta Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwaka jana 2011.

Kabla ya kuwa Katibu wa Baraza, alishika nafasi mbali mbali akiwa mfanyakazi wa kawaida wa Baraza la Wawakilishi. Kwanza aliajiriwa kama Afisa Utumishi mwezi wa Ogasti mwaka 1992. Nafasi hiyo aliifanyia kazi kwa mwaka mmoja mpaka Ogasti mwaka 1993 ambapo aliteuliwa kuwa Afisa wa Shughuli za Baraza hadi Januari mwaka 1998, alipopewa dhamana ya kuwa Msaidizi Mshauri wa Baraza. Katika mwezi wa Ogasti mwaka 2000 ndugu Ibrahim aliteuliwa kuwa Mkuu wa Divisheni ya Ushauri wa Kisheria. Dhamana ambayo aliendelea nayo mpaka alipoteuliwa kuwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Pamoja na nyadhifa hizo ndugu Ibrahim alikuwa Katibu Kamati kwa kipindi chote alichotumikia Afisi ya Baraza mpaka alipoteuliwa kuwa Katibu wa Baraza. Nje ya Afisi ya Baraza aliwahi kuwa Mratibu wa Programu katika Kamati ya Vyama vya CCM na CUF *Inter Party Committee* yaani (IPC), iliyoundwa kufuata muafaka wa kisiasa wa mwaka 1999.

Nataraji sote tunamfahamu ndugu Ibrahim katika utendaji wake hapa Baraza la Wawakilishi. Ingawa baadhi yetu tumekaa naye kwa muda mfupi. Ni mtendaji makini, mkweli, muamuzi na muaminifu na ndio maana ameweza kufanya kazi zake vizuri hapa Baraza na kupata uteuzi mwengine ambao ameupata hivi karibuni. Tunataraji Mwenyezi Mungu atamsaidia katika kupata mafanikio zaidi. Vile vile tunataraji mrithi wake naye atafanya kazi zake vyema na kuendeleza mfanikio aliyoyaacha ndugu Ibrahim.

Waheshimiwa wajumbe naomba kutoa taarifa hiyo kwenu, ili muelewe mwenzetu huyu kwa kiasi gani amefanya kazi na usoefu wa kiasi gani anao ndani ya Baraza hili na hatimaye kupata uteuzi mpya wa kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Labda zaidi wananchi wanaweza wakasema mbona mwanzo alikuwa Katibu lakini sasa anakuwa Mkurugenzi. Mkurugenzi wa Mashtaka kwa maana ya Director of Public Prosecution (DPP) ni nafasi ya kimataifa hasa katika vyombo vyetu vya kisheria katika *Common Wealth* . Sasa anaitwa *Director* lakini kwa kweli ni mtu mwenye hadhi kama Jaji wa Mahakama Kuu. Kwa hiyo isionekane kwamba ametoka kuwa Katibu ambaye alikuwe sawa sawa na Katibu Mkuu wa Wizara nyengine yoyote na kenda kwenye *Director* tukaona kama ameshushwa cheo. Hapana, hilo ni jina la kimataifa (*Director of Public Prosecution)* Mkurugenzi wa Mashtaka lakini kihadhi yake anafikia sawa na Jaji wa Mahakama Kuu.

Waheshimiwa Wajumbe, waheshimiwa wasikilizaji wetu na wananchi kwa ujumla naomba kutoa taarifa hiyo kwenu. Ahsante sana.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyeke, kuanzia tarehe 27 Oktoba mwaka 2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba

ya Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya Mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Nam. 6 ya Mwaka 1999 na kutunga Sheria mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu, Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu. Sasa naomba kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Wajumbe wangu wa Kamati ya kusimami Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba Kuwasilisha Mezani ripoti ya Kamati ya Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi juu ya Mswada wa Sheria ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa kisiasa, baada ya kustaafu Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

TAARIFA

Mhe. Spika: Nadhani kabla ya kuendelea jana tulikubaliana katika brifing ambayo tulipeana taarifa kwamba kutokana na muda tulionao wa Mkutano huu wa Sita na kwa mujibu wa masuali tuliyonayo wingi wake, tulikubaliana kwamba tutenge kando kanuni ili kuongeza muda mpaka saa 5:00 kabla ya shughuli nyengine hazijaendelea. kwa hivyo kwa kuwa jambo hilo linaanza leo basi tumuombe Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kutoa hoja hiyo ili tuende kwa mujibu wa utaratibu. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ya kutenga kuweka kando muda wa maswali badala ya kumalizia muda wetu wa kawaida saa 4:00 na sasa uweze kuendelea mpaka saa 5:00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili*: Mhe. Spika, naafiki.*

Mhe. Spika: Kwa hivyo sasa kipindi cha Maswali kitaendelea mpaka saa 5:00 penye majaaliwa.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 45

Malipo Kwa Wahanga wa Meli ya *MV Spice Islanders*

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza:

Mhe. Waziri, tumepata taarifa kwamba mezi mmoja tu baada ya Meli ya *MV. SPICE ISLANDER* kuzama, tayari tajiri wa meli hiyo ameshalipwa malipo ya Bima ya meli yake iliyozama, pamoja na abiria na mizigo.

(a) Je, Mhe. Waziri ni kweli tajiri wa meli hiyo ameshalipwa Bima hiyo, na kiasi gani cha fedha alizolipwa.

(b) Kama ameshalipwa Je, kiasi gani kimetumika kuwalipa watu waliozama na meli hiyo pamoja na mizigo iliyokuwemo.

(c) Na kama ameorodhesha abiria na mizigo aliopakia je, ni watu wangapi waliopata malipo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:
Mhe. Spika, kabla ya kujibu suali naomba kutoa salamu za kheri ya mwaka mpya kwako wewe Mhe. Spika, Waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wote. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba kutoa maelezo mafupi kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake lenye vifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri wa Baharini ya Zanzibar Nam. 5 ya mwaka 2006 inataka walimiliki wa meli kukata bima ili kumuwezesha mmiliki huyo kulipa fidia pale yanapotokezea majanga yanayosababisha maafa. Aidha sheria hiyo kifungu cha 394 kinaeleza kuwa wamiliki wa meli, watawajibika kwa maafa ya kuumia au vifo vya abiria na uharibifu au upotevu wa mizigo unaotokea wakati wa safari ikiwa umesababishwa na uzembe au makosa ya wafanyakazi au mawakala au wamiliki wenyewe.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamo wa Pili wa Rais sasa naomba kujibu suala la Mwakilishi kwa pamoja kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, serikali haina taarifa ya mmiliki wa meli wa *MV Spice Islanders I* iliyozama tarehe 10/9/2011 katika mkondo wa Bahari ya Nungwi kuwa

amelipwa bima hiyo. Isipokuwa tunachofahamu ni kwamba kuna mazungumzo baina ya Kampuni ya *Alliance* ambayo ndio kampuni mama iliyotoa Bima kwa kampuni hiyo na *Visiwani Shipping Company Limited*. Hata hivyo serikali itaendelea kufuatiliwa kwa ukaribu taarifa hiyo na mara tutakapoweza kupata taarifa rasmi tutawajulisha wananchi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais naomba kumuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alivyojibu amesema kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Baharini kwamba wamiliki wa meli wao ndio wanaotakiwa waweze kulipa fidia kwa wale walioathirika.

(a) Suala langu liliuliza je, Mhe. Waziri ni kweli tajiri wa meli hiyo ameshalipwa Bima hiyo na ni kiasi gani cha fedha alizolipwa?

Mhe. Spika, jawabu alilonipa Mhe. Waziri amesema kwamba hawana taarifa, mimi sijaridhika nalo. Kwa sababu suala hili limeliuliza kwa muda mrefu. Ilikuwa ni wajibu wa serikali kufatilia ili kujua Sherika la Bima ambapo ndipo walipokata Bima hiyo ili kujua kwamba wamelipwa au hawajalipwa. Mpaka leo Mhe. Waziri ananilijibu suala hili anasema kwamba serikali inafuatilia wakati Shirika la Bima ambalo tunalohisi kwamba wamekata bima hii ni Shirika la Bima la Zanzibar.

Je, Mhe. Spika, yupo tayari Mhe. Waziri kabla ya kumaliza kikao hichi cha Baraza kuja kutujibu tena suala hili akatueleza kwamba Kampuni imeshalipwa Bima au haijalipwa.

(b) Mhe. Spika, kama kampuni hii imeshalipwa hiyo bima je, kuna watu wangapi mpaka sasa hivi wameshaweza kulipwa fidia zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama jibu langu la msingi linavyosema kwamba sisi mpaka sasa ndani ya serikali hatujapokea taarifa rasmi iliyoonesha kwamba hii Kampuni ya Bima imewalipa wahusika Bima waliyokata. Nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba tumewasiliana na wahusika na wao wamesema kwamba bado hawajalipa Bima Kampuni ya *Visiwani Shipping Company*.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize suala la nyongeza Mhe. Waziri lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Waziri kwa mujibu wa taarifa yake ni kwamba serikali haina taarifa ya ulipaji wa bima hii na kwamba wanaendelea kuwasiliana.

(a) Tunaomba atwambie anahitaji muda gani, siku ngapi, miaka mingapi, ili kuweza kujua taarifa hiyo.

(b) Ni wajibu wa nani wa kujua kwamba meli hii inabima na kwamba tayari wameshalipwa Bima kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nimeeleza hapa kwamba kampuni hii ya Visiwani *Shipping Campany Limited* haijalipwa Bima, na tutaendelea kufuatilia kwa karibu, ili mara takapolipwa basi taarifa tutazitoa kwa wananchi.

Kuhusu bima waliyokata *Visiwani Shipping Company*, wamekata Bima ya abiria kwa ajili ya meli yao, ndiyo taarifa ambazo tunazo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi niungane na Mhe. Waziri kuwatakia kheri ya mwaka mpya wote.

Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyonge. Kwa sababu maswali ambayo yameibuliwa katika suala hili kuu mengi ,yangetegemewa majibu yake yatokane na ripoti ya suala zima la uchunguzi wa kadhia hii. Lakini anatwambia ripoti ya uchunguzi kuhusiana na ajali hii ya *MV. Spice Islanders* lini itafikishwa katika Baraza la Wawakilishi na wananchi kuijua ili wananchi wako waweze kuijadili na kujua uhalisia wa jambo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli tume iliyoundwa na Rais kuchunguza uzamaji wa meli ya *MV. Spice Islanders* I imekamilisha kazi yake na yatari ripoti hiyo imewasilishwa serikalini. Serikali imeshaanza kuifanyia kazi ripoti hiyo na hivi sasa imo katika hatua za mwisho. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kabla ya kumalizika kikao hichi cha Baraza la Wawakilishi Serikali kupitia Katibu Mkuu Kiongozi atatoa taarifa rasmi kuhusu ripoti hiyo ya uzamaji wa meli ya *Spice Islanders.*

Nam. 26

Uharibifu wa Fukwe.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:

Ukataji wa miamba na uchimbaji wa mchanga katika ufukwe ni changamoto inayowakabili wakaazi wa visiwani hivi vya Unguja na Pemba katika baadhi ya maeneo na kuleta uharibifu wa fukwe.

(a) Kwa vile visiwa hivi vimezungukwa na bahari ni nini hatima ya uharibifu huo.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe athari zinazoweza kujitokeza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Anajibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu suala naomba na mimi unipe ruhusa ya kukutakia wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kheri na fanaka katika mwaka huu mpya wa 2012. Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kujibu suala hili la Mhe. Mwakilishi naomba kwanza nitoe maelezo ya ufafanuzi yafuatayo.

Miamba ya baharini na matumbawe ni sehemu muhimu ya mazingira ya baharini katika kuongeza viumbe vya baharini na hasa samaki ambao wamekuwa ndio tegemeo kubwa la kitoweo kwa Wazanzibari waliowengi. Aidha miamba hiyo inasaidia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza kasi ya mawimbi ya bahari yanayofika ufukweni na hivyo kupunguza kasi ya mmong'onyoko katika maeneo ya fukwe.
Mchanga uliopo katika fukwe umekuwa na kazi kubwa ya kupunguza kasi ya mawimbi ya bahari na kupunguza kasi ya mmong'onyoko unaosababishwa na mawimbi hayo, endapo hautochukuliwa au kuchimbwa. Mchanga wa fukwe ni miongoni kwa kivutio kikubwa katika uwekezaji katika shughuli za kitalii, hali ambayo inaiyongezea nchi yetu kipato na hasa fedha za kigeni.

Mhe. Spika kasi ya mmong'onyoko unaosababishwa na mawimbi hayo endapo hauotochukuliwa au kuchimbwa. Mhe. Spika, mchanga wa fukwe pia umekuwa ni miongoni mwa kivutio kikubwa katika uwekezaji wa shughuli za kitalii hali ambayo inaiongezea nchi yetu kipato na hasa fedha za kigeni.

Mhe. Spika, kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa kwa kukata matumbawe na kuchukua mchanga katika maeneo ya fukwe, hivi sasa maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba yameonyesha kuathirika. Baadhi ya maeneo hayo kwa Pemba ni Kisiwa Panza, na Tumbe; na kwa Unguja baadhi ya maeneo yaliyoathirika ni Jambiani, na Nungwi. Aidha, maeneo yenye mahoteli kama vile Kiwengwa na Uroa kumekuwa na athari za mmong'onyoko kutokana na uchukuaji wa mchanga katika fukwe.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hatima ya uharibifu huo kwa Zanzibar ni kukabiliwa na upungufu mkubwa wa samaki kutokana na kuharibiwa na mazalia ya samaki; pia kupoteza ardhi za kilimo na makaazi kutokana na kupanda kwa maji ya bahari na kuharibika kwa mfumo wa maji safi na salama yaliyopo nchi ya ardhi. Ili Zanzibar iwe salama kimazingira hatuna budi viongozi wawekezaji na wananchi wote kuheshimu na kufuata sheria zilizopo na tushirikiane kwa pamoja katika kuondoa muhali uliopo wa kufumbia macho uharibifu unaoendelea.

(b) Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea na mpango wa kuwaelimisha wananchi juu ya athari zinazotokana na ukataji wa miamba pamoja na uchukuaji wa mchanga katika maeneo ya fukwe. Mpango huo umekuwa ukihusisha redio, TV na mikutano mbali mbali ya jamii. Aidha, hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira inaendelea kutekeleza kazi za usimamizi wenye uwiano wa ukanda wa pwani (*Integrated Coastal Zone Management – ICZM*) ili kuwawezesha wananchi katika kila Shehia kuunda Kamati za *ICZM* katika maeneo yao. Kwa sasa kamati 10 za *ICZM* zimeundwa kwa majaribio, kamati moja ipo katika kila Wilaya Unguja na Pemba. Kamati hizo pamoja na mambo mengine zina majukumu ya kuhakikisha usimamizi endelevu wa maliasili na kutoa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira ya bahari na fukwe ili kupunguza athari za kimazingira.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maeneo mengi sasa hivi yameanza kuathirika na matatizo hayo ya uharibu wa mazingira, na kwa kuwa serikali kila siku inapiga kelele kuhusu suala la uharibifu huo wa mazingira na bado wananchi hawajaelewa tatizo hili. Je, Mhe. Waziri huoni kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais kuweka mabango kila shehia na kila fukwe ili wananchi waweze kuelewa matatizo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, mimi nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli pamoja na serikali kukemea suala hilo na pamoja na kuwepo kwa sheria ya mazingira, na kuwepo na sera ya mazingira lakini bado kuna ugumu mkubwa kwa wananchi kufuata kama inavyotakiwa kwa kuyatunza mazingira. Mhe. Spika, mimi nakubaliana nae kwa kweli kazi hii mabango yamewahi kuwekwa katika maeneo mengi lakini tutashirikiana pia na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili kuona kwamba tunayaimarisha hayo na msisitizo wa kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili kuzuia uharibifu huo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Je, hii sera iliyopo ni ya mwaka gani na inafanyakazi au imepitiwa na wakati, na kama imepitiwa na wakati ni jitihada gani zimechukuliwa na wizara yake kuona kwamba inapatikana mpya katika mazingira mapya.

b) Mhe. Waziri amekiri kwamba kweli kuna uharibifu wa mazingira. Je, ni nani wanaoshiriki ni makampuni ya nje, wawekezaji au raia wa ndani na ni hatua gani zinazochukuliwa katika kudhibiti hali hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kuhusiana na sera ya mazingira hivi sasa kama tulivyomuahidi wakati wa bajeti sera mpya ya mazingira hivi leo ninapozungumza hapa inapitiwa katika hatua za mwisho katika Kamati ya uongozi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ili iweze kutolewa rasmi ile ambayo imefanyiwa mapitio.

Mhe. Spika, kuhusu suala la pili wale ambao amewataja wote wawekezaji, wananchi wote kwa pamoja wanashiriki katika uharibifu huu kila mmoja kwa aina yake, na matatizo kama haya yanapotokea sisi huwa tunaongozwa na sheria. Mhe. Spika, tatizo kubwa linalolikabili suala hili ni suala mtambuka halihusishi ofisi moja. Kwa hivyo, lile suala zima la kwamba kila mmoja anahusika maana yake tunaposema kwamba tuna sheria hapa ina maana tuna watu ambao wao ndio wanaosimamia zile sheria kuona kwamba zinatekelezwa, au tunapowakamata watu katika uhalifu wa kuharibu mazingira wao ndio wanaotakiwa kuwashughulikia nao inabidi wawajibike ipasavyo.

Lakini vile vile tunajitahidi kuendelea kutoa elimu na kujenga mashirikiano ya karibu zaidi na *coordination* ambayo itatuwezesha wote wadau tunaohusika

kuweza kukaa pamoja na kuhakikisha kwamba suala hili tunalipunguza na hatimae kuliondoa.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, je Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna baadhi ya wawekezaji ndio wanaosababisha uharibifu wa mazingira hasa kwa kuzifukia fukwe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, mimi naomba nikubaliane nae kwamba kweli baadhi ya wawekezaji ndio wanaoshiriki katika uharibifu huu wa mazingira, lakini serikali haikukaa kimya wala haikuwafumbia macho huwa tunachukua juhudi za lazima kuona kwamba uharibifu huo unazuiliwa.

Nam. 24

Chuo Cha Mafunzo Kengeja

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:-

Serikali ilichukua mashamba ya wananchi yalioko Maumbwini Kengeja kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Mafunzo na Mashamba ya Makomba Kengeja kwa ajili ya kujenga nyumba za askari na Gereza.
Wanafunzi wa Chuo hicho ni wachache ukilinganisha na idadi ya askari. Aidha Chuo hicho kinalima mazao ya mihogo na mpunga ambayo hayalipi gharama za uendeshaji wa Chuo.

Kwa kuwa Chuo kinaendeshwa kwa hasara Je, Mhe. Waziri huoni kuwa ni vyema Chuo hicho kikafungwa na mashamba yakarejeshwa kwa wenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo Kengeja Pemba kimeanzishwa katika miaka ya sabiini (70), chuo hiki kinauwezo wa kuchukua wanafunzi sitini kwa wakati mmoja. Chuo kina eneo lisilozidi ekari mia tano (500) zinazojumuisha maeneo ya kilimo cha juu, makaazi ya wanafunzi na maeneo ya makaazi ya Maafisa, Askari na familia zao pamoja na kilimo cha mabondeni. Aidha, mashamba yaliyopo katika chuo hiki ni mazuri sana kwa ukulima wa mpunga. Hii inapelekea kwamba wakati wa msimu wa kilimo cha mpunga, wanafunzi

kutoka katika vyuo vya Wete, Tungamaa na Kangagani wanahamishiwa Kengeja ili kushiriki kilimo cha mpunga na kukiletea tija zaidi.

Mhe. Spika, kwa zile ekari ambazo hazikutumika, uongozi wa chuo umeweka utaratibu maalum wa kuwaazima wananchi wanaoishi karibu na mashamba hayo kwa mkataba na kwa kawaida maeneo yote hulimwa katika msimu husika. Hii ndio sera ya Chuo cha Mafunzo kuishi vizuri na wenyeji wake walioko mipakani ili kuepuka malumbano.

Mhe. Spika, naomba kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba chuo hakiendeshwi kwa hasara kwa vile lengo lake ni kutoa mafunzo bila ya malipo kwa wanafunzi wake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c).

a) Kwa kuwa lengo la suala hili ni kutoa nafasi kwa wananchi kujiendeleza kwa kilimo na kuna ukweli uliokuwa haupingiki kwamba idadi ya wanaopelekwa pale ni kidogo kiasi cha kwamba Mhe. Waziri amethibitisha kwamba hutolewa wengine kutoka Tungamaa na Kangagani jambo ambalo sio la kawaida kwa sababu magari hayo sisi hatuyaoni na sijui kama yapo ya kuwachukua wafungwa hawa kwenda kulima. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kwa manufaa ya kilimo tulichokiweka sasa kuwa serikali ingeliangalia upya suala la kuwepo tena kwa Chuo hicho cha Mafunzo katika eneo hilo.

b) Mhe. Spika, kwa manufaa ya wananchi si rahisi Mhe. Waziri kama atakubaliana na mimi kungojea mpaka watu wameshamaliza kulima ukaambiwa sasa njoo uchukue kikataa ulime, kwa sababu kilimo si kama maandishi kwamba unakwenda na kalamu yako ukalima. Je, Mhe. Waziri anaona haoni kwamba anawatia tatizo tu wananchi kwa kungojea mpaka mashamba yameshawashinda ndio wakawaita.

c) Katika uendelezaji wa sera ya kilimo ni kwamba mashamba haya ya eka mia 500 wananchi wa kisiwa cha Pemba kuyakosa haoni kwamba yanatia upungufu wa chakula kwa sera hii ya serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane nae Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli katika vyuo vyetu vingi vya mafunzo idadi ya wanafunzi ni wachache, lakini hii inaotokana na kwamba kwanza kuna kesi nyingi ambazo

bado tunasubiri zihukumiwe. Kwa hivyo, tuna matokeo kwamba tuna wanafunzi walioko rumande wengi kuliko wafungwa, lakini hizi ni sehemu zile za magereza au katika vyuo vikuu.

Kwa hivyo, kwa wale waliopo na hasa kwa Mtambile pale tunazalisha chakula na unajua ugumu wa kilimo cha mpunga kwani kilimo hiki si kilimo cha rahisi matayarisho yake na hasa pale hatuna *machine* za kisasa. Kwa hivyo, tunahitaji nguvu kazi nyingi kwa wakati mmoja kuanza kutayarisha ardhi na mambo mengine. Hivyo, atakubaliana na mimi Mhe. Mwakilishi kwamba kilimo cha mpunga sio masihara na ndio maana matokeo yake tunapata mavuno madogo kwa eneo. Mhe. Spika, kama nilivyosema mabonde yote pale yanalimwa, hivyo tukiona kwamba nguvu yetu ni ndogo basi tunazungumza vizuri na wananchi tena mapema kabla ya msimu.

Mhe. Spika, pia tunajitahidi katika vyuo vyetu vya mafunzo kujitegemea kwa chakula. Kwa hivyo, kambi moja utakuta inalisha kambi nyengine hili ni suala la msingi kabisa kwamba tunaendesha kilimo katika kambi nyengine, kambi nyengine tuna ufugaji lakini kusaidia kulisha kambi nyengine kama tungetegemea kwa bajeti tu basi wanafunzi wetu watakuwa hawashibi vizuri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba wafungwa katika magereza yetu ni wachache na kwa kuwa tuna maeneo mengi ambayo yanabeba hao wanafunzi wa chuo cha mafunzo, na kwa kuwa eneo hili linalotajwa lina ekari nyingi za kilimo na wafungwa kwa sababu ni wachache.

Je, haoni Mhe. Waziri kwamba kuna haja ya kuhamishwa wafungwa walioko kule Kengeja na wakaachiwa hilo eneo wananchi wakalima kwa sababu tunahitaji kilimo na sasa hivi ni wakati wa mapinduzi ya kilimo. Kwa hivyo, kwa sababu kuna ekari nyingi za kilimo ni bora wakaachiwa wananchi wakaliendeleza kwa kilimo na wale walioko kule wakahamishiwa katika magereza mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nafikiri kwa malengo yetu ya kilimo hasa cha mpunga bado maeneo mengi yapo wazi na naamini tukijipanga vizuri hasa katika mabonde ya Mkoa wa Kusini kule Pemba tunaweza tukawapeleka wananchi na wakazalisha vizuri zaidi na tukaleta mapinduzi tunayoyataka ya kijani na tukahakikisha kwamba lile tunalolitaka lipo. Kwa hivyo, unajua kwenye vyuo vya mafunzo ni kama *graph* inapanda na kushuka, leo wapo wanafunzi wanane mimi nilitembelea mwenyewe Kengeja nikakuta wanafunzi 12, lakini hatujui baada ya miezi 6 utakuta ushafika 60.

Mhe. Spika, kama nilivyosema maeneo haya ni *potential* ya kuzalisha chakula kwa kambi nyengine. Mhe. Spika, mimi naomba tugawane kazi, wananchi maeneo mengine yapo walime kwengine na huku watuachie chuo cha mafunzo tulime. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 38

Utaratibu wa Wafanyakazi Kupokelea Benki

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza :-

Serikali yetu imeanzisha utaratibu mpya wa kutoa mishahara ya wafanyakazi wa SMZ kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar, lakini imekuwa ni usumbufu kwa wafanyakazi hasa wanaoishi maeneo ya Vijijini (shamba), kwani hulazimika kufuatilia huduma hiyo ya haki yao ya mishahara Mjini, wakati ambapo hutoa nauli ya kwenda na kurudi na pia siku nyingine hukosa pesa kutokana na foleni kuwa kubwa huko Benki.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa utaratibu huo mpya unaleta usumbufu kwa wafanyakazi wanaoishi vijijini.
(b) Kwa kuwa bado huduma za benki huko Vijijini hazijaimarika huoni kuwa zoezi hilo lingelisitishwa kwanza hadi hapo huduma hiyo itakapoimarika huko Vijijini.
(c) Je, unataka kuwaambia nini wafanyakazi hasa wa Vijijini na lini usumbufu huo utaisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, utaratibu uliowekwa na Serikali wa kulipia mishahara ya watumishi wa Umma kupitia Benki unasaidia sana kunusuru upotevu wa fedha za Umma na wala Serikali haina nia ya kumsumbua mtumishi yeyote yule. Utaratibu wa kulipia mishahara kupitia Benki hutumika nchi nyingi duniani. Aidha, Serikali haimlazimishi mfanyakazi yeyote aliyeko mjini au kijijini kupokea mshahara wake kwa kutumia Benki ya Watu wa Zanzibar. Mtumishi anaweza kutumia benki yoyote ile kama anahisi benki hiyo ipo karibu na eneo analoishi au analofanyia kazi.

b) Mhe. Spika, ni kweli huduma za kibenki hazijaimarika sana vijijini, lakini zoezi la kutoa mishahara kupitia Benki haliwezi kusimamishwa kwa sababu ni njia moja wapo itakayosaidia katika kuziimarisha benki zilizopo Zanzibar, kutokana na ushindani utakaojitokeza. Aidha, serikali itasimamia kwa karibu zaidi uimarikaji wa huduma za kibenki vijijini.

c) Mhe. Spika, napenda kuwafahamisha wafanyakazi wote waliopo mijini na vijijini kuwa nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa fedha za umma hazipotei. Hata hivyo, Serikali itachukua juhudi za kuhakikisha kuwa huduma za kibenki zitaendelea kuimarishwa awamu kwa awamu kwa lengo la kuwasaidia zaidi wananchi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba wananchi au wafanyakazi wa serikali wanaruhusiwe mishahara yao kuelekeza kwamba ulipwe katika benki yoyote. Mimi suala langu nilielekeza zaidi kwa wafanyakazi ambao wanaishi vijijini ukiangalia mazingira ya Zanzibar sasa hivi mabenki takriban karibu yote yako katika maeneo ya mjini, lakini katika maeneo ya vijijini hakuna mabenki hayo.

Je, Mhe. Waziri haoni hivi sasa iko haja ya kuwaita viongozi wa benki zote kuangalia uwezekano wa kufungua *ATM* katika maeneo ya vijijini katika utaratibu kama wanaofanya *PBZ* kwa kushirikiana na Benki ya Posta kwa kuweka *ATM* ambazo zitaweza kusaidia zaidi ya wananchi wa vijijini kuacha kupata usumbufu wa kuja mjini kwa ajili ya kupanga foleni.

Mhe. Spika, kama vile nilivyoeleza katika suala langu ni kwamba wakati mengine anakuja mjini kupanga foleni basi huwa anakosa huo mshahara na anakwenda siku nyengine anakosa mpaka anakuja siku nyengine ndio anapata mshahara. Kwa hivyo, je Mhe. Waziri haoni hili wazo sasa hivi la kuwataka kuweka *ATM* katika maeneo ya vijiji ili kuweza kupunguza usumbufu kwa wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, ni kwamba ushauri wake Mhe. Mwakilishi ni mzuri nitawaita mameneja wa benki zote zilizopo Zanzibar ili tuweze kutoa nasaha hizi na hatimae ni dhahiri kwamba kwa sababu hii ni biashara watakubaliana na sisi kufungua *ATM* katika maeneo ya vijijini. Nitalifanya jambo hilo Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nimuulize swali Mhe. Waziri lenye kifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kutoa huduma bora kwa wananchi hasa katika kisiwa cha Pemba *PBZ* iliamua kujenga jengo moja kule Wete jengo zuri na la kisasa kwa nia ile ile ya kuwapa huduma wananchi hasa wa Kaskazini Pemba. Kwa bahati mbaya sana *PBZ* waliliuza jengo hilo kwa *ZECO*.

a) Mhe. Spika, ni sababu zipi zilizoifanya PBZ wauze jengo hilo kwa ZECO.

b) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kitendo hicho cha benki kilichofanya cha kuuza jengo lake hilo hakiendani na dhamira yake ya kuboresha huduma kwa wananchi.

c) Kwa kuwa baada ya kuliuza jengo hilo *PBZ* waliona umuhimu wa nalo jengo hilo na ndio maana katika kipindi hiki wamelazimika kwenda kukodi chumba katika jengo lake hilo ambalo wameliuza kwa *ZECO*. Mhe. Spika, kwa sababu hiyo huoni Mhe. Waziri kwamba kuna haja baada ya kuona umuhimu *PBZ* wakarudia kulinunua tena jengo lile kwa *ZECO*.

Mhe. Spika: Hili suala halina mnasaba wa moja kwa moja na utoaji wa mishahara, haidhuru ni kweli ni suala ambalo linahusu Benki ya PBZ lakini suala mama ilikuwa ni utaratibu wa utoaji mishahara kupitia Benki ya PBZ. Mhe. Mwakilishi nakuomba utafute utaratibu wa kuliuliza kwenye suala la msingi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, naipongeza PBZ kwa kujenga jengo jipya Chake-Chake Pemba ili kupunguza usumbufu wa wateja katika benki hiyo. Mhe. Spika, ni kwamba bado inaonekana benki hiyo ina wingi wa wateja wengi kwa vile kuna jengo kongwe pembeni yake. Je, serikali ina mpango gani wa kulifanyia matengenezo jengo hilo ili kukidhi haja ya kuhudumia wateja katika benki hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, jengo la zamani la PBZ lililoko Chake-Chake Pemba liko katika mpango mkubwa wa kufanyiwa matengenezo ili kuweza kutoa huduma ikiwa ni pamoja na huduma za kutoa mishahara. Hili lipo na tutalifanyia matengenezo karibuni tu.

Nam. 2

Watu Wenye Ulemavu Walioajiriwa

Mhe. Raya Suleiman Hamad - Aliuliza:-

Mhe. Waziri tokea kupitishwa kwa Sheria ya Watu wenye ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 9 ya mwaka 2006 inayotaka watu wenye ulemavu walio na sifa za kuajiriwa waajiriwe, Je ni watu wangapi wenye ulemavu wameajiriwa katika taasisi za Serikali.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora –Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjbu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba sheria ya watu wenye Ulemavu Nam. 9 ya mwaka 2006 imewataka watu wenye ulemavu walio na sifa za kuajiriwa waajiriwe. Hata hivyo, kabla ya kujibu suala hili naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza dhana na kauli hii ni pana sana, kwa hivyo inahitaji ufafanuzi na kuekewa utaratibu unaoeleweka ili iweze kutekelezeka. Wizara yangu ilikutana na Uongozi wa Baraza la Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar siku ya Jumatatu tarehe 07/03/2011 katika mkutano huo makubaliano kadhaa yalifikiwa. Miongoni mwa hayo ni kuingiza rasmi katika sheria na kanuni za utumishi wa umma utaratibu wa utekelezaji wa suala la uajiri wa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya Baraza lako tukufu, ni kwamba Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011, kifungu cha 58 (3) kimempa uwezo Katibu Mkuu Kiongozi kulegeza masharti ya ajira kwa Watu wenye Ulemavu. Hii inaonesha jinsi Serikali inavyowajali Watu wenye Ulemavu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora haikuwa na utaratibu wa kutenganisha takwimu zinazoonesha idadi ya watu wenye ulemavu walioajiriwa tokea kuanza kwa sheria hiyo. Suala la takwimu za aina hiyo linashughulikiwa na sekta inayosimamia watu wenye ulemavu.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa sababu watu wenye ulemavu wenye sifa kuanzia shahada ya mwanzo mpaka ya pili watu hao wanatafuta masomo sehemu mbali mbali ili kujiondolea mzigo na tegemezi kwa wazee wao au kwa jamii, lakini bado katika taasisi zote tunazopita watu hawa hawana ajira hata ile ya kuwa yeye ni *operator.* Kwa maana hiyo huwa wanakata tamaa ya kwamba wao ni watu ambao hawawezi kufanya kazi au hawawezi kutumikia jamii.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakuwa na nasaha gani za kuwa atapotoa ajira angalau katika taasisi japo moja moja watu hao wakapata ajira kujiondolea matatizo yao.

Mhe. Waziri wa Nch (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, na mimi nataka nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza watu wenye ulemavu kwa juhudi kubwa waliyonayo katika kujitafutia au kujiendeleza kujiongezea kiwango cha elimu mpaka kufikia ngazi ya *degree* ya kwanza na kuendelea. Hilo ni jambo jema kwa wananchi hawa.

Nilipokuwa nikijibu swali mama nilisema Sheria yetu ya Utumishi Nam. 2 imeweka mazingatio maalum kwa watu wenye ulemavu, nimuombe Mhe. Raya Suleiman kwa sababu watu wenye ulemavu nao ni wananchi wa nchi hii, sasa sheria ya Utumishi wa Umma tayari imeshaanza kazi zake na kwa sababu tayari Tume ya Utumishi Serikalini ndio inayohusika na masuala ya ajira, baada tu ya chombo hicho kuanza kazi zake rasmi masuala ya watu wenye ulemavu yatazingatiwa kwa nguvu zote za serikali.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Katika swali lake mama Mhe. Waziri alisema kwamba sheria hiyo inawataka watu wenye sifa ili kuajiriwa. Je, Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri ni sifa zipi ambazo zinatakiwa awe nazo muajiriwa huyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, sifa zinazohitajika ni viwango vyao vya elimu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kuwatakia heri ya mwaka mpya Waheshimiwa wote pamoja na wananchi.

Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri anakubaliana nami kwa sasa hivi kuwa imefika wakati kwa upande wa walemavu kwa sababu na wao ni katika jamii ambao wana haki, fursa sawa na wananchi wote, kufanya utafiti wa kina ili kuhakikisha kwamba tuna walemavu

wangapi, wangapi ambao wamesoma, na ni visomo vya aina gani ili wakati wa kuajiri waweze na wao kupatiwa nafasi za kuajiriwa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na Mhe. Asha kama swali lake alivyolieleza. Hivi sasa serikali kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais tayari inaifanya kazi hiyo, na kwa sababu ya suala ambalo limeulizwa hapa na kwa sababu ya suala zima la kiutumishi la kuajiriwa watu wenye ulemavu, wizara yangu itashirikiana na wizara ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ili kuweza kujua walemavu au watu wenye ulemavu waliopo nchini na haja ya wale ambao wanataka kuajiriwa kwa mujibu wa sifa walizonazo.

Nam. 19

Sala ya Iddi Kutosaliwa Pemba

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuulisa swali hili ameliondoa)

Nam. 21

Uezekaji wa Mabanda ya Skuli

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:-

Wizara ya Elimu imekuwa ikiwahamasisha na kuwashajihisha wananchi kujenga mabanda ya skuli katika maeneo yao, hadi kufikia hatua ya kufunga linta na hatua ya kuezeka kufanywa na Serikali.

(a) Je, kwa mwaka 2011, ni mabanda mangapi yaliyoezekwa Unguja na Pemba.
(b) Je, ni mabanda mangapi yaliyoezekwa katika Jimbo la Mtambile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 21 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Ni kweli kwamba Wizara ya Elimu imewashajihisha wananchi kupitia Kamati za Skuli na Kamati za Maendeleo za Vijijini kuanzisha miradi ya ujenzi wa madarasa katika maeneo yao ili kukabiliana na ongezeko la idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiunga na skuli zetu. Pia skuli mpya zinapojengwa katika

maeneo ya vijiji huwawezesha wanafunzi kupata elimu katika maeneo ya karibu ya sehemu ambazo wanaishi.

Sera yetu ya elimu inawahimiza wananchi waanzishe ujenzi wa madarasa mapya na waendeleze ujenzi hadi jengo linapofikia hatua ya kuezekwa na baada ya hapo Wizara ya Elimu na pamoja na wahisani humalizia kazi hiyo na kuyapatia madarasa samani. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Kwa mwaka 2011, jumla ya madarasa 136 yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yaliezekwa. Kati ya madarasa hayo madarasa 87 yapo Unguja na Madarasa 49 yapo Pemba.

b) Hakuna madarasa yaliyoezekwa katika skuli zilizomo katika Jimbo la Mtambile kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha. Hata hivyo, wizara inakusudia kuliezeka jengo la madarasa manne katika Skuli ya Sekondari ya Kengeja hivi karibuni baada ya kupatikana kwa fedha za Bajeti. Kazi za uezekaji zinatarajiwa kuanza katika mwezi wa Februari 2012.

Mhe. Moh'd Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa wizara yake katika mwaka 2010 mwezi wa Machi, Mhe. Rais Mstaafu alifanya ziara Kengeja na wizara yake iliahidi kuezeka hayo mabanda manne ya sekondari na mabanda saba ya *primary*, lakini hadi hii leo hakuna hata moja lililoezekwa. Je ni sababu zipi za msingi zilizofanya kuhalifu ahadi yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane naye kwamba ni kweli, lakini kama nilivyozungumza katika swali mama hatukuweza kuezeka wakati tulioahidi kutokana na bajeti tuliyokuwanayo. Lakini nataka nimuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yetu tayari katika kipindi hiki cha hivi sasa tumepeleka shilingi milioni hamsini katika Wilaya ya Kusini ili kuezekea skuli tatu za Wilaya ya Kusini na moja ikiwa ni skuli ya sekondari ya Kengeja ambao ina mabanda manne.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru sana. Mhe. Spika, wiki tatu zilizopita Kamati yako ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii uliituma kufanya kazi zake na moja katika kazi zake tulifika skuli ya sekondari ya Kengeja.

Kamati yako Mhe. Spika, ilishuhudia majengo matatu ambayo yamewekewa mwega ya majiti na huku wanafunzi wanasoma, kwa busara na huruma za kamati yako waliamua kuchangia bati mia moja. Swali langu.

Kwa sababu wizara imeshindwa kuwafanyia haki yao ya msingi wanafunzi wa Kengeja je, Mhe. Naibu Waziri lini hasa atafuatana nami na mwenyekiti wangu kwenda kukabidhi bati mia moja katika skuli ya Kengeja.

Lakini la pili, kwa sababu kamati imetoa agizo na imesema kwamba haitokuwa na haja ya kupitisha bajeti ya Wizara ya Elimu hadi wanafunzi wale wapatiwe haki yao. Naibu Waziri anasemaje kwa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nataka nikiri kama kamati ni kweli ilikwenda katika skuli hiyo ya Kengeja na ikaona kile Mhe. Hija ambacho amekieleza. Na kwa sababu hiyo Mhe. Spika, ndio maana huwa tunawahimiza wananchi kuchangia katika ujenzi wa maskuli yetu na wananchi wamehamasika katika Jimbo la Kengeja na kama hivi nilivyozungumza kwamba tayari Wizara ya Elimu kwa kuwa waziri wangu alikwenda baada ya ziara yao na kwenda kujihakikishia hali halisi waliyoikuta kuwa ni kweli, hivyo ile pesa chache ambayo tumetiliwa basi tutahakikisha tunaipeleka katika skuli hiyo ya Kengeja..

Mhe. Spika, kwa hivyo skuli hii itafanyiwa matengenezo kadiri inavyostahili na niko tayari kufuatana na Mwenyekiti wa Kamati kwenda kupokea hizo bati mia moja na kwa kweli nataka niishukuru kamati hiyo kwa walivyojitahidi kutoa msaada wao na niombe michango hii isiwe kwa kamati hii tu, bali kwa kamati yoyote ile ambayo itaona kuna tatizo basi ni vizuri isaidie. Tunashukuru sana Mhe. Spika.

Nam. 8

Umuhimu wa Alama za Barabarani (*Zebra Cross*)

Mhe. Raya Suleiman Hamad - Aliuliza:

Zebra Cross ni alama muhimu za barabarani ambazo madereva na wananchi kwa ujumla wanapaswa kuzielewa kwa kina. Je, Wizara yako imechukua juhudi gani za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa alama hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Raya Suleiman Hamad swali lake Nam. 8 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba alama za vivuko (*zebra*) ni moja kati ya alama muhimu za barabarani ambayo huonesha kivuko cha watembeao kwa miguu.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani inachukua juhudi kubwa na za kuendelea za kuwaelimisha madereva, wananchi pamoja na wanafunzi kwa kutumia vyombo vya Habari pamoja na kutoa mafunzo kwa skuli mbali mbali siku na miezi kadhaa wa kadhaa.

Mhe. Spika, mafunzo hayo ni pamoja na matumizi ya fimbo nyeupe kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa pamoja na mafunzo na matangazo wanayoyatoa lakini bado sheria ya *zebra* inaendelea kuvunjwa na kwa macho yangu nimeshuhudia watoto wakigongwa ndani ya alama ile ya *zebra*.

Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kunambia ni watu wangapi wameshtakiwa Mahkamani kwa kuwa wamekiuka sheria za *zebra*.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba madereva wetu wamekuwa na desturi ya kuvunja sheria hizi za *zebra* na kusababisha ajali. Napenda nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wenzetu wa Jeshi la Polisi kuendelea kusimamia sheria na kuwafikisha wavunjaji wa sheria hiyo katika vyombo vinavyostahiki ikiwa ni Mahkama.

Aidha, kwa jibu la idadi halisi ya watu ambao wameshtakiwa naomba nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba nitampatia majibu hayo kwa maandishi baada ya kufanya mawasiliano na wenzetu wahusika wa Idara ya Jeshi la Polisi.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka nimuulize kwamba pamoja na hatua nzuri za kuweka *zebra* katika maeneo mbali mbali, lakini kuna matatizo katika maeneo yetu ya Wilaya ya Mjini kuwa *zebra* nyingi zimekuwa katika maeneo ambayo pembezoni mwa barabara kuna vikuta, hii inapelekea kuwapa changamoto au uzito ndugu zetu walemavu ambao wanatumia *wheel chair*. Je, wizara yake ina utaratibu gani wa kuweka maeneo maalum ya kupita watu wenye ulemavu katika *zebra line.*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, azma ya serikali ni kujenga barabara ambazo zitaweza kukidhi mahitaji yote ya matumizi, lakini kutokana na ufinyu wa fedha barabara nyingi tunazozijenga zinakosa huduma hiyo ambayo ingehitajika ya watembeao kwa miguu na hao

watu wenye ulemavu nje ya barabara. Pamoja na hayo, tutahakikisha kwamba maeneo hayo maalum ya zebra kwa ajili ya watu wenye ulemavu tunayatenga na tunasimamia katika matumizi yake.

Nam. 79

Huduma ya *ICU* Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Suala la *ICU* kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja bado ni kitendawili ambacho hakina majibu. Katika Mkutano wa Bajeti 2011 Mhe. Waziri aliahidi kulifanyia kazi suala hili kwa nguvu zote na akaahidi kujiuzulu endapo suala hilo halitakamilika ndani ya miezi 6, sitaki kuulizia juu ya kujiuzulu kwake lakini naomba Mheshimiwa Waziri atujulishe.

(a) Amefikia wapi katika kutekeleza ahadi yake hiyo.

(b) Je, sasa tuamini kuwa SMZ imeshindwa kuimarisha huduma hii kwenye Hospitali ya Rufaa ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, nataka kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii tena leo kusimama mbele yenu kujibu maswali na kukupongezeni nyote mlioko hapa kwa kushuhudia mwaka mpya pamoja na wale wote ambao tunasaidia nao na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 79 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo;-

(a) Mhe. Spika, nina furaha kujibu swali hili muhimu lenye mvuto katika Baraza hili suala la *ICU*. Katika kutekeleza ahadi hiyo kuna hatua zilizochukuliwa na wizara zote mbili zinazohusika nazo ni Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa sehemu mbili tofauti.

(i) Kukamilisha makubaliano Kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Watu wa China juu ya ujenzi wa *ICU* mpya. Mkataba huo uliwekwa saini na Waziri wa Fedha tarehe 23/7/2011. Na Mtaalamu kutoka China atakuja wakati wowote nchini hivi sasa kufanya maandalizi ya ujenzi huo.

(ii) Kuifanyia matengenezo *ICU* iliyopo. Kwa pamoja Mawaziri hao, Makatibu Wakuu na Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja walikagua *ICU*, chumba cha Upasuaji, Kitengo cha dharura (*Emergency room*) na Wodi ya Wazazi. Baada ya kuiona hali halisi na matatizo yaliyopo na kwa ushauri wa daktari ambaye ndiye Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kipaumbele kilipewa mtambo wa hewa safi (*Centralized Oxygen)* kwa sehemu hizo na ndipo Wizara ya Afya ikatoa zabuni Novemba 2011, na uteuzi wa wajenzi na waleta vifaa vya *ICU* ulishafanyika na taarifa ya mahitaji kuhusu matengenezo yalifikishwa Wizara ya Fedha tarehe 17/11/2011 na nyaraka zote zinazohusiana na zabuni ziliwasilishwa tarehe 27/11/2011.

(b) Kutokana na maelezo haya ya kifungu (a) nathubutu kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar haijashindwa kuimarisha huduma hii kwenye Hospitali ya Rufaa ya Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami hii imekuwa ni kawaida kwa wakati wowote, maana yake haijulikani wakati gani sio *specific time* aliyotoa. Serikali imo mbioni matunda yake yataonekana hizi zimekuwa ndio kauli za manaibu waziri na mawaziri wanavyojibu sasa sijui mbio zimeanzia wapi na kumalizikia wapi, matunda yake yatakuwa lini na kupea lini, huu wakati sijui ni wakati gani.

(a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri tuna mkataba kati ya wizara yake na watu wa China, unaweza kutwambia ni lini itaanza shughuli hiyo.

(b) Kwa kuwa suala la *ICU* ni suala muhimu je hakuna haja ya kufikiria kupitisha harambee kuwashirikisha viongozi wetu, wafanyabiashara wetu na wananchi wenyewe waathirika wa hiyo *ICU* kama lilivyofanywa Kombe la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, anachokisema ni kweli *ICU* ni muhimu na nafikiri umuhimu wa *ICU* naweza nikaujua mimi zaidi ya yeye. Lakini suala la kusema tuko mbioni sikulitamka nilichokisema kwamba mkataba umeshatiwa tarehe 23/7/2011na wataalamu kutoka China wanakuja, hivyo ndivyo nilivyosema. Sasa watakuja lini wamekubaliana vipi, labda Waziri wa Fedha kwa sababu ndiye aliyetiliana mkataba pengine na Waziri wa Afya labda wanayo taarifa, lakini ninavyojua kwamba serikali hizo mbili zimetia mkataba na wakitia mkataba tabaan watakuja kufanya kazi.

Pili, ningependa kusema kwamba pendekezo alilolitoa sio baya, lakini sidhani kama Wizara ya Afya tena ikae kitako ifanye harambee, isipokuwa kama wameona kweli kuna umuhimu huo wafanyabiashara na watu wengine tukusanyike pamoja tufanye harambee tujenge *ICU*. Tutakushukuru ikiwa utafanya hivyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa kuwa hili ni Baraza la Wawakilishi na kwa kuna nia ya wajumbe ni kuwaona mawaziri wetu wanafanya kazi kwa ufanisi na wanafanikiwa, na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Wizara ya Afya aliwahi kusema kwamba, kama itafikia miezi sita hajafanya suala hili anaweza akaamua kujiuzulu, na kwa kuwa nia yetu sisi ni kwamba waendelee kufanya kazi kwa maslahi ya Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri haoni sasa ni wakati kwa sababu miezi ile inakaribia kumalizika akaona kuna haja ya kubadilisha kauli kidogo akaongeza siku mbele. Lakini pili sababu zipi za msingi ambazo zinapelekea Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha kuamua kutafuta mkandarasi na mkataba kwa fedha ambazo ni chini ya dola laki nne lakini mradi kama huu wa Wizara ya Afya kule Pemba ambao gharama yake ni dola laki nne hamsini elfu haukuingia kwenye *process* hizo za Wizara ya Fedha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza naomba na mimi kukupa kheri ya mwaka mpya na nilikuacha China ukifanyiwa matibabu kidogo nafurahi kwamba umerudi macho yako ni mazuri. Naomba kwa ruhusa yako kumsaidia Naibu wangu Waziri kumjibu Mhe. Hija.

Hapa kwa sababu ya unyeti wa suala lenyewe nimechukua na *hansard* sijasema baada ya miezi sita na naomba kama utaniruhusu noisome. Nilisema kwamba, “Kama mwaka huu wa bajeti utamalizika, kama Wachina hawatatengeza baada ya miezi sita serikali itakata pua ijenge wajihi’, serikali imeshakata pua kujenga wajihi na ujenzi utaanza wakati wowote kuanzia sasa. Kwa hivyo, sidhani kwamba nahitaji kubadilisha kauli yangu na sidhani kwamba kutakuwa na haja hiyo kwa sababu *ICU* inajengwa na itaendelea kujengwa kama tulivyoahidi. Namshukuru Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa mashirikiano makubwa aliyonipa kuweza kutekeleza ahadi hii.

Mhe. Spika, la pili sikulielewa vizuri alisema thamani yake dola 450,000. Zabuni ilionesha kwamba vitu viwili hivyo kutiwa *pipe* na *oxygen*. Kwa taarifa ya Waheshimiwa Wajumbe si *pipe* na *oxygen* kwenye *ICU* tu, tunatia *pipe* na *oxygen* kwenye *theatre* ya kinamama, *maternity*, chumba cha *emergency* na katika chumba cha *ICU*. Kwa hivyo, tunachofanya ni zaidi ya hapa kuliko kile tulichoahidi.

Kutia mtambo wa *oxygen* jana tulizungumza kwenye *brief*, ni kwamba hivi sasa akija mgonjwa kuna yale ma-*cylinder* yanayotumiwa kuchomea gari, akitokea mgonjwa anayetaka kutiwa *oxygen* inabidi uliburure lile kama unataka kwenda kuchoma kifaa cha gari, tukasema hili halistahiki. Kwa hivyo, baada ya mwezi Juni Mwenyezi Mungu akijaalia tukimaliza shughuli hii ni kwamba ile *system* kama tunavyotia mfereji kwenda msalani pale pwaa *oxygen* iko pale pale.

Gharama ya shughuli yote hiyo ni shilingi 894,162,750/= ambazo hizo ni dola laki 571,350 kwa shughuli zote mbili hizo. Serikali imekata pua imejenga wajihi kutoa fedha hizo kukabili suala hili.

Suala la kwamba mradi wa Pemba haukuingia sikulifahamu Mhe. Hija Hassan Hija naomba ulirudie.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali langu ni kwamba mradi wetu huu mkubwa wa *emergency, maternity ward* na *ICU* ni dola 500,000 kama nimemfahamu. Lakini mradi huu muhimu Wizara ya Fedha wameamua kuingia mkataba, maana yake kuna urasimu wa mkataba. Katika mradi wa dola 450,000 ni upungufu kidogo tu wa fedha hii lakini Wizara ya Fedha haikuona haja hiyo ndio swali langu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hapa na Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo atanisaidia kwa sababu huu mradi ulioulizwa kwamba haukutiwa mkataba unahusu fedha. Lakini sisi kabla ya ujenzi kuanza ambapo hivi sasa ndio tunkamilisha na hao waliopata zabuni tutatiliana mikataba. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha anaweza kunisaidia ile sehemu ya pili. Sisi tutatiliana mkataba na wazabuni watakaojenga *ICU* kabla ya kujenga.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija amezungumzia mradi wa Pemba lakini sijausikia mradi gani hasa anaoufanyia *reference*. Hata hivyo, si utaratibu kwa mujibu wa sheria za fedha, kwa mujibu wa sheria za manunuzi hatupaswi kutoa mradi wowote ule bila ya kutiliana saini. Ile inajengwa kwa kutumia mkopo au inajengwa kwa pesa za moja kwa moja.

Lakini baadae Mhe. Hija anisaidie anambie ni mradi gani halafu na mimi niweze kuufuatilia kuweza kuona ukweli wake.

Nam. 103

Sera za Uekezaji na Utalii

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:-

Kwa kuwa Sera za Uwekezaji katika Utalii zinaonekana kuwalinda na kuwavutia zaidi wawekezaji hao jambo linalopelekea kupotea kwa rasilimali zetu hususan rasilimali watu na rasilimali vitu, na kwa kuwa inaelekea pia kuwa sera hizo zilitungwa muda mrefu uliopita.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuzipitia upya sera hizo kwa maslahi ya Zanzibar na wananchi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 103 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, si kweli kwamba Sera ya Uwekezaji katika Utalii inawalinda wawekezaji. Aidha, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ipo haja ya kuipitia upya Sera ya Utalii kwa maslahi ya Zanzibar na wanachama wake.

Mhe. Spika, Sera ya Utalii Zanzibar ilianza kufanyakazi rasmi mwaka 2004 katika kipindi hicho kumejitokeza maendeleo makubwa katika sekta ya Utalii na hivyo marekebisho ya Sera ni kitu cha lazima. Wizara imeliona hilo na hivi sasa iko katika hatua za mwisho za kumaliza marekebisho ya Sera ya Utalii Zanzibar na tayari semina mbali mbali za kukusanya maoni ya wadau zimeshafanyika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake amesema kwamba sera iliyopo hivi sasa bado ipo na inawalinda hata Wazanzibari. Moja katika maeneo ya sera hiyo ni suala la kuhakikisha kwamba ajira katika sekta ya utalii zinawanufaisha Wazanzibari hasa kwa yale maeneo ambayo Wazanzibari wapo wenye ujuzi nayo na wanaweza kuzifanya.

Lakini mara nyingi tumeliuliza Baraza hili la Serikali limekiri kupitia Mawaziri wake kama kumekuwa na matatizo katika utekelezaji wa sera hii kwa wawekezaji kutozingatia kikamilifu katika kutoa ajira kwa nafasi hizo kwa watu ambao si Wazanzibari. Sijui wizara imejipanga vipi kuona baada ya kauli nyingi kama hivi suala hili linafanyiwa kazi na kuona kwamba nafasi za ajira katika sekta ya utalii ambazo Wazanzibari wanazimudu na wana ujuzi nazo

kama inavyoagiza sera iliyopo sasa ya utalii yansimamiwa na Wazanzibari wananufaika na utalii unaotumika katika nchi yao.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa hii ya kuweza kutoa ufafanuzi juu ya suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Spika, kwa faida ya Baraza hili kwanza tuelewe tu kwamba unapozungumzia uwekezaji katika visiwa hivi basi elekea *ZIPA* yaani Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Uwekezaji wa aina yoyote unahusiana na *ZIP*A isipokuwa uwekezaji huu una sehemu mbili. Tunapozungumzia uwekezaji ni kwamba sasa hivi tunaelekea zaidi katika sekta ya utalii na ndio hali halisi ilivyo. Kwa sababu hatuna masuala ya viwanda bado nchi yetu uwekezaji wake ni mdogo sana. Kwa hivyo, uwekezaji wake kwa zaidi labda ya asilimia 95 ni kwenye sekta ya utalii.

La pili tunapozungumzia uwekezaji yaani ukizidi zaidi ya shilingi3,000,000/= basi uwekezaji huo huwa unahusiana na *ZIPA* na uwekezaji ukiwa chini ya shilingi 3,000,000/= uwekezaji huo ndio Kamisheni ya Utalii ndio wanawajibika kusajili au kupitisha miradi hiyo.

Mhe. Spika, miradi hiyo tumepitisha mingi tu ni kama 175 ya wazalendo, tumepitisha kwa sababu haizidi zaidi ya shilingi 3,000,000/=. Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba uwekezaji wowote ule utakuta ni wawekezaji kutoka nje ndio wenye fedha bado sisi hatuna fedha. Lakini tukasema hapana ni lazima na wawekezaji wetu nao tuwape nafasi ya kuweza kuwekeza katika nchi yetu. Ndio maana tukatoa kiwango kidogo kwamba chini ya shilingi3,000,000/= basi wazalendo wanaweza wakawekeza. Tumefanya hivyo na tumepitisha miradi 175 kwa makusudi ili ku-*encourage local investing.*
Mhe. Spika, ndio maana wenzetu wa Seychelles waliona hata kama mradi umezidi zaidi ya asilimia basi mwekezaji wa nje lazima ashirikiane na mwekezaji wa ndani ili kuhakikisha kwamba fedha haziondoki zinabakia pale pale ndani ya visiwa. Kwa hivyo, sisi vile vile baada ya muda tutafanya hivyo kwamba wawekezaji wote lazima washirikiane na *local investors* ili kuhakikisha kwamba fedha inabakia hapa.

Kwa hivyo, kwa heshima ya Baraza hili lielewe kwamba uwekezaji hata kama ni wa utalii umezidi zaidia ya shilingi 3,000,000/=, ukizidi ni ZIPA, ukipungua ni Kamisheni ya Utalii.

Mhe. Spika, hapa niseme tu kwamba kwa kweli wawekezaji wa ndani tumewapa kipaumbele lakini kwa sababu ya uwezo wao tukasema hapana tuwawekee kiwango chao ili na wao wapate nafasi ya kuwekeza ndani ya visiwa hivi.

Mhe. Spika, suala la ajira ni kweli tumejaribu kulitazama ni kwamba ajira nyingi zaidi zinakwenda kwa watu kutoka nje ya visiwa vya Zanzibar na ndio maana tukasema kwamba lazima tukae kwa sababu haihusiani na sekta moja. Hii sekta ya ajira inahusiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwa hivyo, ni suala zuri mimi nitakaa na Waziri anayehusika ili kuhakikisha kwamba tunaibadilisha hii sekta ya ajira na tuone kwamba wale wanaohusiana na ajira wawe ni Wazanzibari kwa sababu wao ndio wanaohusika zaidi.

Kwa hivyo, hili ni suala la kukaa na waziri ili tuibadilishe na ilikuwepo lakini ikabadilishwa sijui kwa nini. Tuhakikishe kwamba ma-*PO* wote wa mahoteli wawe ni Wazanzibari kwa sababu wao ndio viranja wakubwa wa ajira. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu awe na subira na tutalishughulikia suala hili.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana yaliyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri na kusaidiwa na Mhe. Waziri nadhani suala la msingi ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka zaidi ni suala zima la ajira ambazo zimetolewa kwa watu ambao si Wazanzibari na pengine Wazanzibari wenyewe wana uwezo wa kufanya hivyo.

Mhe. Spika, napenda nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba wizara yangu tayari sera ya ajira tumeifanyia marekebisho na suala hilo tutaliweka wazi wazi katika sera yetu ya ajira. *(Makofi)*
Mhe. Spika: Naomba tukubaliane suala limeelezwa kwa mapana sana na kwa hiyo tuendelee.

Nam. 14

Kodi kwa Majengo ya Serikali

Mhe. Salma Mussa Bilal - Aliuliza:

Serikali hutoza kodi kwa majengo yake inayoyapangisha kwa wananchi ili kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina na matengenezo ya majengo hayo.

(a) Mhe. Waziri, ni kiasi gani cha fedha wanachodaiwa wapangaji hao wa nyumba za Serikali.

(b) Je, Hoteli ya Serena ambayo inaingiza mamilioni ya fedha inalipa kiasi gani kwa mwezi.

(c) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuwa kiwango kinacholipwa hivi sasa kwa wapangaji wa nyumba za Serikali kimeshapitwa na wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam**.** 14 lenye kifungu a, b na c kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali hutoza kodi kwa majengo yake inayoyapangisha ili kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Katika kukusanya kodi za nyumba wapo wapangaji ambao hawalipi kodi hivi sasa kwa madai ya kupewa nyumba hizo na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Wananchi wasiolipa kodi kwa madai hayo hivi sasa wanadaiwa jumla ya shilingi mia moja na arubaini na mbili, laki moja sitini na tisa elfu mia tatu na thalathini na tano milioni (T.Shs. 142,169,335/=).

(b) Hoteli ya Serena inalipa kodi ya shilingi milioni tano na laki tatu (T.Shs. 5,300,000/-) kwa mwaka na imeshalipa hadi 2011.

(c) Ni kweli tunakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kodi zinazolipwa sasa ni ndogo sana, lakini pia tunapenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi pamoja na Baraza lako Tukufu kuwa hivi sasa mapendekezo ya kodi mpya yapo tayari na yanasubiri kujadiliwa katika vikao husika kwa ajili ya kupata baraka kabla ya kuanza kutumika.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kiwango cha kodi kinacholipwa ambacho amekitaja Mhe. Waziri ni kidogo sana. Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba ipo haja ya kupanga viwango kwa asilimia kwa yale majengo yanayotumika kibiashara ili kuweza kuipatia serikali mapato zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kama nilivyojibu katika jibu mama kwamba kiwango kinachotozwa sasa hivi ni kidogo na wizara yangu inakaa na kulifanyia kazi suala hili na itakapomaliza tu basi kodi hii itakuwa katika kiwango kizuri ambacho kinakidhi kwa sasa hivi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009 inaonesha kwamba kuna madeni mengi sana yaliyorundikana katika majengo haya ya serikali. Katika

kadhia hiyo serikali iliunda tume maalum ya kushughulikia madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuchunguza na kuratibu kwa umakini zaidi suala hilo la umiliki pamoja na madeni.

Sasa kwa kuwa ni zaidi ya miaka mitatu tangu tume hiyo iteuliwe. Je, ni lini itamaliza kazi yake na kuikabidhi serikalini.

Mhe. Spika, swali (b) tume imechukua muda mrefu. Je, huoni kuwa tume hiyo kuchukua muda wote huo ni sawa na kusema kwamba imeshindwa kazi.

Lakini swali la mwisho ni nini hatima ya tume hiyo kazi yake pamoja na hatima ya madeni ya serikali ambayo ni sehemu ya fedha za umma katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli tume imechukua muda mrefu wa kulifuatilia suala hili. Lakini wakati wowote unapotaka kufanya haki lazima ufuatilie mpaka uthibitishe kile unachokifuatilia kiko katika misingi inayohitajika.
Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Mwakilishi avute subira na namhakikishia kwamba tume hiyo haijashindwa kufanya kazi zake isipokuwa inafanya kazi zake kwa juhudi na itakapokamilisha uchunguzi wake basi tutapata ripoti rasmi na uamuzi utachukuliwa kama vile unavyostahiki.

Mhe. Spika, kuhusu kodi za serikali ni kwamba bado tunaendelea kufanya utafiti wa kuzifuatilia kodi hizo na *inshaallah* zitalipwa kwa mujibu wa sheria inavyostahiki.

Nam. 22

Bidhaa kupanda Bei

Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza:

Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 Serikali haikuongeza ushuru wa bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje. Lakini kumekuwa na upandaji mkubwa wa bei za mchele, unga wa ngano na sukari. Kwa kuwa hakuna kodi iliyoongezwa ni sababu zipi zinazopelekea bei za bidhaa hizo kupanda.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nataka nikubaliane nae Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 serikali haikuongeza ushuru wa bidhaa za mchele, unga wa ngano na sukari zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, pia nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba kumekuwa na upandaji wa bei za bidhaa hizo. Mhe. Spika, kodi ni moja tu kati ya sababu zinazochangia bei ya mwisho ya bidhaa. Zipo sababu nyengine zinazopelekea kupanda kwa bei za bidhaa ikiwa ni pamoja na kubadilika kwa bei ya bidhaa yenyewe wakati inanunuliwa hadi wakati inakuja kuuzwa kwa mtumiaji ambapo mara nyingi huchangiwa na kubadilika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kulingana na dola za Kimarekani.

Mhe. Spika, pia kuna suala la gharama zinazotumika wakati wa utoaji wa mizigo bandarini pamoja na gharama za uchukuzi na usafirishaji mpaka madukani.

Kwa hivyo, ingawa hakukuwa na ongezeko la kodi lakini ongezeko la bei ya bidhaa ilisababishwa na sababu nilizozitaja hapo juu pamoja na kubadilika kwa thamani ya sarafu ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Kimarekani ambapo ilipanda kutoka 1,590 mwezi wa Julai mwaka jana hadi 1,780 kufikia mwezi wa Novemba mwaka jana. Ingawa hivi sasa thamani ya pesa za Tanzania inaonekana kupanda kidogo lakini bado haijafikia kiwango kile cha wakati Bajeti ya mwaka 2011/2012 inapitishwa.

Mhe. Spika, bei ya mchele katika soko la dunia imeonekana kupanda kutoka dola za Kimarekani 560 kwa mwezi wa Julai hadi sasa na kuwa dola 583 kwa tani.

Mhe. Spika, bei ya sukari imeonekana pia kupanda kutoka dola za Kimarekani 850 kwa tani mwezi wa Julai hadi kufikia 870 kwa tani hadi sasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake kwamba sababu zilizopelekea kupanda kwa bei za bidhaa ni nyingi na sio suala la kuongezeka kwa kodi tu.

Lakini kama tunavyojua hivi sasa si Zanzibar tu nchi nyingi duniani zimekumbwa na mitikisiko ya kiuchumi ambayo imepelekea kupanda kwa bei za bidhaa na kupelekea ukali wa maisha kuongezeka kwa wananchi. Serikali tofauti katika nchi tofauti zimechukua hatua mbali mbali za kuwapunguzia makali hayo wananchi wake. Sijui kwa upande wetu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa imefikiria kuchukua hatua gani ili pamoja na kutuongezea kodi, hii athari ambayo ameizungumza Mhe. Naibu

Waziri iweze kuwapungukia walaji ambao ni wananchi maskini wa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, suala la uagiziaji wa bidhaa na hasa za chakula ni suala ambalo limebinafsishwa na liko kwa wafanyabiashara binafsi. Hivyo, serikali kubwa itakaloweza kufanya ni kushughulika na suala la kodi na ndivyo inavyofanya na ndio maana utakuta kwamba ushuru kwenye bidhaa hizi za chakula umeondoshwa na katika mazao mengine ukaongezwa.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Naibu Waziri aliyatoa hatuoni kwamba umefika wakati kwa mara nyengine tena sasa kuweza kuangalia upya utaratibu wa hizi bei zinazopandishwa na hawa waletaji na wauzaji wa michele katika nchi yetu na kuwasaidia wananchi ambao hali zao ni za chini. Kwa sababu kwa mujibu wa maelekezo ya Mhe. Naibu Waziri mchele umeondoka kwa tani kutoka dola 560 mpaka dola 583, kuna ongezeko la asilimia ndogo sana hapo katika ununuzi na uuzaji wa mchele huu.

Lakini kiwango kilichokuwa kabla ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa wananchi wetu walikuwa wananunua mchele shilingi 1,100/= kwa kilo. Lakini sasa wananchi wale wale wananunua mchele kilo moja shilingi 1,600/= pengine na ushei. Je, ongezeko hili la asilimia ndogo ndio limesababisha hata wananchi waweze kununua mchele katika kiwango cha ghali kama hivi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, serikali katika kulitatua tatizo hilo imeandaa kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara kila pale haja inapotokea ya kufanya hivyo.

Mhe. Spika, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba bei hii inayotumika sasa hivi katika maduka ni bei ambayo kimsingi wizara imekaa na wafanyabiashara ili kuangalia kwamba wafanyabiashara wanapata faida stahiki lakini na watumiaji nao pia hawaonewi kwa kupandishiwa bei isivyokuwa kihalali.

Nam. 105

Bei na Matumizi ya Mwani

Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa wananchi wengi wa Wilaya ya Micheweni wanajishughulisha sana na upandaji wa mwani hasa akinamama. Kwa kuwa mpaka hivi sasa bado mwani haujawa na bei inayokidhi haja kwa wakulima hao. Kwa kuwa katika Bajeti iliyopita uliwaahidi wananchi kwamba utahamasisha matumizi ya mwani ikiwemo kutengeneza sabuni na usarifu mwengine kwenye matumizi ya vyakula mbali mbali.

(a) Ni sababu gani zinazopelekea zao la mwani kutokuwa na bei nzuri kwa wakulima.

(b) Kwa upande wa uhamasishaji wa matumizi ya mwani ni hatua ipi iliyotendeka kwa kipindi cha miezi sita iliyopita.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba wananchi waliowengi wa Wilaya ya Micheweni wanajishughulisha sana na upandaji wa mwani hasa akinamama. Nawapongeza wakulima wa mwani wa vijiji vya Kiuyu Mbuyuni, Tumbe na Wingwi katika Wilaya ya Micheweni kwa kuzalisha mwani mwingi zaidi katika Kisiwa cha Pemba.

i) Mwani unaolimwa kwa wingi hapa Zanzibar ni mwani aina ya *Spinosum* (mwani mwembamba) ambao katika soko la dunia hauna bei kubwa. Serikali imefanya utafiti wa mwani aina ya *Cotonii* (mwani mnene) ambao una bei nzuri katika soko la ulimwengu kuweza kulimwa hapa Zanzibar na matokeo yake ni ya kutia moyo.

ii) Wafanyabiashara wanaounua mwani wetu kwa muda mrefu wamekuwa wakihodhi soko la mwani na wamekuwa wakiwalipa wakulima wetu bei ndogo. Serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inatafuta soko la bei kubwa kwa wakulima wa mwani hapa Zanzibar. Wizara

inapongeza sana jitihada binafsi za Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuwatafutia bei nzuri wakulima wa mwani.

iii) Kutokuwepo kwa viwanda vya usarifu mwani hapa Zanzibar kunalazimisha nchi yetu kusafirisha mwani kwenda nchi za nje, mbako huko wanaufanya mwani wa Zanzibar kama mali ghafi ya viwanda vyao. Jitihada zinafanywa za kuwaomba wawekezaji wawekeze katika viwanda vya usarifu wa mwani na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wanaombwa tusaidiane ama katika kuwekeza au kuwashawishi wawekezaji waanzishe viwanda vya usarifu wa mwani.

iv) Kutokuwepo nchini matumizi makubwa ya mwani ndani ya jamii ya Wazanzibari. Jitihada zinafanywa kuangalia namna gani ya kukuza matumizi ya ndani ya mwani wa Zanzibar unaozalishwa ndani ya nchi yetu. Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Ubalozi wake mdogo uliopo Zanzibar, unapongeza kwa kuendeleza jitihada hizo.

(b). Mhe. Spika, kwa upande wa uhamasishaji wa matumizi ya mwani, hatua za kipindi cha miezi sita iliyopita ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wanajamii kwa kutumia wataalamu wetu kutoka Unguja na kushirikiana na wataalamu wetu walioko Pemba, mafunzo ya uimarishaji wa ubora wa mwani *quality maintaining.* Uhamasishaji wa mwani kwa ajili ya soko la ndani kama vile utengenezaji wa sabuni na utengenezaji wa vyakula na pia kikaushio cha mwani kinatolewa kisiwani Pemba. Mafunzo hayo yalianza kwa wazalishaji wakubwa wa mwani kisiwani Pemba katika vijiji vya Kiuyu Mbuyuni, Tumbe na Wingwi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umemalizika, Mhe. Waziri nakushukuru.

Kabla ya kuendelea nimeombwa nitowe taarifa kuwatangazia wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii,wakutane hivi punde katika chumba kile kile cha kawaida ambacho huwa wanakutana, kuna masuala muhimu ya kuzungumzwa huko. Kwa hivyo, tunaombwa twende huko. Tunaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi, kanuni ya 42 imeweka utaratibu wa hoja ya kujadili

jambo la dharura. Kwa ruhusa yako, haidhuru ni refu kidogo, naomba niisome ili nieleweke kile ambacho nataka kuliomba Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kanuni ya 42:-

Fasili ya kwanza inasema,

> "Baada ya muda wa maswali kwisha mjumbe yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Baraza liahirishe shughuli zake zilizooneshwa katika orodha wa shughuli za Baraza na lijadili jambo la dharura na muhimu kwa umma kwa ruhusa ya Spika".

Fasili ya pili inasema,

> "Hoja ya namna hiyo itakuwa ni maalum na haitatolewa wakati majadiliano yanaendelea kuhusu jambo jengine".

Fasili ya tatu inasema,

> "Hoja itatolewa na mjumbe kwa kusimama mahali alipo na kuomba idhini ya Spika, kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Baraza kwa madhumuni ya kujadili jambo la dharura na muhimu kwa umma".

Fasili ya nne,

> naomba hapo nitaparejea baadae inasema,
> "Kadiri inavyowezekana kabla ya kikao kuanza mjumbe atakuwa amewasilisha kwa Spika kwa maandishi maelezo ya jambo analopenda lijadiliwe".

Fasili ya tano inasema,

> "Endapo Spika ataliona jambo hilo ni la dharura na muhimu kwa umma, ataruhusu hoja hiyo itolewe na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda usiozidi saa moja".

Fasili ya sita inasema,

> "Hoja ya dharura haitoruhusiwa iwapo inahusu jambo ambalo taarifa ya hoja imeshatolewa au jambo ambalo limekwishawekwa katika orodha wa shughuli".

Naomba nichupe Fasili ya saba na ya nane, lakini Fasili ya tisa inasema,

> "Jambo linalotolewa kwa hoja chini ya kanuni hii litahisabiwa kuwa ni jambo la dharura iwapo,
>
> (a) Ni jambo mahususi.
> (b) Halikuwekwa katika lugha ya jumla au haligusii mambo mengi mbali mbali.

(c) Halikusudii kujadili habari zisizo na uhakika au habari ambazo ukweli wake hauwezi kupatikana.

(d) Linahitaji mazingatio ya haraka kiasi kwamba haliwezi kusubiri kushughulikiwa katika njia za kawaida katika siku za baadae na

(e) Limetokea siku za karibuni na limeletwa bila kuchelewa.

Fasili ya mwisho ya kumi ya kanuni hii inasema,

> "Kwa madhumuni ya kanuni hii jambo lolote litahisabiwa ni muhimu kwa umma iwapo litagusia maslahi ya nchi au wananchi wake na utatuzi wake utategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kiutawala peke yake". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, nimeomba ruhusa yako nitumie kanuni hii na ukiniruhusu kuomba uliruhusu Baraza lako kujadili kwa muda huo usizidi saa moja, suala ambalo limejitokeza jana katika vyombo vya habari na ambalo limeonekana kuwagusa na kuwashtua wananchi wengi wa Zanzibar na ambalo wao kama wananchi wa Zanzibar hawajapata taarifa kabla. Nimesema pale kabla Mhe. Spika, kwamba ile fasili ya nne imetaka kadiri inavyowezekana kabla ya kikao kuanza mjumbe atakuwa amewasilisha kwa Spika, kwa maandishi maelezo ya jambo analopenda lijadiliwe. Bahati mbaya hiyo kadiri inavyowezekana imenishinda Mhe. Spika, kwa sababu ya mazingira ya suala lenyewe lilivyoibuka. Naomba nilieleze na ikiwa wa hekima zako utaona linafaa tulijadili kwa saa moja, laa ukiliona halifai nitakubali maelekezo ya kiti chako.

Mhe. Spika, suala lenyewe ni; jana katika vyombo vya habari tumesoma juu ya taarifa iliyotolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anaitwa Professor Annet Baijuka, juu ya maombi ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewasilisha Umoja wa Mataifa, kutaka kuongezewa eneo la bahari kuu, yaani *exclusive economic zone*.

Sasa kabla sijaelezea yale ninayotaka kuliomba Baraza Mhe. Spika, niombe tu ruhusa yako kwamba utaruhusu suala hili lijadiliwe, basi nitowe ile hoja yangu kwa ufupi kabisa na mahususi kama kanuni inavyotaka, naomba jambo moja tu kwa Baraza, kwa wababu kama unavyokumbuka Mhe. Spika, suala la *exclusive economic zone*, lilikuwa ni katika maeneo matatu ambayo Baraza lako lilipitisha azimio, wakati likijadiliwa suala la mafuta tarehe 08/04/2009. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli kanuni inaruhusu kukiwa na jambo la dharura la aina hiyo, lenye umuhimu mkubwa kuweka utaratibu wa kuliangalia na kulijadili suala hilo ili kufikia pahala pazuri. Asili ya suala

lenyewe kama alivyolieleza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ni suala kubwa na ni muhimu ambalo lingefaa kutafakariwa kwa kiasi kikubwa.

Nafikiri sio jambo jepesi sana kulitolea hoja haraka katika chombo hiki katika muda huu, ni jambo ambalo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama lilivyo nukuliwa katika magazeti mbali mbali hayo, hapa sinayo, lakini linagusa kama lilivyo suala la Muungano ambapo pande mbili za Muungano zinahusika. Ukilitizama suala lenyewe ni muhimu kama ulivyoeleza sikatai kabisa, lakini sina uhakika kwa kiasi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejihusisha na suala hilo.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani ili kufikia pahala pazuri kwa maoni yangu, jambo hili ingefaa tukajua sio tu kupitia wizara inayohusika na waziri wake, kwa bahati mbaya hivi sasa ametoka nje pengine angeweza kutupa taarifa kidogo. Lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipangaje, wameshauriana nini juu ya jambo hilo kiasi cha kufikia waziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia hatua ya ombi hilo, kumekuwa na mawasiliano gani. Nadhani hayo ni mambo ambayo kwa hoja ya haraka, nina mashaka halitaweza kutoa picha nzuri kwa manufaa ya serikali zaidi hapa niseme Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa manufaa ya wananchi.

Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwamba hebu serikali, suala alilolizungumza mwenzetu ni muhimu, tulione suala hili na mtupatie mwelekeo, njia na taarifa juu ya vipi pande mbili za Muungano tulifikia juu ya suala hilo mpaka kufikia nafasi ya kwamba Mhe. Waziri mmoja wapo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupeleka ombi katika Jumuiya ya Kimataifa ili kuongezewa eneo.

Eneo ambalo lina umuhimu mkubwa sana katika masuala ya kiuchumi. Ningefurahi zaidi kwa niaba ya Baraza hili, lakini pia kwa niaba ya wananchi wote wa Zanzibar, serikali ikawa imejipanga vizuri na kujua kwa kiasi gani wameelewana pande mbili za Muungano juu ya jambo hilo.

Kwa hivyo, kwanza nichukuwe nafasi hii kukupongeza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa kutanabahisha chombo hiki cha wananchi, lakini pia kuiarifu serikali kuwa kuna jambo hilo ambalo ni jambo kubwa na linafaa kuzingatiwa ili hatimaye kupata taarifa juu ya makubaliano yaliyokuwepo juu ya taarifa ya ombi hilo.

Nashauri hivyo na pengine itakuwa ni haraka mno kuweza kutoa hoja hapa katika kipindi kifupi hicho. Nataka niishie hapo, isipokuwa kama serikali ina taarifa inataka itowe juu ya hili hivi punde basi naweza kuruhusu taarifa hiyo ikatolewa, lakini hatimaye tuone tunafanya nini juu ya jambo hilo.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea hebu tusikie taarifa kwa upande wa serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu. Aidha, nichukuwe nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa kututanabahisha jambo muhimu lenye maslahi ya nchi yetu.

Ninachoweza kusema mbele yako Mhe. Spika, ni kwamba ushauri wako tumeupokea na tumesikia kauli ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, hivyo tutawasiliana na Mhe. Jussa ili jambo hili tulipate zaidi kwa undani, tushauriane vizuri na baadae serikali itatowa kauli yake hapo kesho. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana, kila wakati busara na hekima zako zinatupa imani kwamba huwa hatufanyi makosa kukuchagua kuwa kiongozi wetu katika muhimili huu muhimu wa dola.

Mhe. Spika, sina matatizo na ushauri wako na maelezo ya serikali, lakini wasi wasi wangu na ningeweza kulileta kwa utaratibu wa kawaida, lakini labda nieleze ule wasi wasi wangu halafu tena tutaona tukubaliane vipi.

Mhe. Spika, ile kanuni niliyoisoma kwenye fasili ya kumi inazungumzia kwamba “kwa madhumuni ya kanuni hii jambo lolote litahesabiwa ni muhimu kwa umma iwapo litagusia maslahi ya nchi au wananchi wake na utatuzi wake utategemea hatua zaidi kuliko zile za kiutekelezaji wa kiutawala peke yake.

Sasa Mhe. Spika, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya jana na kwa mujibu hata wa taarifa nilizozifuatilia baadae katika mtandao, ombi hili linawasilishwa leo. Bila shaka kwa mujibu wa mpishano wa masaa, itakuwa bado kwa wao saa hizi bado wamelala kwa kule inakopelekwa New York. Lakini nilikuwa napata wasi wasi mmoja tu, kwa sababu sijui utaratibu wake ukoje kule.

Lakini hofu yangu mimi ni kwamba likipelekwa na ikiwa litaamuliwa na hata tukija kutoa taarifa hapa, kwa sababu likiamuliwa likiingia katika sheria za kimataifa litaongeza matatizo zaidi. Ndio maana nilitaka nilitanabahishe Baraza ili lilione hili halafu tuone tutafanya nini kwa sababu moja tu Mhe. Spika. Kwa sababu hiki chombo ili kiheshimiwe na wananchi kwa sababu ni chombo kikubwa sana, ni lazima yale maamuzi yaliyopitishwa nayo yasimame na yasimamiwe. Kama maamuzi yaliyopitishwa hapa yakionekana kama vile tunapitisha hapa halafu siku ya pili tunayasahau au baada ya mwaka mmoja yawe hayana nguvu tena, basi wananchi watakuja kukitoa maanani chombo hiki jambo ambalo Mhe. Spika, litatufikisha pahala pabaya sana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nimekumbusha katika yale maazimio ya tarehe 08/04/2009 ambayo yanapatikana katika Hansard. Suala la *exclusive economic zone* liliamuliwa kabisa kwamba nalo kusiwe na ushirikiano Zanzibar isimamie wenyewe mamlaka yale. Sasa hofu yangu ni kwamba tunaweza kama ulivyopendekeza kwamba serikali ilete maelekezo katika suala hili, lakini je ikiwa maelezo yatakuja wakati Umoja wa Mataifa umeshachukua hatu ya kukubali mapendekezo yaliyopelekwa na kwa mujibu wa taarifa hizi, maeneo yaliyotajwa ni pamoja na maeneo yanayozunguka visiwa vya Pemba, Unguja na mpaka kwenda chini Mafya huko. *Exclusive economic zone* Mhe. Spika, kama tunavyojua ni eneo ambalo ni haki ya ile nchi iliyopakana nayo.

Kwa hivyo, kwa upande wa Jamhuri ya Muungano upande huu wa mashariki wa visiwa ni eneo ambalo lingekuwa la Zanzibar. Sasa kwa sababu Baraza lako lilikwishapitisha azimio kwamba suala hili lisimamiwe na Serikali ya Zanzibar na ikiwa Umoja wa Mataifa ukija ukitoa haki hiyo kwa Jamhuri ya Muungano, yametajwa na masuala mengine ni pamoja na masuala ya kutafiti mafuta, sijui itakuja kusimama wapi maamuzi ya Baraza lako limepitisha. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sina pingamizi na maelekezo yako, lakini *concern* yangu ni hiyo tu kwamba je hatutokuja kufika pahala tukajakuletewa taarifa wakati maamuzi yameshafanyika. Umesema serikali ije itueleze kama imeshirikishwa, pengine hata kama imeshirikishwa na ikiwa imebariki haitakuwa imekiuka ile azimio la Baraza ambalo lilitaka suala hili lisimamiwe na Zanzibar peke yake, huo ndio wasi wasi wangu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nataka kusema kwamba nia yangu ni njema na ninataka kuheshimu nafasi ya chombo hiki na maamuzi tuliyofanya, kwa sababu kama nilivyosema tukija kufika pahala wananchi wakija kuona maamuzi tunayofanya hatuyasimamii basi chombo hiki kitakuja kupoteza hadhi mbele ya wananchi wetu Mhe. Spika, ahsante. *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niendelee kumshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Hofu yake inatuambia basi suala hili serikali tulifanyie kazi haraka iwezekanavyo. Sasa naomba nitowe maelekezo hayo kwa serikali kwamba jambo hili tulifanyie kazi haraka iwezekanavyo kabla maamuzi ya Jumuiya ya Kimataifa hayajatolewa.

Baada ya mashauri hayo, kuna taarifa nyengine juu ya hili. Taarifa.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, imebidi nisimame kidogo. Muongozo ulioutoa ni sahihi na suala hili Mhe Spika, kweli tulilijadili na wewe mwenyewe ulilionga Baraza siku hiyo. Ulikuwa mjadala mrefu sana na wewe ukatoa wazo, mambo matatu yalikuwa, kwamba kila jambo

tulizungumze na tulipigie kura. Kwa hivyo, suala hili katika mapendekezo lilikuwa tushirikiane, lakini katika mjadala wa Baraza tukaamua suala hili tusishirikiane liwe letu. Wewe mwenyewe ulilliongoza Baraza, kila jambo katika yale matatu ulitaka tulipigie kura. Kwa hivyo, azimio la Baraza lilitoka hivyo. Sasa kwa tabia ambazo tumeziona mara nyingi, kuna sisemi dharau, lakini maazimio ya Baraza tunavyoyatoa yanakua na tabu sana kupatikana ufumbuzi wake kwa wenzetu.

Kwa mfano suala la mafuta, Baraza lako tukufu lilitoa azimio lake lakini mpaka leo kimpya. Kwa hivyo, ningeomba Baraza hili wengi ni wapya, lile azimio la Baraza lililotolewa wakati ule, ningeomba afisi yako ligawe kwa wajumbe ili wapitie na serikali iangalie haraka. Lakini ombi langu kwanza wajumbe wajuwe kuwa hii kitu ni nini. Wengi wajumbe hapa hawakuwepo, kwa hivyo ningeomba afisi yako itowe lile azimio ligaiwe kwa wajumbe wasome ili wajuwe na serikali haraka sana jambo hili walifanyie kazi kama ulivyoagiza Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri jambo hili ni zuri na hasa kwa kuwa Baraza hili ni jipya na jambo hili liliamuliwa katika Baraza lililopita la saba, basi nakubali ombi hilo, sekreterieti mtatoa hilo azimio ili Waheshimiwa Wajumbe wote wawe nalo na litasaidia katika kulifanyia kazi jambo hili ambalo mwenzetu Mhe. Jussa ametutanabahisha. Nadhani tuitowe hiyo na kwa sababu ni kitu ambacho kiko katika mamlaka ya Baraza, basi wajumbe wote tuwasambazie na litasaidia kwenda pamoja na jambo hili ambalo Mhe. Jussa ametuelekeza. Ahsante.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ulipaji Mafao ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa Namba 4 ya mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa Namba 6. ya mwaka 1999 na Kutunga Sheria Mpya ya Maslai na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu pamoja na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana, naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kwa madhumuni ya kupokea na kujadili na hatimaye kupitisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Namba 4. ya mwaka 1988 na Sheria Namba 6 ya mwaka 1999 na Kuanzisha Sheria Mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wote mmeupata mswada mpya baada ya ule wa mwanzo ambao tuliugawa katika kipindi kilichopita. Sasa naomba ule wa mwanzo tuusahau kabisa na tuushughulikie ule mpya na pamoja na marekebisho ya serikali ambayo tumeyasambaza leo. Sasa yale marekebisho ya serikali ndio muhimu sana ambayo tumeyasambaza leo. Baadae nitawachukua kwenye jadweli lile kifungu kwa kifungu. Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuupate ule mswada mpya ambao tuliugawa ambao uligaiwa kabla ya kikao hiki na marekebisho ya serikali ambayo yamesambazwa hii leo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hapa tukiwa wazima na afya njema. Kwa aina ya pekee nachukua fursa hii kukushukuru sana wewe Mhe. Spika kwa miongozo na ushauri wako ulioutoa katika matayarisho ya mswada huu.

Aidha, naishukuru Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura, kwa kuwa nasi kwa ukaribu sana kwa ushauri walioutoa ili kufanya mswada huu kuwa bora zaidi.

Mhe. Spika, vile vile naomba kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi hasa kwa maoni mliyotupa wakati wa semina na hata nje ya semina. Vile vile na wadau wengine mbali mbali waliotoa maoni na kuuchangia mswada huu kupitia vyombo mbali mbali.

Mhe. Spika, naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba serikali imeyazingatia kwa makini maoni yote yaliyotolewa na wadau mbali mbali katika kuufanya mswada huu kuwa bora zaidi. Pia serikali imezingatia kifungu nambari 11 cha sheria nambari 4 ya mwaka 1988 inayokataza mafao ya viongozi wakuu wa kitaifa kuyapunguza kinyume na sheria iliyowekwa. Tumejitahidi kutoa *photocopy* zile sheria mbili za zamani ziko njiani wakati wowote zitakuja itabidi tuzifuate katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Naomba radhi Mhe. Spika kwa hilo.

Aidha, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein katika hotuba yake ya kusherehekea Mapinduzi ya Zanzibar aliyoitoa katika kiwanja cha Amani, alisisitiza haja ya serikali katika kuwaenzi na kuwatunza viongozi wastaafu, katika hotuba hiyo Mhe. Rais alieleza nia ya serikali ya kuwasilisha mswada huu katika Baraza la Wawakilishi ili kuendana na marekebisho ya 10 ya katiba.

Madhumuni na Sababu ya Kutayarisha Mswada huu. Mhe. Spika, madhumuni na sababu ya mswada huu ni kuwasilisha mapendekezo ya kufuta sheria nambari 4 ya mwaka 1988 yanayohusu malipo ya kustaafu kwa viongozi maalum wa kitaifa na sheria nambari 6 ya mwaka 1999 inayohusu malipo ya kustaafu kwa viongozi wa kisiasa na kuweka sheria moja inayozingatia mafao ya viongozi wa kisiasa.

Mhe. Spika, umuhimu wa kuzifuta sheria hizo umekuja baada ya kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

1. Kuweka sheria moja ambayo itasimamia malipo ya mafao kwa viongozi wa kisiasa pamoja na utaratibu wa kuwalipa wategemezi wao kwa vipindi tofauti.

2. Marekebisho ya 10 ya katiba ya Zanzibar yameondosha nafasi ya waziri kiongozi na kuweka makamu wawili wa Rais wa Zanzibar. Hivyo kuwepo Makamu wawili wa Rais wa Zanzibar, hivyo kuwepo haja ya kuzingatia mafao ya viongozi hao na kuweka utaratibu wa kuendelea kuwatunza waziri kiongozi wastaafu.

3. Kumjumuisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika orodha ya viongozi wa kisiasa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 43(3) na 55 cha Katiba ya Zanzibar mwaka 1984.

4. Kufanya mapitio ya utaratibu wa kulipa mafao ya kustaafu kwa baadhi ya Viongozi wa Kisiasa hasa kwa kuzingatia marekebisho ya mishahara.

5. Kuwaingiza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Orodha ya Viongozi wa Kisiasa na kuweka utaratibu wa kulipa mafao yao.

Mswada wenyewe wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi mwaka 2012.

Mhe. Spika, mswada wenyewe wa sheria nilioutaja hapo juu sasa utakuwa na vifungu 25 badala ya 24 vilivyomo ndani ya Gazeti Rasmi la Serikali. Kuongezeka kwa vifungu hivyo kunatokana na kuongezeka kifungu kipya cha 16 katika Jaduweli la Marekebisho kinachosomeka “Huduma za Wategemezi”. Aidha kifungu 10(3) na 12(3) vilivyomo katika mswada vimefutwa kama vilivyooneshwa katika Jaduweli la Marekebisho.

Mhe. Spika, mswada huu sasa utakuwa na Sehemu Tano na Majaduweli Manne.

Sehemu ya Kwanza Utangulizi na ina vifungu vinavyoeleza jina fupi la sheria, kuanza kutumika kwa sheria, ufafanuzi wa baadhi ya maneno.

Sehemu ya Pili Mhe. Spika, sehemu hii inaanzia kifungu cha 4 hadi 8, ina vifungu vinavyoelezea stahiki za kulipwa mafao, masharti ya kutokuwa na sifa ya kulipwa mafao, mamlaka husika. Kuhusu mamlaka husika hapa tunakusudia:

(a) Kwa madhumuni ya vifungu vinavyohusiana na kulipa mafao kwa Rais Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu, maana yake ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na hiyo ndio mamlaka husika.

(b) Kwa madhumuni ya vifungu vinavyohusiana na kulipa mafao kwa Mwanasheria Mkuu Mstaafu, Mawaziri Wastaafu, Naibu Mawaziri Wastaafu pamoja na Washauri wa Rais, maana yake ni Katibu Mkuu mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma.

(c) Kwa madhumuni ya vifungu vinavyohusiana na kulipa mafao kwa Spika Mstaafu, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Mstaafu, maana yake ni Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Vile vile kifungu hiki kina kifungu kinachoonesha kupokea mafao kwa utaratibu mwengine na mwisho Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, Sehemu ya Tatu inaanzia kifungu cha 9 hadi 16, kwenye mswada huu uliosambazwa utaona umeishia 15 na sasa tumeongeza kifungu 16. Kwa hivyo, kifungu cha 16 sasa kitakuwa 17 na tutarekebisha mpaka tumalize cha 25.

Hivyo, Sehemu ya Tatu kama nilivyosema inaanzia kifungu cha 9 hadi 16 ambacho ni kipya. Vifungu hivi vinaeleza mafao ya Rais Mstaafu, mafao ya Warithi wa Rais Mstaafu, mafao ya Makamu wa Rais Mstaafu, mafao kwa Warithi wa Makamu wa Rais, mafao kwa Spika Mstaafu, mafao kwa Warithi wa Spika Mstaafu na kusita kulipwa mafao maalum na mwisho Huduma za Wategemezi.

Mhe. Spika, Sehemu ya Nne inaanzia kifungu cha 17 hadi 18 na ina vifungu vinavyoeleza mafao kwa viongozi wengine wanaoshikilia Ofisi za Kisiasa, pili kwa Viongozi wengine wanaoshikilia Ofisi za Kisiasa kama nilivyosema Mwanasheria Mkuu, Waziri, Naibu Waziri, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Mshauri Maalum wa Rais.

Sehemu ya Tano inaanzia kifungu cha 19 hadi 25 na vifungu vyenyewe vinaelezea ugawaji wa mafao kwa warithi, mazingatio ya kuweka asilimia maalum, kanuni, kufuta na kubakiza sheria, marekebisho ya jaduweli, mkopo kwa kiongozi wa kisiasa, mafao kwa Mjane wa Kiongozi wa Kisiasa na mwisho kuna majaduweli manne.

Majaduweli hayo yanaonesha utaratibu. Jaduweli la kwanza mafao anayostahili kulipwa Rais Mstaafu, Jaduweli la pili linaonesha mafao anayostahili kulipwa Makamu wa Rais Mstaafu, Jaduweli la tatu linaonesha mafao anayostahili kulipwa Spika Mstaafu na mwisho *Formula* ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa na sasa ni Jaduweli la Marekebisho.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba serikali imefanya marekebisho makubwa baada ya michango pamoja na maoni yenu Waheshimiwa Wajumbe tumeyazingatia na tumetafakari na ndio maana tukaja na marekebisho haya. Marekebisho haya tunahisi ni ya msingi ya mswada huu ambayo yameingizwa katika Jaduweli la Marekebisho kwa kufuata kifungu cha 83(2)(a) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ambacho kinaturuhusu kama serikali kuleta marekebisho hayo ya mswada. Marekebisho yenyewe ni kama yafuatayo:-

Mhe. Spika, kama nilivyosema tumetoa haya marekebisho na sasa tutayapitia moja baada ya jengine.

Kwanza kifungu cha 2 kinarekebishwa kwa kuongezwa tafsiri ya neno Spika, yaani neno Spika pale lilisahauliwa, kwa sababu kuna Spika Mstaafu, lakini Spika mwenyewe hayupo. Kwa hivyo, tunamuongezwa kwenye orodha Spika, maana yake Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Kifungu cha 10(3) Mhe. Spika, kifungu hiki kinasomeka kabla ya marekebisho “Endapo Rais Mstaafu atafariki watoto wake waliochini ya umri wa miaka 18 watastahiki kulipwa pencheni ya kila mwezi iliyosawa na kima cha chini cha mshahara wa Mtumishi wa Umma, ikizingatiwa kwamba malipo ya pencheni yanayolipwa kwa watoto kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 3 cha kifungu hiki yatasita endapo watatimiza umri wa miaka 18 au ikiwa ni watoto wa kike pale watakapoolewa au lolote litakalotokea”.

Mhe. Spika, kwa maoni yenu Waheshimiwa Wajumbe, serikali imeamua kukifuta kabisa kifungu hiki cha 10(3).

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho tumefanya marekebisho ni 12(3) ambacho naomba nikisome kabla ya marekebisho kilikuwa kinasomeka kwamba “Endapo Makamu wa Rais Mstaafu atafariki watoto wake waliochini

ya umri wa miaka 18 watastahiki kulipwa penchini ya kila mwezi iliyosawa na kima cha chini cha mshahara wa Mtumishi wa Umma, ikizingatiwa kwamba malipo ya pencheni yanayolipwa kwa watoto kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 3 cha kifungu hiki yatasita endapo watatizima umri wa miaka 18 au ikiwa watakuwa watoto wa kike pale watakapoolewa au lolote litakalotokea mwanzo". Kifungu hiki nacho serikali imeamua kukifuta kabisa.

Sasa tunakwenda kwenye kifungu cha 14. Mhe. Spika, kifungu hiki kinarekebishwa kwa kukifanya kifungu cha 14(1) na pili kuongeza kifungu kipya cha 2 ambacho sasa kitasomeka kama ifuatavyo:-

> "Endapo Spika Mstaafu atafariki basi Mjane wake atastahiki kulipwa na mamlaka husika na pencheni ya kila mwezi kwa miaka mitatu itakayokuwa sawa na asilimia maalum ya mshahara wa Spika ambaye huko madarakani".

Mhe. Spika, marekebisho mengine yako kwenye kifungu 16. Kifungu hiki ni kipya, yaani kinaongezwa kifungu kipya kama nilivyosema cha 16 baada ya kifungu cha 15 na vifungu vilivyobaki vimebadilika nambari kwa mtiririko wa vifungu vilivyopo na baadaye tunabadilisha tu mpaka kifungu cha 25.

Kifungu hiki Mhe. Spika, Huduma za Wategemezi, yaani watoto wale, endapo Rais, Makamu wa Rais au Spika wa Baraza la Wawakilishi wakati akiwa madarakani, mtoto au watoto wao watahudumiwa na mamlaka husika hadi watakapotimia umri wa miaka 20 ama ikiwa mtoto wa kike pale atakapoolewa au lolote litakalotokea mwanzo.

Mhe. Spika, marekebisho mengine ambayo tumeyafanya ni kifungu 17(2) hivi sasa kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

> "Kiongozi anayeshika Ofisi ya Kisiasa atakapomaliza muda wake wa kazi atalipwa Kiinua Mgongo sawa na asilimia maalum ya mshahara wa mwisho aliopokea zidisha na miezi aliyotumikia nafasi hiyo".

Mhe. Spika, marekebisho tuliyoyafanya kifungu cha 17 kama kilivyorekebishwa, kinarekebishwa katika kijifungu cha 2 kwa kufuta maneno "sawa na asilimia maalum ya mshahara wa mwisho zidisha na miezi aliyotumikia nafasi hiyo" na badala yake kuweka maneno "kama ilivyoelezwa katika Jadweli Nam. 4 la sheria hii", yaani jadweli la mwisho.

Kifungu cha 17 kama kilivyorekebishwa, kinarekebishwa katika kijifungu cha 4 kwa kufuta maneno ambalo litakuwa "sawa na asilimia maalum ya mshahara wa mwisho zidisha na miezi 24".

Kwa hivyo, baada ya marekebisho kifungu hicho 17(2) sasa kitasomeka kama ifuatavyo:-

> "Kiongozi Anayeshika Ofisi ya Kisiasa atakapomaliza muda wake wa kazi atalipwa Kiinua Mgongo kama ilivyoelezwa katika jaduweli Nam. 4 la sheria hii, mbali na Kiinua Mgongo Kiongozi Anayeshika Ofisi ya Kisiasa atalipwa posho la kumaliza muda wa utumishi kama ilivyoelezwa katika jaduweli Nam. 4 la sheria hii".

Marekebisho mengine Mhe. Spika, yako kwenye kifungu cha 20. Kifungu hiki kama kilivyorekebishwa hivi sasa kitakuwa kama ifuatavyo:-

Kukifanya Kifungu cha 20(1) na cha pili kuongeza kijifungu kipya cha 2. Sasa itasomeka kama ifuatavyo:-

"Rais ataweka asilimia maalum katika kifungu cha 17 kwa kushauriana na Spika wa Baraza la Wawakilishi na Makamu wa Pili wa Rais. Waheshimiwa Wajumbe wakati ule tunakumbuka kwamba tulisema kama itakavyoamuliwa na Rais.

Sasa serikali imesikia maoni yenu na imetafakari, tukaona hapa Barazani Mhe. Spika ambaye ndiye kiongozi, katika hayo mashauriano basi na yeye awepo kwa kushirikiana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye Kiongozi Mkuu wa Shughuli za hapa Barazani. Kwa hivyo, ile *element* ya ushauri tunahisi itakuwepo kama ilivyo hivi sasa, maana yake hivi sasa huo ndio utaratibu unaotumika".

Jadweli la Nne chini ya kijifungu cha 16(5). Mhe. Spika, kifungu hiki kinarekebishwa kama ifuatavyo:-

"Maneno chini ya kijifungu cha 16(5) yasomeke chini ya kijifungu cha 16 na ile kwenye mabano 5 tuiondoe. Kwa hivyo, itasomeka baada ya marekebisho chini ya kijifungu cha 16. Pili kufuta maneno mfano (Kiongozi wa Kisiasa ametumikia nafasi ya Utumishi wa Kisiasa miaka 3 na miezi 6, mshahara wa mwisho ni shilingi 100,000/= na Kiinua Mgongo ni X *percentage* zidisha 100,000 X 42 na posho na kumaliza muda ni X *percentage* X 100,000 X 24 X 4 ÷ 5". Kwa hivyo, kifungu hiki chote tunakiondoa.

Mhe. Spika, haya ndio marekebisho ya msingi ambayo serikali tumehisi na tumekubali kuyaondoa baada ya fikra na michango ya Waheshimiwa Wajumbe waliyotushauri.

Kwa hiyo, Mhe. Spika pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo yangu haya niliyoyatoa hapa juu naomba sasa kuchukua fursa hii kukushukuru kwanza Mhe. Spika binafsi, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako, Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa) kwa kutusikiliza kwa makini wakati wote.

Vile vile natanguliza shukurani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wote ambao watapata fursa ya kutoa michango yao na hatimaye kutushauri ipasavyo na kuweza kuupitisha mswada huu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kusoma muhtasari wa Taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi juu ya Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote, nataka kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kukutana hapa mbele ya Baraza lako tukufu tukiwa wazima kabisa wenye afya njema, ili kujadili mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu pamoja na mstakbali mzima wa wananchi wetu. Ikiwemo ya kupitisha miswada mbali mbali ukiwemo mswada uliopo mbele yetu, Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Baada ya Kustaafu pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu tena kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili niweze kuwasilisha Muhtasari wa Taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi juu ya mswada niliyokwisha uanisha hapo juu.

Mhe. Spika, pia naomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Kamati nitoe shukrani za dhati kwa serikali kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza

la Mapinduzi kwa kutuwasilishia mbele ya Kamati Mswada huu na kuweza kuujadili kwa kina na uwazi.

Vile vile, kwa niaba ya Kamati nitakuwa mwizi wa fadhila nisipoishukuru ofisi hii kwa kuamua kutuandalia semina iliyotoa fursa kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kuujadili na kutoa maoni yao juu ya mswada huu.

Mhe. Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii, niwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati yetu kwa michango yao muhimu wakati tulipoujadili mswada huu siku ya tarehe 3/10/2011, 4/10/2011, 18/10/2011, 9/01/2012 na 10/01/2012. Naomba niwataje wajumbe wanaounda Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid - Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohammed Ali - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Jecha Simai - Mjumbe
8. Ndg Ramadhan Khamis Masoud - Katibu,
9. Nd, Rahma Kombo Mgeni - Katibu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati yangu kwa kiasi inapongeza hatua zilizochukuliwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufanya marekebisho yaliyotokana na maoni ya Kamati. Hata hivyo, baadhi ya marekebisho hayo hayajakidhi haja kutokana na kutofanyiwa kazi kama kamati ilivyoagiza ambayo ni muhimu kwa mstakbali mzima wa maendeleo ya nchi yetu. Baadhi ya marekebisho hayo ni kama yafuatayo:-

Sehemu ya Kwanza ya Mswada

a) Mhe Spika, Sehemu ya Kwanza katika kifungu cha 3 kinachoelezea tafsiri ya maneno “Asilimia Maalum”, kamati iliagiza maneno haya yafutwe na neno “Mshauri Maalum wa Rais” pia kamati iliagiza litolewe katika tafsiri ya “Kiongozi wa Kisiasa” na “Ofisi ya Kisiasa”, kutokana na sababu zifuatazo:-

    i) Neno “Asilimia Maalum” iliagizwa na kamati kufutwa katika kila sehemu iliyojitokeza katika mswada huu, kwa sababu katika zama hizi za demokrasia na utawala bora, panahitajika uwazi katika utekelezaji wa sheria zote hasa

kutokana na uzito wa suala hili la hatma ya malipo ya mafao ya viongozi wa kisiasa .

Hivyo kamati inashauri utaratibu wa sasa wa Sheria Namba 6 ya mwaka 1999, uendelee kufanya kazi. Kwa utaratibu wa Viinua Mgongo na Posho la Kumalizia Muda, hasa ukizingatia wao baada ya kulipwa Kiinua Mgongo hawatokuwa hata na pencheni.

Sehemu ya Pili ya Mswada

ii) Neno "Mshauri Maalum wa Rais" iliagizwa na kamati kutolewa katika tafsiri ya "Kiongozi wa Kisiasa" na "Ofisi ya Kisiasa" kwa sababu yeye si mwanasiasa bali ni mshauri na badala yake ni vyema akafanya shughuli zake kama mshauri, ili kuleta ufanisi katika shughuli za kiushauri. Kwa maana hiyo, washauri maalum waajiriwe kwa mkataba maalum kama ni washauri (*Advisors*) na watafanyakazi zao za kumshauri Rais na waajiriwe kwa masharti ya Utumishi wa Umma, kwani sio kila mshauri kuwa ni mwanasiasa. *(Makofi)*

Sehemu ya Tatu ya Mswada.

b) Sehemu ya Tatu, kifungu 10(2) kifungu 12(2) na kifungu 14(2) maneno "asilimia maalum" kama tulivyosema mwanzo maneno yote yafutwe na katika vifungu hivi yasomeke "asilimia 50". Mhe Spika, kamati yangu inashauri sheria itamke wazi wazi haki watakayo stahiki kuipata wajane wa marehemu kuliko kumwachia Rais kuwafikiria kwani hii itampa mzigo usiokuwa na maana yeyote, kwani Rais anayo majukumu mengi ya kufanya na pia malalamiko kwa familia ya marehemu kwani sheria tu peke yake ndio itakayofuata mkondo wake. *(Makofi)*

c) Pia kifungu 10(3), 12(3) vifutwe kwani bado kwa mila zetu watoto wote wanakuwa ni wategemezi kwa wazazi wao. Kwa maana hiyo, kamati yangu imeona ni vyema watoto hao wategemee mafao mengine kutoka kwa wazazi wao ikiwemo urithi pamoja na pencheni. *(Makofi)*

d) Mapendekezo mapya yaliyoletwa na Mhe. Waziri, yaani kifungu 16 kinachozungumzia "Huduma za Wategemezi" hayatokuwa na msingi,

kwani kamati yangu imeshapendekeza yafutwe katika kifungu hiki. *(Makofi)*

Sehemu ya Nne ya Mswada

e) Mhe Spika, katika kifungu 16(1) maneno “Mshauri Maalum wa Rais” yafutwe kama kamati yangu ilivyoshauri kwenye sehemu ya kwanza na marekebisho ya kamati katika mswada huu.

f) Kifungu 16(2) na (4) neno “asilimia maalum” lisomeke “asilimia mia moja” kwa vifungu hivi ambavyo nimevizungumza, yaani kifungu hiki kama Sheria ambayo tunataka kuifuta ya inavyosema katika kifungu cha 4(2).

Sehemu ya Tano ya Mswada, Mhe Spika, kamati yangu inapendekeza kifungu cha 19 cha mswaada huu kifutwe, kwani hakina mantiki yeyote katika sheria hii, ukilifuta neno “asilimia maalum” kifungu hichi tayari kimefutika wenyewe.

Mhe Spika, kifungu cha 20 kamati yangu haina pingamizi na kifungu cha 20 cha mswada huu kuhusu waziri kutunga kanuni, lakini tunashauri yaongezwe maneno “na kanuni hizo zipate baraka ya Kamati husika ya Baraza la Wawakilishi.”

Mhe Spika, kifungu cha 22 kamati yangu bado haikubaliani na kifungu cha 22(1) cha mswaada huu kwa kuwa kinahusu suala la maslahi. Kwa hiyo, kamati yangu inashauri ni vyema yakaongezwa maneno “na marekebisho hayo yakaridhiwa na Baraza la Wawakilishi”, yanayozungumza katika majaduweli ya sheria hii”.

Na maneno “kwa kutoa toleo litakalochapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali” pia yafutwe.

Mhe Spika, kamati yangu inashauri kifungu cha 24 kifutwe kwani kinakiuka mamlaka ya kazi za Baraza la Wawakilishi, kama kifungu 88(a) cha Katiba ya Zanzibar, kinachosema:-

“Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya katiba hii, litafanya kazi kwa mambo yafuatayo ya utekelezaji:

a) “Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo”.

Majadweli

g) Katika Jaduweli la Kwanza kamati yangu inapendekeza kuzifuta aya (i), (j) na (k) "kwa sababu zifuatazo;-

a) Mhe Spika, aya (i) ya mswaada unapendekeza kuanzisha "Ofisi kwa Marais Wastaafu". Kamati yangu haikubaliani kuanzisha Ofisi kwa Marais Wastaafu kwa sababu ni kuongeza matumizi ya fedha za umma bila ya sababu za msingi, kwani maana ya kumwita mstaafu ni kuwa apumzike na kama atahitaji kufanya shughuli zake nyingine, basi awe huru kuzifanya yeye mwenyewe binafsi kwa gharama zake mwenyewe. Hivi sasa Zanzibar tayari tunao Marais Wastaafu Wanne na wala kamati yangu haijaona umuhimu wa kuwa na ofisi hizo.

Mhe Spika, aya ya (j) kwa kuwa aya ya (n) inaelezea usalama wa lazima na huduma nyingine za kinga kifungu hiki kitakuwa kinajitosheleza, kwa hiyo kifungu (n) kifute kifungu (j). Hivyo kamati inapenedekeza kifungu kidogo cha (j) kiondoke.

(c) Mhe. Spika, kamati yangu inashauri kifungu (k) katika kaduweli la kwanza kifutwe kwani kifungu (i) kikifutwa tayari katibu Mukhtasi atakuwa hana kazi. Kwa kufuta vifungu hivyo tutakuwa tumepunguza matumizi makubwa ya fedha za umma.

(h) Katika Jadweli la Pili katika aya (q) neno **"Kizuka"** lisomeke **"Mjane wa Makamo wa Rais Mstaafu"**

i) Katika Jadweli la nne Kamati imejaalia " X" ni asilimia mia moja. Kwa hiyo neno 'X" liondoke lisomeke **"100%"**

Mhe. Spika, mbali na marekebisho hayo, kamati pia ilifanya marekebisho ya mswada wa **WA SHERIA YA MASLAHI YA MAFAO YA VIONGOZI WA KISIASA BAADA YA KUSTAAFU** na marekebisho hayo yamegawika kama ifuatavyo:-

1. Marekebisho ya Mswada kwa kuongeza maneno ili mswada usomeke vizuri kama nilivyokwishaainisha katika maelezo yangu pamoja na mapendekezo ya marekebisho ya Kamati.

2. Marekebisho ya irabu katika baadhi ya maneno ili maneno hayo yaende sawa na mpangilio wa maneno mengine kwa mfano neno "**yeyote**" katika kifungu cha nne, ukurasa wa 295 limebadilishwa na kusomeka " **yoyote"**

3. Marekebisho ya Mswada kwa kuongeza vifungu kwa lengo la kuimarisha mswada huu, mfano katika kifungu cha 4 kimeongezwa kifungu kidogo cha (g) kinachosomeka **"iwapo atateuliwa katika nafasi nyengine ya utendaji na kulazimika kuacha nafasi ya kisiasa kwa mujibu wa sheria."**

4. Marekebisho ya mswada kwa kuviweka vifungu au tafsiri ya maneno ili ilete maana iliyokusudiwa kwa mujibu wa sheria inayotaka kutungwa kwa mfano katika tafsiri ya maneno " **Mrithi**" na " **Mjane**" yalionekana kutoleta maana iliyokusudiwa na badala yake kuandikwa vile ilivyokusudiwa kama inavyoonekana katika nakala ya marekebisho ya mswada.

Mhe Spika, kazi kubwa iliyofanywa na kamati yako hii na marekebisho yote tulioyafanya yametokana na maoni ya wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi wakati wa semina, pia maoni ya wadau mbali mbali wakiwemo wanasiasa wasiokuwa na uwakilishi ndani ya Baraza letu la Uwakilishi, wanasheria, wananchi wa kawaida majimboni mwetu na maoni kupitia vyombo vya habari, redio, magazeti, *Internet* pamoja na busara za kamati yako kwa Serikali. Kwa hiyo naamini waheshimiwa wajumbe wako wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi watayaunga mkono marekebisho ya kamati hii ili kuuboresha mswaada huu. Naamini Waziri atayakubali ili mswaada huu upite bila ya pingamizi yoyote ili baadaye uwe sheria.

Lakini pia Kamati yangu bado imesikitishwa na mswada huu kwa kuletwa ukiwa na tarehe ya mwezi wa Septemba ambao unaonesha wazi kuwa hakuna umakini katika utaarishwaji wa Mswada.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nikushukuru kwa mara nyengine tena na kwa niaba ya Kamati nitaunga mkono hoja pale ambapo maoni ya kamati yatakapokubalika katika mswaada huu.
Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba kuwashukuru sana. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nikushukuru wewe na hasa leo asubuhi ulivyotuambia kutokana na hali yako ya afya uko fit na mimi naamini hivyo Mheshimiwa na Ishallah Mwenyezi Mungu akubariki na akuendelezee hivyo hivyo avya yao iliyokuwa nzuri sana.

Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati aliyeondoka sasa hivi kwa maelezo yake mazuri sana. Namuunga mkono asilimia mia kwa mia. Baraza lako hili Mheshimiwa mimi nasema *International*.

Naomba Mhe. Spika, uyathamini maelekezo ya Mwenyekiti wetu ili lisiweze kudharaulika Baraza lako. Ni jambo la kushangaza sana kwamba mtu uwe unakwenda ukirudi, unakwenda ukirudi, tunakuwa kama watoto wadogo tunaochezeshwa foliti. Sote hapa ni watu wenye akili.

Mhe. Spika, niseme wakati viongozi wetu wanapotembea nchi za nje, mimi nilifikiria kuwa kwenda nchi za nje kwenda kutafuta mafunzo kwenye Mabunge au katika kuangalia mambo ya miradi na kutuletea katika nchi yetu. Sijui Mheshimiwa wangu Waziri Mswada huu kutuletea hapa sijui niseme kaiga nchi gani. Nchi ambayo iliyokuwa na mfano ambao sasa hivi sisi tunataka kuelekea kuuiga. Hichi kitu Mheshimiwa sikuweza kuona kabisa ni Bunge gani au ni nchi gani ambayo uliyokuwa unapanga jambo ambalo unaonesha mafao yao wao juu juu tu, kwenye wa chini huku kusiwe na mafao haya. Ambacho hiki Mheshimiwa kichwa kinaniuma sana.

Mhe. Spika, utashangaa sana kwa nini leo naeleza hivi. Kwa sababu huko nje sisi ni watu ambao tunawawakilisha wananchi. Hivi karibuni hapa Wizara husika ilipandisha mishahara na ikasema kuwa inapandisha mshahara 25%. Wale watu wengi sana walipiga kofi na wengine wakawa hawakuelewa, lakini wengine walielewa hasa. Lakini sasa hivi baada ya kuwa tayari ile 25% inataka kuanza kufanya kazi.

Mhe. Spika, 25% haijakamilika wala haijaanza kufanya kazi. Leo tunaanza kuleta mafao ya ngazi za juu, tutaeleweka vipi. Tutaeleweka vipi kwa wananchi wetu. Kuna vilio sasa hivi vya wafanyakazi hawana mishahara, sijui kusema tutakuwa waongo kusema kuwa tuyakubali haya hawa wastaafu waongezwe mishahara ya juu pamoja na hawa watu wa siasa. Mimi ni kitu ambacho kinanishangaza tutazipata wapi fedha Mhe. Spika. Wakati leo watu wa chini fedha tunashindwa kuwaongezea kwenye mishahara yao. Tutakuwa tunasema uongo na mimi kitu cha uongo nasema sasa mwiko kabisa.

Mhe. Spika, nimebadilika sasa hivi Mheshimiwa wako Mwakilishi, nataka niwe mkweli na muwazi. Mswada huu hasa haya marekebisho, mimi mtu mmoja naongoza watu 10,000. Mhe. Waziri kaniletea sasa hivi, ghafla hii kuwa marekebisho haya ameyasoma hapo. Hetu niambie muheshimiwa nitakaa saa ngapi ili kuyafikiria ili kuweza kutoa hoja nzuri. Sasa nyengine Mheshimiwa tusidharaulike kiasi hicho. Mimi mwenyekiti wangu alisema pale vizuri sana na uzoefu wake umeonekana. Kuna mambo mengine amejibu hivi hivi kutokana na uwezo wake na uzoefu wake wa kuwa yupo katika Baraza hili kwa muda mwingi sana.

Mheshimiwa mimi haya siyakubali haya marekebisho tuliyoletewa, siyakubali kabisa. Kwa sababu nasema kuwa serikali yangu ni change. Mimi najiuliza fedha hizi tutazipata wapi. Sasa hivi tunasheria kuwa kila baada ya miaka 10 tunaweka Rais mwengine.
Kama unavyotujua Mhe. Spika, Maraisi wetu wengine wanao wake wawili, wengine zaidi. Sasa tutakuwa na fedha za kiasi gani ili kuweza kuwalisha kama ije kutokezea hao wajane, wenye watoto na kuzaa tunazaa sana sio mchezo.

Mhe. Spika, kutokana na hali hii mwenyekiti wangu amesema kuwa ripoti yake hii kama ilivyoeleza humu kuwa kuna maeneo amayaainisha. Katika huu Mswada mpya ulioletwa Mswada mpya ambao Mhe. Waziri amesema kwamba tuusahau ule wa zamani. Mimi nasema ni ule ule haujabadilika kitu, mwaka jana nilivaa suti, mara hii nimevaa bunge, ndio yale yale. Lile bunge lakini lina shoo ya suti, lakini na kuna suti ambayo unayoivaa inaitwa vile vile suti lakini ile inaitwa bunge kwa sababu ina shingo ya raund.

Mimi nafikiria waheshimiwa wetu mawaziri hebu tuwafikirieni na watu wa chini. Mheshimiwa mishahara ingali midogo. Leo tunataka tujipandishe sisi mishahara mingi ambayo kwa kuwa ni waheshimiwa. Hebu tuwafikirieni hawa, askari wetu wa vikosi vya SMZ pesa mishahara midogo na tu nawakata pesa za chakula, Idara ya Afya mpaka sasa hivi maspeshalisti, maodali, mpaka leo pesa zao bado hawajapata. Halafu leo Mhe. Mshimba aunge mkono asilimia hii. Sikubaliani nao Mhe. Spika, na hasa wananchi wa jimbo la Kitope wamenikataza katu nisikubaliane na suala hili.

Mheshimiwa utanishangaa sana kwa kuwa sijenda vifungu hadi vifungu kwa sababu nazungumza kwa mambo ya jumla jumla. Sitaki niende kwenye vifungu kwa sababu mimi Mswada huu nimeshaukataa wote. Ndio maana nikasema kwamba siendi lakini nitakwenda kwenye pointi ambazo zinalingana na masuala ya fedha Mhe. Spika, naomba unistahamilie.

Mhe. Spika, sasa hivi kuna zogo kubwa na hasa wafanyakazi wetu wa afya. Hili ongezeko la 25% mpaka leo pesa zao hawajapata, leo wanatusikia tumekaa hapa tunazipitisha fedha hizi za wakubwa wetu, watatuhisi vipi. Mhe. Mwenyezi Mungu atutaalie sasa hivi Zanzibar hatujui kununa, hatujui kugoma. Wenzetu nenda Muhimbili hapo kila leo ukisikia wanagoma watu, kwa kuwa nini pengine kuna nyongeza haijafanyika sawa. Lakini sisi Mwenyezi Mungu yupo anatulinda, lakini watu watasema nalitote. Je, wakiandamana wataulizwa nani sasa.

Jamani kuna mambo ambayo unaweza ukatengeneza kitu na watu wakakupenda, lakini tusitengeneze kitu watu wakachukia. Mheshimiwa

kuongeza mafao makubwa kwa wakubwa ni tatizo kubwa sana na ni sugu, huyu wa chini je, tunamfanya nini?
Mhe. Spika, nikasema kwamba ni lazima kwanza tuanzie chini. Mheshimiwa Mswada urudi tena huko huko ulikotoka au usije kabisa ni bora usije kabisa. Kuja kwake uje ukiwa huku chini kumesharekebishwa, wananchi wetu wanapata fedha zao zile za ongezeko ambazo kuwa huku nyuma hawajapewa ambazo tumesema 25% mpaka leo hawajalipwa pesa zao. Hilo tungeliomba waheshimiwa.

Mwisho niseme dunia nzima hii ina maana kuwa sasa hivi Zanzibar ndiyo katika dunia nzima inayopata mshahara mdogo wafanyakazi wake, ukizunguka kote. Kila leo waheshimiwa wetu unasikia leo Waziri gani kenda pale, waziri gani kenda wapi, kumbe nimegundua tunakwenda kuuza uzuri, hatuendi kutafuta maendeleo tukawaletea wananchi wetu, hatuendi kwenda kutafuta viwango vile vya wafanyakazi wenzetu wanalipwaje mishahara yao. Tunakwenda tukirudi na brifkesi zetu na makoti tunabakia tukae kitako tupige kofi, sasa hatupigi koti.

Mheshimiwa kwa kumalizia nasema kwa kuwa mimi nataka nijisafishe na wananchi wangu wananisikia na Wazanzibari wanasikia kama natetea haki yao kuwa ni lazima mishahara yao ipandishwe halafu ndio tupandishe mafao ya watu wakubwa.
Kwa hayo machache Mheshimiwa sitokuwa na mengi kwa sababu nasema tayari Mswada huu nimeshaukataa. Naunga mkono hotuba ya Mwenyekiti wangu asilimia mia kwa mia na wananchi wa jimbo la Kitope pamoja na Wazanzibari. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi ya tatu baada ya hotuba ya Mhe. Waziri. Kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu. Pili nawaombea kheri ya mwaka mpya wajumbe na wananchi wote wa Zanzibar na Watanzania kwa jumla, ili tuweze kushirikiana kuijenga nchi yetu.

Mhe. Spika, si vibaya kumtunza mtu aliyekuwa keshafanya kazi. Lakini pia ni dhambi kumpa mtu iliyokuwa si njia ya sadaka kitu cha ziada ambacho yeye hawezi akakitumia. Kwa hivyo Mswada huu kwa fikira yangu haukuja wakati mnasaba. Huu Mswada unazungumza malipo ya wastaafu, viongozi wakubwa wa kisiasa. Lakini sasa hivi tupo karibu mwaka mmoja tu toka tuanza awamu hii, si dhani kama tumepata tathmini ya kuona kwamba viongozi wetu wanatufanyia vizuri ili tuweze kuwatunza. Tatizo kubwa linakuja hapa kwamba hakuja na tathmini kamilifu ya kuona kwamba hayo waliyotuomba sisi tuwaidhinishie tunaweza kutathmini utandaji wao wa kazi na pale

walivyotufikisha katika ukuwaji wa uchumi ili tuweze na sisi kuwatunza hilo la mwanzo.

Pili Mhe. Spika, nije katika Mswada wenyewe. Nikianza na sehemu ya kwanza ya ufafanuzi kifungu cha tatu. Kama alivyotangulia kusema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Utafatiliaji wa Viongozi Wakuu, mimi naomba niseme kwamba tafsiri wa kiongozi wa kisiasa naweza nikakubaliana na maneno yote isipokuwa neno la mwisho tu, Mshauri Maalum wa Rais. Mimi sikubaliana na Mshauri Maalum wa Rais kwamba ni kiongozi wa kisiasa. Hoja yangu ni Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar katika sehemu ya kwanza inayozungumza kuhusu mgawanyo wa madaraka kifungu (5) (a) nanukuu Mhe. Spika.

"Kifungu cha (1) kinasema:

Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu.

(1) Mamlaka ya Utendaji.

(2) Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma.

(3) Mamlaka ya Utekelezaji wa Utoaji Haki.

Kifungu cha (2) kinasema:

1) Mamlaya ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

2) Mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi.

3) Mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ni Mahakama. "

Kwa hivyo kama kutakuwa na viongozi Mhe. Spika, basi watatokana na vyombo hivi vitatu. Sidhani kama kutakuwa na kiongozi aliyekuwa hakutokana na vyombo hivi ataingia katika mamlaka ya dola.

Mhe. Spika, katika Sehemu ya Nne ya Katiba ya Zanzibar kifungu cha 58, sehemu hii ya (4) inazungumza madaraka ya Serikali. Kifungu 58 kinazungumza *marginal note* washauri maalum na kote hapo 58(1) nanukuu.

"Raisi anaweza kumteuwa mtu yoyote kama ni mshauri wake maalum ili kumsaidia katika utendaji wa kazi zake. Hakuna ushauri hapa wala siasa, hii ndio katiba ya Zanzibar."

Kwa hivyo pale kweli *marginal note* imeandikwa washauri maalum. Lakini kazi yao imekuwa *very specific* kumsaidia Raisi katika utendaji wa kazi zake, hawawezi hawa kuitwa wana siasa kabisa. Hawa wanafanya kazi ya kumsaidia Rais katika kazi zake, akiwa yeye chimbuko lake alitoka Baraza la Wawakilishi au alitoka wapi hiyo haihusiani. Kitu kinachozungumza katiba ni kazi yake ni kumsaidia rais kufanya kazi zake.

Mheshimiwa mimi binafsi na nawaomba wenzangu wote wakatae kabisa kifungu hichi cha kuwafanya washauri maalum wa Raisi kwamba ni viongozi wa kisiasa. Lakini hata katika utaalamu wa neno kiongozi, wenzetu walioandika *learder***,** kiongozi ni lazima ashiriki katika maamuzi. Sasa ukimwita mtu kiongozi wa kisiasa anashiriki vipi moja kwa moja katika maamuzi ya kisiasa.

Ndio maana Zanzibar Baraza la Wawakilishi viongozi wake wote wakawa ndio wanasiasa kwa sababu wanashiriki moja kwa moja katika maamuzi ya kisiasa. Kwa hivyo wale hawawezi washauri maalum wa Rais wakawa ni viongozi kwa sababu hawashiriki moja kwa moja katika uwamuzi wa maamuzi ya kisiasa. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri aje awatoe hawa, si hivyo hoja yake sisi hatuiyungi mkono.

Mhe. Spika, sasa nakwenda katika kifungu cha jadweli katika mafao ya viongozi wakuu wastaafu kuanzia Mhe. Rais Mstaafu. Jadweli hii ya kwanza katika Mswada huu inataja mambo mengi orodha kubwa ya posho watakalopewa. Tukianza na kifungu (a) kinasema kiunua mgongo sawa na asilimia 50% ya mshahara wa juu aliyopokea wakati wa kuwa Rais.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha. 35(1) napenda nikinukuu kinasema kwamba:-

> "Rais atapokea mshahara na posho na atakapostaafu atapata malipo ya uzeeni yaani kiunua mgongo na posho kama ilivyoamuliwa na Baraza la Wawakilishi."

Kweli walichukua madaraka lakini wangelitwambia hayo madaraka waliyochukua kumpangia mshahara ni ngapi pesa anazopata sasa hivi. Mimi tokea nije hapa mwaka 2005, hatujawahi kuletewa kifungu cha kupanga mshahara wa Mhe. Rais. Lakini baada ya huko kuchukua madaraka ya kumpangia Raisi mshahara, basi angalau sasa hivi wangetueleza kwa sababu sasa hivi tunataka kuamua tumlipe asilimia 50% ya mshahara tuliokuwa hatuujui ndio itakuwa vipi? Hii ni sawa sawa na kumuandikia mtu *open cheque* aende akajaze mwenyewe.

Kwa sababu haya ni mamlaka ya Baraza la Wawakilishi kumuandalia mshahara wa Raisi, sisi hatukupewa madaraka hayo lakini hata kutujuilisha kwamba huo

mfuko wa hazina unampa ngapi sasa hivi, hatuambiwi. Sasa hapa tupitishe nini?

Mhe. Spika, mimi ninao ushahidi wa mtandao kwamba waheshimiwa wengi huko nyuma walikuwa wakiisifu sana Singapore kwamba ni nchi nzuri ya kuiga, iliyoendelea. Mheshimiwa hii hapa karatasi. Nilioitoa kwenye mtandao. *Heading* yake imeandikwa (*The Greed of Singapore Rulers)* "Uroho wa viongozi wa Singapore" au ulafi.

Jadweli hii kwanza imeigwa kutoka Kenya. Katika hii karatasi Kenya ndio iliyooneshwa kwamba ni nchi inayowalipa viongozi wake wa kisiasa mishahara mikubwa yao `na wastaafu wake, katika ulimwengu mzima ni nchi ya kwanza karatasi inaonesha.

Sasa ukisema asilimia 80% Mhe. Spika, kwa kweli ni mshahara mzima. Asilimia 80% ya mshahara au posho lililokuwepo, kwa kweli hatufahamu tutawabakishia ngapi wananchi. Ikiwa kila mstaafu atapewa asilimia 80% ambao ni karibu wa ule ule mshahara anaopokea Rais au posho lile lile analopokea Rais, pencheni anayopokea Raisi, kwa hivyo hatutofahamu.
Mheshimiwa jaduweli hii inasema kwamba Singapore, iliingia katika madeni makubwa na kufilisika katika kipindi fulani kwa sababu ya kutoa pencheni kubwa sana kwa viongozi wao wa kisiasa, nanukuu, *"Former Minister George Yeoh lost his seatingParliament, he is out. He now gets Singapore U$ dollar 2 millions",* inaandikwa *U$ dollars two millions equivalent to U$ dollar one million, six hundred and thirty six thousand, three hundred and six plus every year for sitting at home and doing nothing.*

Mhe. Spika, sisemi mimi inatoka kwenye mtandao hii kwa sababu sisi tumo kwenye ulimwengu tufuate na wenzetu. Mhe. Spika, ni kwamba sikuitaja, mimi nina heshimu Baraza, kwa hivyo tuangalie lipi la kuwapa wastaafu wetu.

Mhe. Spika, sisi tulipokuwa wadogo tukielezwa vile visa vya zamani, halafu mwisho ulikuwa unaambiwa "wakakaa raha mustarehe" visa vya kale vilikuwa vinamalizia kama hivyo. Kwa hivyo, tuwaulize hao wastaafu wetu tunataka kuwapa stara wastirike wao na familia zao au tunataka kuwapa raha mustarehe hali ya kuwa wananchi wengi wanateseka?

Mhe. Spika, mimi kwanza asilimia 80 jambo hili siliungi mkono kabisa, lakini jambo la ajabu zaidi hebu isikilize hii sentensi kwa kituo kabisa. Kifungu cha (d) kinasema posho la matunzo la kila mwezi ambalo litakuwa sawa na asilimia 80 ya posho la matunzo analolipwa Rais aliyekuwepo madarakani.

Mimi nimetizama ile ofisi ya faragha nimeona 1.6 bilioni mara hii. Kwa hivyo, 1.6 bilioni kama ingelikuwa yupo Rais mstaafu analipwa sasa hivi na yeye angelipwa 1.2 bilioni za raha mustarehe tu hizo. Mhe. Spika, ndivyo ilivyoandikwa hapa za Rais aliyekuwepo madarakani kwa sababu maendesho ya Rais aliyekuwepo madarakani ndio 1.6, sasa huyu angelipwa 1.2 ndio asilimia 80 mbali na hizo nyengine hiki ni kifungu cha (d) tu. Mhe. Spika, ni kwamba hatukufanya mahesabu…

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, hapa tulipo tunajadili mswada wananchi wanatusikiliza nataka nitumie kifungu cha 58(3) cha Kanuni zetu.

Mhe. Spika, ni kwamba tunapochangia tunatakiwa tuchangie maelezo ya kweli tusipotoshe umma, kifungu cha faragha tofauti na maslahi au huduma ambazo tunataka kumuwekea Rais Mstaafu.

Mhe. Spika, sisi ni serikali ni kwamba tuna akili, tunaelewa uzito wa thamani ya 1.6 bilioni hatuwezi tukasema asilimia 80 ndio apewe Rais Mstaafu yaani 1.2 bilioni, sicho tunachokizungumza. Naomba sana Mhe. Spika, tumechaguliwa na wananchi tuchangieni yale ambayo ni ya kweli tusiupotoshe umma.

Mhe. Spika: Tuchukue tanbihi hiyo na tuone kwamba tunazungumza kitu ambacho tuna uhakika nacho.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwanza nakuhakikishia kwamba mimi sina utashi wa mazungumzo, nimepitia kitabu hiki hapa ambacho Mheshimiwa mwenyewe amekitoa. Kwa hivyo, ufafanuzi ikiwa haumo ni tatizo jengine sio ukiukaji wa kanuni kwa sababu mimi sifanyi kazi Ikulu na wala siyajui yanayopita kule. Lakini kitabu hiki ulichotuletea wewe ndivyo nilivyochukua na mwisho akasema maelezo ya matumizi yametajwa mpaka vyakula vya wageni vimetajwa humu humu.

Mhe. Spika, ndio nikasema kwamba hizi sentensi zilizotumika hazifafanui vizuri, Mhe. Spika, watatushutumu bure mimi siwezi nikaja hapa nikadanganya umma hata siku moja, mimi katika miaka mitano iliyopita hata siku moja sijatoa sentensi yakudanganya umma na huu ni mwaka wa sita naendelea nao. Lakini hili jadweli lilivyopangwa imepangwa kiasi cha kwamba wengine wasifahamu, kwa nini hazikuwekwa *figures* kama pesa zetu hazuziamini basi tuweke kwenye U$ dollars ni kiasi fulani basi sisi tutafahamu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia mimi naunga mkono tena hoja iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi kwamba kifungu (i), (j) na (k) juu ya mambo ya kupeana ofisi *special*. Mhe. Spika, ni kwamba ofisi ziko za aina mbili, kuna *private office* na kuna *public office*. *Public office* ndio kuna jengo lazima lijuulikane liandikwe bango, ndio ofisi za kiserikali, ofisi za umma, ofisi za kikampuni lakini *private office* basi atiliwe AC mle katika nyumba yake, awekewe vitabu katika nyumba yake, atiliwe *internet* kwenye nyumba yake au ajengewe ofisi nyengine mpya iliyokuwa ina mambo tele, hiyo itakuwa hatuwafanyii haki wananchi wetu. Mhe. Spika, kwa kweli itakuwa hatuwafanyii haki wananchi kutumia pesa zao zote hizi kwa kutengeneza mambo kama haya.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ni kwamba wenzetu katika jadweli yao kama hii ya Kenya huko walikokuwa wanapeana sana kuna mambo mawili wameyasema humu hayamo, kwamba hii bajeti inapangwa miezi mitatu kabla ya ule muhuri wa kufikia na inatajwa wazi wazi, lakini nayo inafanyiwa *auditing* matumizi yake isijekuwa asisitiza pesa yeye akenda akaweka katika mabenki tu. Kama inaonekana kwamba ana akaunti kubwa sana mwaka wa pili inapunguzwa. Kwa hivyo, ni lazima zifanyiwe *auditing* pesa zake kweli zinatumika au anaweka katika mabenki anafanyia makampuni.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo yangu hayo ambayo nakuhakikishia tena kwamba mimi sizungumzi kwa utashi wa kusema nipoteshe Baraza au niwapotoshe wananchi, hiyo mimi sio fani yangu. Mimi nazungumza ukweli na ukweli na ukweli wa nafsi yangu nilionao, naomba sana Mhe. Waziri apunguze kwa kiwango kikubwa mafao haya ili na wananchi wengine wafaidi isijekuwa ikafikia wakati tukawalipa wastaafu wale wastaafu wa kawaida na wananchi wengine wakenda na sahani saa saba kwa viongozi wetu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mola wetu mtukufu kwa kutujaalia uhai na uzima mchana huu tukawa tunajadili mswada huu ulioletwa mbele yetu wa Sheria ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 2012. Pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii niendelee kuwashukuru wapiga kura wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe kwa kuendelea kuniamini na kunipa heshima ya kuwakilisha katika chombo hiki adhimu kinachosimamia maslahi yao.

Mhe. Spika, kwanza nimwambie Mhe. Omar Ali Shehe ajiandae kwa jioni tukijaalia maana nadhani muda nitauramba wote huu. Mhe. Spika, nitangulize kusema na mimi kama walivyosema wenzangu kwamba endapo mswada huu hautafanyiwa marekebisho makubwa yaliyopendekezwa na kamati na wajumbe wengine, basi hoja hii mimi naikataa na ninawashauri wenzangu waikatae.

Mhe. Spika, mtu akisema la maana sio vibaya kumnukuu, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani aliyekaa punde hivi amesema sio vibaya kuwatunza watu ambao wametumikia nchi na wamefanya kazi nzuri, naomba ieleweke kabisa kwamba tunapotoa maoni haya hatukusudii kuwadharau au kusema kwamba viongozi waliotumikia nchi hii wasitunzwe. Lakini Mhe. Spika, ni muhimu tutizame na hali ya nchi yetu na pia matarajio ya wananchi tunaowaongoza mara nyengine hupenda kusema humu wananchi wangu, mimi sina wananchi, wananchi ni wa Zanzibar, wananchi tunaowaongoza.

Mhe. Spika, kabla sijaingia katika vifungu tatizo la mswada huu linaleta joto lote hili ni kwa sababu umeifanya Zanzibar kama vile nchi iliyokuwa katika ulimwengu wa nchi zilizokuwa zimefikia hatua kubwa sana katika maendeleo ya uchumi. Lakini Mhe. Rashid Seif ametuonesha hapa kwamba hata hizo nchi kama Singapore zilizofikia maendeleo makubwa zinafika kuhojiwa juu ya viongozi wao, ulafi wao seuze nchi inayojikongoja kama ilivyo nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ningekuwa sina pingamizi kabisa na haya yaliyopendekeza achilia mbali asilimia 80 hata ingekuwa asilimia 100, lakini ingelikuwa mswada huu umeletwa mwaka 2014 tumeona miaka 4 ya serikali hii imeweka maendeleo makubwa ya kiuchumi na hali za wananchi za uchumi wao zimetononoka. Nadhani hapo wananchi hata wasingekuwa na kelele, lakini tunauleta mswada huu wakati wananchi wengi bado wanatuhoji matarajio waliokuwa wameyaweka katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa mbona bado hakuonekani dalili za kufikiwa.

Mhe. Spika, serikali hii tuliitetea kwa nguvu zote na tutaendelea kuiamini mimi mmoja nitaendelea kuitetea kwa nguvu zangu zote juu ya mfumo huu wa umoja wa kimataifa. Mhe. Spika, nikwambie hata katika mikutano yetu mengine ya huko nje tunaendelea kuutetea mfumo huu na tutaendelea kutaja mafanikio yaliyokwishafikiwa mpaka sasa hivi, huku tukiwataka wananchi wetu waendelee kuwa na stahamala. Kwa hivyo, ninachosema ikiwa matarajio yale hayajafikia malengo ya matarajio waliokuwa nayo wananchi bado kuleta suala hili ni mapema mno.

Mhe. Spika, tulivyoelezwa katika madhumuni ya mswada huu kumetajwa mambo kadhaa hapa, moja ni kwamba tulifanya marekebisho ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ambayo imeondosha nafasi ya Waziri Kiongozi na kuwa Makamo wawili wa Rais. Kwa hivyo, kuna haja ya kuzingatiwa hilo katika sheria zinazotumika hivi sasa. Lakini najua pia marekebisho yale yaliondosha nafasi za Wakuu wa Mikoa kama ni nafasi za kisiasa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningetegemea serikali ingetuletea mswada wa kurekebisha sheria zilizokuwepo na kama kuziweka mbili pamoja ni sawa ikaondosha nafasi ya Waziri Kiongozi ikataja Makamo wa Kwanza na Makamo wa Pili, ikaondoa Wakuu wa Mikoa katika nafasi za viongozi wa kisiasa na haya mengine yakasubiri hapo nchi yetu itakapotononoka tukazungumzia uchumi mkubwa.

Mhe. Spika, punde tu hapa tulikuwa tunazungumza katika kipindi cha maswali na majibu, kila linalozungumzwa hapa ikiwa *ICU*, ikiwa barabara, ikiwa kuezeka mabanda ya skuli yote tunazungumza serikali haijakuwa na uwezo wa kutosha. Kwa hivyo, wananchi hawatuelewi kwamba hatuna fedha za *ICU*, hatuna fedha za barabara, hatuna fedha za kuezekea mabanda ya skuli, hatuna fedha za madawa, hatuna fedha ya kuwapatia vitabu na madeski wanafunzi wetu, lakini fedha za kulipana asilimia 80 kwa mafao tunazo, hivyo wananchi itakuwa hawatuelewi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba hilo nisite hapo niende katika mswada.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa mswada huu waukufanyiwa marekebisho makubwa nitaukataa na nitawaomba wenzangu tuukatae na katika marekebisho hayo na mimi niongeze sauti yangu tu kwa sababu mengi yemeshatajwa na kamati na mjumbe aliyetangulia hapa. Mhe. Spika, kwanza nakubaliana na pendekezo la kamati kwamba neno asilimia maalum liondoshwe. Mhe. Spika, dunia ya leo inaendeshwa kwa uwazi, tunaposema asilimia maalum maana yake ni asilimia itakayoamuliwa na Rais, ndio maana yake tunatunga sheria hapa bubu. Hivyo tunatakiwa tupitishe lakini muamuzi sio sisi tunaopitisha sheria.
Mhe. Spika, tusidanganyane tunalikataa kwa sababu sote tunajua kwamba hata kama itasema itakayoamuliwa na Rais mwisho kuna watendaji wa Ofisi ya Rais ndio watakaoamua na halafu apelekewe Mhe. Rais aidhinishe. Kwa hivyo, nadhani chombo hasa cha kusimamia kodi za wananchi za matumizi ni chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, na mimi nakubaliana na pendekezo kwamba asilimia maalum iondoke pawe na asilimia zinazojuulikana.

Mhe. Spika, pia nikubaliane katika tafsiri na katika maeneo mengine yote nisirejee tena kila palipoingizwa katika tafsiri mshauri wa Rais waondolewe katika orodha ya viongozi wa kisiasa. Mhe. Spika, sina haja ya kutoa hoja za ziada Mhe. Rashid Seif amemaliza katiba yenyewe inasema hawa ni wasaidizi katika utendaji wa kazi za Rais na sio viongozi wa kisiasa.

Mhe. Spika, ingekuwa ni viongozi wa kisiasa ningeuliza mimi wanamuongoza nani, maana wengine wote tumeambiwa kwamba mawaziri wanaongoza wizara zinazowahudumiwa wananchi, wawakilishi wanaongoza majimbo, Rais anaongoza nchi, Makamo wa Rais anaongoza Serikali, hivyo hawa washauri wa Rais wanamuongoza nani hata waingie katika fungu la viongozi? Kwa hivyo, mimi nakubaliana kwamba hili neno liondoke katika tafsiri.

Mhe. Spika, naomba niende katika sehemu ya tatu kifungu cha 10 (3) na kifungu cha 12 (3) nikichangie kwa pamoja. Mhe. Spika, hivi kwa mujibu nilivyofahamu mimi ni kwamba vimefutwa, lakini badala yake kumeingizwa kifungu kipya hapa ambacho kinasema kwamba endapo Rais, Makamo wa Rais au Spika, wa Baraza la Wawakilishi atafariki wakati akiwepo madarakani mtoto au watoto wao watahudumiwa na mamlaka husika hadi watakapotimia umri wa miaka 20 au ikiwa mtoto wa kike pale atakapoolewa lolote litakalotokea mwanzo.

Mhe. Spika, bado hii haijaondosha hisia walizonazo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi tunaowaongoza. Kamati hapa imekuja na pendekezo zuri, Mhe. Spika, nchi yoyote duniani ina mila zake na desturi zake kwa wenzetu kama Waingereza zile mila na desturi zao ndio zinazoongoza nchi hata hawana katiba iliyoandikwa na miswada inayopitishwa na Bunge lao.

Kwa hivyo, hapa kwetu kama walivyosema kamati tuna mila zetu namna ya kulea watoto wakiachwa na mzazi aliyetangulia kwa vile mila zile zingepaswa zichukue mkondo wake, na kama kuhudumiwa hawa mara nyingi wanahudumiwa na warithi wa marehemu na warithi wameshasemwa katika sheria hii kwamba wao ikiwa Rais atafariki au kiongozi mwengine yeyote aliyetajwa katika mafungu haya basi zile haki zake zitachukuliwa na warithi wake. Kwa hivyo, ni akili ya kibinadamu kwamba haki zote zikichukuliwe na wale warithi zitumike pia kulelea wale watoto.

Mhe. Spika, sasa nataka niende katika sehemu ya tano, sehemu hii ndio ile inayofafanua asilimia maalum iliyopendekezwa iondoke kifungu cha 19 kinasema kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya sheria hii katika kuweka kiwango cha asilimia maalum Rais atazingatia kiwango cha fedha atakachopokea kiongozi wa kisiasa kwa ajili ya mafao hakitakuwa pungufu ya kiwango cha mafao alichopokea kiongozi wa kisiasa aliyepita kabla yake.

Maana yake nini Mhe. Spika, hiyo? Ni kwamba amewekea *minimum* huku chini kwamba akija akenda chini anachopata huyu aliyeondoka, lakini kwenda juu ameachiwa huria aweze kupanga chochote anachokitaka. Mhe. Spika, huu sio utaratibu wa msingi wa utawala bora na uendeshaji wa serikali kwa misingi ya uwazi ambayo tunakwenda kuimba kila siku hizi.

Mhe. Spika, kifungu cha 20 kimesema mamlaka ya waziri kutunga kanuni katika utaratibu wa kawaida tusingekuwa na hoja juu ya kifungu hicho kwa sababu ni kawaida waziri kupewa mamlaka ya kutunga kanuni zinazohusu sheria ambazo anazisimamia. Lakini kwa sheria hii na kauli hii iliyotuonesha serikali labda ilivyokuja nayo mimi nakubaliana kabisa na pendekezo la kamati kwamba waziri atunge kanuni lakini tukifuata utaratibu unaotumika na nchi nyingi za Jumuiya ya Madola kwamba kwa kanuni za baadhi ya sheria basi chombo cha kutunga sheria kupitia kamati husika angalau kinashirikishwa kudhiidhinisha kanuni zile. Kwa hivyo, ni pendekeze na nimwambie Mhe. Waziri kwamba akija hili alikubali la kama sio hivyo basi mswada huu atarudi nao kama alivyorudi nao ule uliopita.

Mhe. Spika, vifungu ambavyo vimenitisha zaidi ni kifungu cha 22 (1) hiki kinasema waziri anaweza muda hadi muda wa kushauriana na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi kurekebisha majadweli ya sheria hii kwa kutoa toleo litakalochapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali. Hii ni kurejesha sheria katika mfumo wa utungaji sheria ambao hatujapatapo kuonekana duniani. Mhe. Spika, roho, msingi wa sheria hii ni majadweli, huku mwanzo kunazungumzwa taratibu tu lakini mafao yao yaweje hasa yamo katika majadweli. Mhe. Spika, huko kwenye viwango hasa kama tungeipitisha basi waziri tu akishakaa huko anaweza kushauriana na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi wakarekebisha majadweli yale, halafu wakachapisha kwenye gazeti rasmi la serikali.

Kwa hivyo, sheria hii inafanywa kuwa *redundancy* haina maana kama kifungu hicho tutakipitisha. Mhe. Spika, huku ni waziri kujipa mamlaka makubwa mno na mimi nimeshangaa kwamba Baraza la Mapinduzi linategemewa kuwa muhimili wa maslahi ya watu wa nchi hii limewacha kifungu hiki wakatuletea katika Baraza la Wawakilishi kifungu hiki. Mhe. Spika, mimi nasema hiki kama hakijarekebishwa kama nilivyosema ikiwa kutakuwa na haja ya Baraza la Wawakilishi lipo liletewe lifanye marekebisho ya majadweli kama sio hivyo mswada huu tutaurejesha Mhe. Spika.

Mhe. Spika, vile vile katika kifungu cha 24 kinachohusu kukadiria mafao kwa mjane wa kiongozi wa kisiasa. Mhe. Spika, haraka hara niende katika majadweli yenyewe ni yale yaliyozungumzwa mwanzo na Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba tungekuwa tumeshajenga uchumi mzuri asilimia 80 tungesema sawa mimi nilisema hata asilimia 100, lakini uchumi wetu tunauona. Mhe. Spika, hapa nimetoa mifano baadhi ya mambo ya msingi yanayokwama yanayohusu huduma za watu, leo Mhe. Spika, asilimia 80 ni karibu mno na asilimia 100 katika hali ya uchumi wetu tunataka kuwalipa viongozi wastaafu sawa sawa na walioko madarakani.

Mhe. Spika, suala hili tulilitahadharisha Januari mwaka jana mwezi kama huu inaonekana mwezi wa Januari unakuwa na mambo makubwa katika mambo ya mafao. Mhe. Spika, mwezi Januari mwaka jana tulikuwa na sheria hapa ya utumishi wa umma ambayo ilikuwa inasema kwamba Katibu Mkuu Kiongozi akiondoka nafasi yake mshahara wake hautopungua hata akiondoka nafasi hii. Mhe. Spika, tulitahadharisha masuala haya na sasa ndio yanaendelea kuwa ndio mwelekeo.

Kwa hivyo, nasema kamati imekuja na pendekezo kwamba kuwe angalau asilimia 50 mimi ningeliliunga mkono pendekezo hilo kumlipa angalau nusu ya kinachofuata aliyekuwepo katika nafasi ile kwa sasa katika kumuhudumia ningeliikubali. Mhe. Spika, tena katika kifungu cha © na (d) katika majadweli haya sio pencheni ya kila mwezi tu lakini na posho la matunzo. Kwa hivyo, ingelikuwa anapewa pencheni ya mwanzi halafu angekuwa hapewi posho la matunzo ningesema kweli anazihitaji, lakini posho la matunzo anapewa halafu na pencheni ya kila mwezi ni asilimia 80. Hii Mhe. Spika, ni kubwa sana.

Mhe. Spika, kamati imependekeza kwamba viongozi wastaafu hawa hivi vifungu (i), (j) na (k) viondolewe. Mimi kidogo nina mawazo tofauti katika hili na kamati na ndio raha ya demokrasi kutofautiana. Mhe. Spika, kwa nchi za wenzetu viongozi wanapostaafu bado huendelea kutumika, ndani ya nchi na hata nje ya nchi za wenzetu hutoa uzoefu wao, wanaweka kumbukumbu za mambo wanayoyafanyia kazi ili iwe ni urithi kwa jamii katika siku za mbele. Kwa hivyo, mimi ningesema kuwa na ofisi mradi ifahamike tu katika madhumuni hii kwamba ofisi yenyewe hatwendi kutengeneza Ikulu ndogo nyengine au Ofisi ya Makamo wa Kwanza ndogo au Ofisi ya Makamo wa Pili ndogo. Lakini kama ni kuwa na ofisi ya kumuhudumia kwa mujibu wa uwezo wake wa kufanya shughuli zake mimi hili silioni pingamizi. Lakini Mhe. Spika, pengine vizazi vyetu vingefaidika sana na uzoefu wao wanaotumia ofisi hii. Mhe. Spika, kwenye jadweli la pili mawazo yangu kwenye vifungu © na (d) ni kama kifungu hiki kinachomuhusu Rais kwamba tupunguze hadi asilimia 50 kwa sababu huduma nyengine kama petroli, simu yote yamezingatiwa humu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika ile *formula* pale palipowekwa (x) kwa sababu tumekataa asilimia maalum ingekuwa ni vizuri ikatajwa ili sheria hii tuipitishe. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba niseme tena moja la jumla halafu nifunge maelezo yangu.

Mhe. Spika, waliotumikia nchi hii na ikasonga mbele sio viongozi wa kisiasa tu, lakini pia ni watumishi wa umma ambao wanafanya kazi kubwa sana hata sisi viongozi wa kisiasa tukapanda juu ya majukwaa tukawa tunajisifu. Katika watu wanaoishi maisha dhalili katika nchi hii ni wastaafu wetu katika utumishi wa umma.

Mhe. Spika, kuna watu humu mwisho wa mwenzi anatoka anakotoka anakwenda kupokea shilingi 20,000 au 25,000 anategemea aishi kwa mwezi mzima, wengine wametusomesha leo tumekuwa tunavaa makoti makubwa makubwa tunakuja hapa, wakitukuta njiani wanatwambia kwamba leo tumekusomesheni nyinyi mnatanua, sisi tuliokufikisheni hapo mnatusahau. Kwa hivyo, ningetegemea kama kulikuwa na *priority* ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayojali watu basi ingekwenda kwanza kutizama mafungu ya watumishi wastaafu.

Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kusema kwamba mambo mawili nataka kuzungumzia, moja msingi wa hoja zetu zote kuanzia kamati tunataka uwazi katika sheria hii. Na uwazi katika dunia ya leo Mhe. Spika, ndio msingi wa muongozi wa jamii za kileo, na katika hilo Mhe. Spika, hata katiba yetu katika kifungu cha 35 (1) hata mshahara wa Rais, posho, malipo ya uzeeni, kiinua mgongo yote haya hayapaswi kuwa siri yalipaswa yapitishwe na Baraza hili la Wawakilishi. Kwa hivyo, waliotunga katiba hiyo nimpongeze sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa sababu ndio walioweka misingi mizuri kwamba katika nchi yetu hata mshahara wa Rais ujuulikane. Leo imesemwa hapa mimi nimeingia katika Baraza la Wawakilishi 2010, lakini hatukumbuki kwamba kuliwahi kuletwa sheria hapa ya kukadiria mshahara wa Rais.

Mhe. Spika, si tatizo lakini tunachosema msingi wake katiba yetu iliweka wazi kutambua uwazi, kwa hivyo nasema uendelee msingi huo katika kutunga sheria zetu nyengine zote. Lakini nimetangulia kusema mwanzo kwamba hoja alizozitoa ni kwamba hatutoi kwa sababu ya kutaka kuikomoa serikali wala kutaka ionekane kwamba hatuwathimini viongozi waliotumikia nchi hii. Mimi nataka ifahamike kwamba katika hili ingelikuwa ni kujipendelea hata wawakilishi tumetajwa katika sheria hii, kwa hiyo tungesema tu kwamba madhali na sisi tumo basi tuiwache iende tu, lakini tunaikataa kwa misingi kwamba bado haiendani na hali halisi ya nchi yetu, haizingatii maslahi ya watu wetu na kwa msingi huo kama nilivyosema isipokuwa tu kwamba yale marekebisho makubwa niliyoyapendekeza basi tutaikataa sheria hii na hatutoiunga mkono hoja hii. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni muda uliobaki ni mchache sana kwa hiyo kwa sasa itoshe kwa hayo tuliyochangia kwa kipindi hiki na tuje kuendelea pale jioni. Nilitaka niseme jambo moja dogo ili isaidie katika kuongoza shughuli zetu za Baraza kwamba tunajadili kitu ambacho kwa kweli ni muhimu sana, na tujadili jambo ambalo linahusu maslahi ya viongozi kama ilivyotajwa kwenye mswada wenyewe, lakini hapo hapo maana yake tunagusa uchumi wa nchi yetu. Kwa hivyo, ningeomba wajumbe pamoja na serikali tunapozungumzia masuala yanayohusu maslahi kwa ujumla,

sizungumzi kwa kiongozi, sizungumzi kwa wajumbe hawa tuzingatie sana masuala ya uchumi wa nchi yetu na haja ya maendeleo ya nchi yetu kwani ni muhimu.

Mimi ninayeongoza kikao hiki na mimi nimetajwa humo, lakini nataka niseme wallahi mimi sina *interest* yoyote, mimi ni kiongozi mlionichagua nimeapa kwa kukamata kitabu cha Mwenyezi Mungu hapo kutumikia nchi hii masuala ya kulipwa au kutolipwa kwangu si muhimu. Inaweza ikastaajabisha kwa sababu sisi viongozi sote tuliomo humu ndani kwa mswada huu maana yake kwanza tuwe tuna-*declare interest* maana sote tunahusika na hii. Kwa hivyo, kwanza tuwe tuna-*declare interest* yetu kwamba jamani nazungumza hiki kitu kwa manufaa ya nchi si kwa manufaa binafsi ambayo hata kanuni yetu hii huwa haipendi. Kwa hivyo, maneno yangu haya nakusudia kwamba tuendeleze mjadala wa mswada huu kwa manufaa ya nchi yetu.

Baada ya maneno hayo machache sana sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru, kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na jioni hii tukaweza kukutana tena hapa. Vile vile tumshukuru kutufikisha salama katika mwaka huu wa 2012 sote tukiwa wazima na kuweza kukutana bila ya mapungufu yoyote kwa Wajumbe wako wa Baraza hili. Ni kitu cha kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia atujaalie mwaka huu uwe wenye neema, uwe wa salama, wenye utulivu mkubwa na awajaalie mawaziri wetu wafanye kazi kwa umakini zaidi awape nguvu zote ambazo wataweza kutekeleza vyema majukumu yao katika kuitumikia serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikushykuru na wewe kwa kunipatia nafasi jioni hii ili niweze na mimi angalau kuchangia mawili matatu. Kwa sababu zile ngoma za zumari zimeshapita sasa sisi wenye vinanda kwa kweli itakuwa ngoma yetu hainogi sasa.

Mhe. Naibu Spika, tutakumbuka kwamba mswada huu ulikuwa uletwe katika kikao kilichopita cha Baraza lako, lakini kutokana na mapungufu makubwa tuliyoyakuta tukaweza kuishauri serikali, tukamshauri Mhe. Waziri ili mswada huu usiletwe katika Baraza na tuipe nafasi serikali zaidi ili iweze kuifanyia

marekebisho mswada huu. Kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati mswada huu hata ukiuangalia sasa hivi ni wa tarehe 16 Septemba, wakati hii ni Januari, 2012 kwa hivyo, twabaan utakuwa ni ule ule ambao tuliomba ufanyiwe marekebisho na serikali ili baadae uletwe mswada ambao tutaweza kuujadili.

Sasa mimi binafsi nisikitike kwamba kile ambacho tumekiagiza kifanyiwe kazi na serikali kwa kweli kwa asilimia kubwa hakikufanyiwa kazi. Mhe. Waziri atakumbuka katika semina mimi binafsi nilimwambia Mhe. Waziri nakuomba zingatia sana hii, kwa sababu utakapokuja kutuletea mswada huu ulio na sura kama ilivyo kwa kweli wajumbe hatutoweza kuupitisha mswada huu, lakini niseme kwamba inaonekana mswada huu haukufanyiwa kazi kama vile ambavyo wajumbe tumeshauri.

Sasa hilo ni la kutusikitisha na hiyo sijui maana yake nini, kwa sababu sisi ndio wajumbe na sisi ndio tulioiambia serikali warekebishe lakini hilo halikutokea sasa maana yake kwa kweli sifahamu, lakini tutaelewa baadae.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya mswada huu kama ilivyoelezwa katika maandiko yake hapa kwamba, ni kuziunganisha sheria mbili ya kwana ni ile Sheria Nam. 4 ya mwaka 1988 na ya pili ni ile Sheria Nam. 6 ya mwaka 1999. kwa sababu inaonekana kwamba kulikuwa na sheria mbili sheria nambari 4 na sheria nambari 6 ya mwaka 1996.

Vizuri hasa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mwaka 1988 wengi wetu tulikuwa hatumo katika Baraza hili na hata mwaka 1999 wengi walikuwa hawamo katika Baraza hili na ndipo sheria hizo mbili ambazo zilikuwa zinahusika na mswada huu mpya ilikuwa kwa vyovyote vile mswada huu uje pamoja na sheria hizo ambazo zilikuwa zinahusika.

Mhe. Naibu Spika, dakika mbili zilizopita mimi binafsi ndio nimepokea sheria hii, dakika mbili tu. Sasa katika dakika mbili zilizopita hebu tuambieni maana yake ni nini? Maana yake dakika mbili hizi kweli nitaweza kuzipitia sheria hizi? Sasa huu ni utendaji mbovu na hatuwezi kama Baraza la Wawakilishi kwenda katika utaratibu huu, tutakuwa hatutekelezi wajibu wetu wala tutakuwa hatuwatendei haki wananchi wetu.

Baraza hili Mhe. Naibu Spika, pamoja na sisi wajumbe tunafanya kazi kubwa, ngumu na muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu. Maana yake isionekane ni mambo ya mchezo mchezo hii hali inaonekana kama ni mchezo mchezo tu, kuletewa marekebisho dakika mbili wakati mimi nazungumza niangalie nini sasa au naweza nikaona nini ndani yake humu.

Sasa bado naiomba serikali kwamba iache utaratibu huu, kama kuna kitu chochote kinachohusiana na mswada tunaoletewa mimi napendekeza na naomba sana kwamba ilivyo kanuni kwamba tupate ndani ya siku 21 ili tupate muda zaidi wa kupitia basin a yote yanayohusiana na mswada napendekeza nayo yafuate katika mfumo huu. Wajumbe wako kutupa dakika mbili na kujadili, wengine waliobahatika asubuhi maana yake hawakupata kabisa fursa kama hii.

Kwa hivyo, naomba sana serikali iachane na tabia hii ili angalau basi ionekane kwamba hatufanyi tu kazi za kuripua ripua hapa. Kwa msingi huo kwa kuwa kuna mambo mengi tulitaka yarekebishwe na hayakurekebishwa, na kwa kuwa kuna mambo mengi ndani ya mswada huu bado hayako wazi. Mhe. Naibu Spika, bado naendelea kusema tena kwamba mswada huu urejeshwe serikalini ili serikali ipate muda zaidi wa kuutayarisha mswada huu ili wajumbe tupate nafasi sasa ya kutengeneza kitu ambacho kitakuwa na maslahi kwa wananchi wetu na kwa uchumi wa nchi yetu na nchi yetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kati ya mambo ambayo hayako wazi kama wenzangu walivyoeleza ni suala zima la mshahara wa rais. Kwa sababu katika kifungu hiki cha 9 na katika jadweli nambari 1 ukiangalia a, b, c utaona kwamba (a) kimeelezea kiinua mgongo ambayo iwe ni asilimia 50 ya mshahara wa rais, kifungu (b) ni posho la kumalizia muda, kifungu (c) ni pencheni ya kila mwezi ya asilimia 80 ya Mhe. Rais. Sasa Mhe. Naibu Spika ili tufike pahala tujenge hoja vizuri kama wajumbe wako maana yake lazima tufahamu huo mshahara wa rais ukoje kama ilivyoelezwa katika katiba. Sisi hatuna tatizo kama walivyosema wajumbe wenzangu, hatuna tatizo na asilimia 80, vile vile hatuna tatizo hata ungelitwambia asilimia 100 ingelikuwa tungelikielewa hicho kiwango cha rais.

Mhe. Naibu Spika, mathalan ungelitwambia rais wetu anapata mshahara laki mbili kwa mwezi basi mimi ungelinambia tuongeze asilimia 80 ningelikwambai hii ndogo na hata asilimia 100 ningelikwambia ndogo labda asilimia 500 hiyo ingelikuwa ni sahihi. Lakini leo mathalan rais anapokea shilingi milioni saba ukinambia tuweke asilimia 80 ya shilingi imilioni saba hapo nitakwambia hii nyingi ungelinambia asilimia 50 naweza nikakubali. Hiyo ndio hoja tunayoizungumza, kitu cha msingi kwanza lazima tufahamu mshahara wenyewe ndio baadae tukubaliane na hiyo asilimia, hatuwezi tukafanya mambo ya kukubali pasina kuelewa huo mshahara wenyewe ni upi.

Kifungu (b) katika jadweli hiyo hiyo katika kifungu hicho hicho cha tisa kimeelezea maposho ya matunzo ya kila mwenzi kwa asilimia 80 ya matunzo anayoyapata rais aliyepo madarakani na hili haliko wazi na hili ndilo lililopelekea kuzusha ubishani baina ya Mhe. Rashid Seif na Mhe. Waziri wa

Fedha. Matunzo, matunzo ni nini? Maana yake ukisema matunzo maana yake ni kitu gani, nyumba tayari keshapewa, gari anayo, watumishi anao, *pocket money* hiyo anayopewa tayari anayo matunzo gani mengine? Pesa ya simu tayari, lakini matunzo nadhani tunaweza tukayapata katika ile tafsiri au katika yale maandishi yaliyoonekana katika kitabu cha bajeti, ukifungua kitabu cha bajeti utaona kwamba rais anakuwa na ofisi ya faranga, sasa ndani ya ofisi hiyo ndio kinaonekana kitu hicho matunzo mathalan Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu bajeti iliyopita.

Kifungu cha 35 ukurasa wa 19 kinasema:

> "Mhe. Spika, ofisi ya faragha ya rais pia inahusika na huduma nyenginezo muhimu za Rais wa Zanzibar zikiwemo huduma za makazi, chakula, usafiri pamoja na utunzaji na matengenezo ya majengo yaliyochini ya Ikulu".

Hii pengine ndipo tunapoweza kupata ile tafsiri ya matunzo. Sasa kama hivyo ndivyo kwamba hiki hiki anachotunziwa rais huyu ndio kwa asilimia yake 80 aje apewe mstaafu wake bado tunasema hii ni hatari tena hatari kubwa. Kwa sababu katika bajeti hiyo hiyo ya mwaka jana imeeleza kwamba Rais atatakiwa apewe shilingi milioni mia tano na ushei kwa mwaka, ikizigawa hizo kwa mwezi unaweza ukapata shilingi milioni 43, kila mwezi inakwenda fedha hizo shilingi milioni 43 katika suala zima la matunzo. Ina maana sasa asilimia 80 ya shilingi 43 milioni utapata kitu kama shilingi 37 milioni kitu kama hicho watu wa mahesabu wanaweza wakappiga hesabu.

Sasa tunakusudia kusema kwamba rais mstaafu apewe shilingi milioni 37 kila mwezi? Inawezekana ikawa hatujafahamu nafikiri hapa ni wakati wake sasa wa kufahamu na ndio tukasema kwa hivi sheria ilivyo kwa sababu sisi wajumbe hatujafahamu basi ilikuwa tupate muda wa kufahamishwa vyenginevyo hatuwezi kuipitisha na wala hatuwezi kufanyiwa hadaa katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, tafsiri yangu mimi iliyonipa ndio hiyo niliyoieleza hapo na mimi ndiye ninaetarajiwa kuwa sheria hii niipitishe na wenzangu kama mimi wangu tele humu ndani, kwamba tukubali tupitishe asilimia 80 ya pesa hizo kama shilingi milioni 43 ambapo ni kama shilingi milioni 37 tunasema hiyo tunakusudia kuweka wafalme katika nchi hii sio marais wastaafu. Enzi ya ufalme kwa kweli imekwisha. Hilo ni moja Mhe. Naibu Spika.

Jengine vifungu vya jadweli zimejieleza vizuri sana Mhe. Naibu Spika, kama utavisoma hivi utaona mstaafu awe na matibabu ya nje na ndani au nje ya Zanzibar yatakayolipwa na serikali, ni matibabu ya aina gain? Hata akijichubua huyu ni haki yake kupelekwa nje ya nchi? Lazima na mambo haya yaainishwe

kwa sababu ukisema tu matibabu ya nje na ndani hakuna *justification* itakuwaje.

Leo asubuhi na takriban Baraza lako hili kila siku tunapigania kwamba hospitali zetu ziimarishwe ili na hata marais wetu na wao si Watume hao, marais wetu ni fahari yetu kuona wanatibiwa na hospitali zilizomo ndani ya nchi na ndio hicho tunachokipigania. Huu mtindo wa kutibiwa kila kitu nje ya nchi akikohoa nje ya nchi, ,mafua nje ya nchi mambo hayo yanakwendaje? Sasa nayo pia kuwekwe aina ya maradhi ambao viongozi wetu hawa watapaswa kwenda nje ya nchi kama vile wananchi wengine nao kuna baadhi ya maradhi hapa hayawezekani nao wanasafirishwa na wao hawa lazima lielezwe vyenginevyo kuliacha wazi suala hili tuna hofu kwamba fedha za umma zitapotea sana katika *style* kama hii.

Watumishi wanne wa ndani na walinzi wawili, wasaidizi wa karibu wawili sijui ni wepi hao, katibu muhtasi mmoja, kiwango cha shilingi laki tano kwa simu tu, sijui simu hizo vipi na huyu keshastaafu yuko nyumbani anapigiwa simu mnamkerea nini jamani. Ikiwa ni ndugu, jamaa na marafiki mimi nadhani hata shilingi laki mbili tu zinatosha, ni ndugu, jamaa na marafiki tu, lakii shilingi laki tano nusu milioni hatari hiyo. Gari mbili za serikali na madereva wawili najua mama na yeye sawa hamna tatizo, usalama wa lazima, posho la petroli, matunzo ya gharama. Waheshimiwa kama tutaangalia hivi mimi nakwambieni tena hii ni hatari kubwa tutakayoizalisha hapa.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kama tutaipitisha sheria hii kwa uchumi wetu huu tulionao tutakujaona ni kiasi gani baada ya kipindi kifupi kijacho fedha nyingi zitakazotumika katika kuwahudumia viongozi hawa na viongozi hawa leo Zanzibar kama tukiangalia tuna marais wastaafu wanne, tuna mawaziri viongozi watatu waliobakia, hivi sasa waliopo ni wawili Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais pamoja na rais mwenyewe watafika siku na wao wataondoka hawa, kila kipindi tutazalisha watatu watatu sasa baada ya *double* tunakwenda *triplet* sasa ndani ya miaka 10 au 15 itakujakuwa ni balaa na hasa ukizingatia hawa huwa hawafi upesi kwa sababu wana afya nzuri, wanaokufa upesi ni watu wenye njaa njaa nje huko lakini hawa wenye shibe wanakaa sana.

Kwa hivyo, serikali itakuwa ina mzigo mzito wa kuwatunza watu hawa, naomba tena suala hilo lizingatiwe kwa upeo wa juu.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nikubaliane katika tafsiri ya neno ‘mshauri’ washauri hawa wa rais wasiingizwe kuwa ni viongozi wa siasa. Maalim Rashid Seif amefafanua vizuri sana kwa kuitumia katiba yetu hawa ni watendaji na hasa kwa kuzingatia kwamba hawa rais hakuwekewa kiwango maalum. Rais

wetu anaweza kuteuwa hata washauri mia moja na rais wetu kama mtamsikiliza vizuri anapenda sana kui-*quote* katiba, rais wetu anapenda sana kwenda kwa mujibu wa katiba, atakapoteuwa 50 na nyinyi mkimhoji atakwambieni katiba yetu ndivyo ilivyoeleza nani anaweza akambana rais. Sasa hawa kuwafanya kuwa ni viongozi wa kisiasa na wakaingizwa katika mkondo huu nakwambieni tena hiyo ni hatari na hilo ni bomu ambalo litahitaji siku moja kuripuka katika nchi.

Kwa hivyo, kwa sababu imeonekana kuwa hawa ni miongoni mwa watendaji katika serikali mimi nashauri anayemshauri rais katika masuala ya ardhi Mhe. Waziri, Alhaj Ali Juma Shamuhuna amtengee kipenu cha ofisi akae ofidini kwake, anayemshauri Mhe. Rais katika mambo ya Fedha na Uchumi Mhe. Waziri wa Fedha, Alhaj Omar Yussuf Mzee amtengee kipenu amuweke kama ni fitina wafanyiane huko huko, maana yake najua ukiweka mafahari mawili kazi yao kubwa itakuwa ni fitina tu.

Kwa hivyo, hili mimi nakubaliana nalo kwamba hawa hawafai kabisa kabisa kwa mujibu wa katiba yetu kuwa ni viongozi wa kisiasa, wanasiasa waachiwe wafanye siasa kama walivyo katika Baraza lako hili.

Mhe. Naibu Spika, jadweli la nne nalo limeelezea fomula kwa viongozi wa siasa na fomula hiyo imeandikwa x, kawaida ya x watu wa hesabu wanasema ni namba isiyojulikana, wanabaiolojia wanatwambiwa x ni alama ya kike katika kuzaliwa katika mambo ya *genetics*, lakini katika mambo ya kidunia x ni alama kwamba usipite au kitu hiki ni hatari haifai. Kwa hiyo kwa muhtaza huo huo na mimi nasema x hii haifai na hatuwezi kutunga sheria ambazo zina x hatujui maana yake haifai iondoshwe, lazima kila kitu kilichomo kwenye sheria tukijue maana yake nini, hatuwezi mkatutungia sheria namna hii.

Leo inaandikwa hapa kwamba sijui Rais wa Zanzibar kwamba atashauriana na Spika, atashauriana na Makamo wa Pili wa Rais, lakini sheria zetu zimeeleza wazi wazi kwamba rais halazimiki kufuata ushauri wa mtu yeyote. Kwa hivyo, hata makamo wa rais, Mhe. Spika akenda kwa rais hata akamshauri vipi rais atawasilikiliza akishawasikiliza kunyweni chai mwende zenu rais anaamua mwenyewe anavyotaka. Kwa hiyo haijawa hoja kwamba rais atashauriana na Mhe. Spika na Mhe. Naibu Spika, una uzoefu mzuri wa mambo haya wewe, kwa hivyo sisi hatuwezi kuruhusu sheria za namna hiyo.

Hii Mhe. Naibu Spika, inatupendelea sana sisi wawakilishi sheria hii, hii x itatupendelea sana na ndio katika muono ule ule rais kuja kutupa mapesa mengi wanasiasa hili hatulitaki, sisi tuko tayari tufe masikini kama hivi tulivyo tunaridhika wawakilishi, umasikini wetu sisi unatutosha kwa hivyo hii x ondosha kwa sababu hii tuna hofu nayo kuwa rais anaweza akapachika mapesa

kwa wawakilishi na wawakilishi nao ikawa ndio sababu ya kuuwa uchumi wa nchi.

Hili nalo hatulitaki, kama ni asilimia mbili tunaomba iandikwe pale sisi tutaridhika ni watu wa kuridhika tu hatuna tatizo, kama ni asilimia tano tuko tayari vile vile lakini x hapana kwa sababu isionekane kwamba tunakataa kwa ajili ya mafao ya marais, lakini sisi ikawa tunajipendelea aa, na sisi ndio kwanza kama alivyosema Mhe. Spika, kuna *declare interest* na hii ni *interest* yetu kifungu hiki kwa hivyo, nasema na sisi tuwekewe mambo wazi na kitajwe hasa sisi hatuna tatizo na hilo. Wawakilishi sisi ni wazalendo na tutaendelea kufa katika nchi hii katika suala hili.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nirudie kwamba sheria hii irudishwe ili ikafanyiwe marekebisho hatimaye tuwe na sheria ambayo inaweza kutekelezeka. Sote tunakubali kwamba marais wetu wamelitumikia taifa hili na watu muhimu sana na kwa vyovyote tunakubali kwamba marais hawa wanahitaji kutunzwa hilo tunalijua, lakini utunzaji wake usiwe katika kile kiwango cha kuwafanya kuwa ni wafalme, watunzwe wasifikie ile hatua ya kwenda kuomba au hatua ya kuuza mikate moto moto, hatutaki marais wetu wafikie hapo, tunataka wapewe nyumba, chakula, usafiri, maji, umeme hatuja shaka nayo na angalau *pocket* kidogo ya kujiona siku ya sikukuu kuwapa jamaa zake. Hatuna tatizo nalo lakini si katika kiwango hiki ambacho kimeainishwa katika sheria.

Nasema rais maana yake na hata makamao wa rais na hata spika, nashukuru kuwa spika wetu leo kazungumza vizuri sana. Spika wetu katuonesha uzalendo wa hali ya juu na hivi ndivyo tunavyomtaka spika awe katika hali kama hiyo, asiwe na makubwa akipewa madogo achukue lakini makubwa asiyachukue. Kwa hivyo, tunamshukuru sana Mhe. Spika, na yeye kutuonesha njia na kama wawakilishi tunaahidi kwamba tutaifuata njia ambayo Mhe. Spika, katuonesha. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwana na mimi nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sisi sote tukaweza kujumuika katika maslahi ya kupanga mambo ya nchi yetu. Lakini pia niunge mkono kwa Mwenyekiti ambaye amezungumza asubuhi kutoa ripoti yake, yale yote ambayo ameyazungumza naunga mkono moja kwa moja.

Pia niunge mkono wale wenzangu wote waliosimama kutetea mswada huu. Lakini mimi nataka niseme Mhe. Naibu Spika, kwanza nasema katika viongozi sote tunawapenda viongozi wetu wale waliostaafu na walioko madarakani,

tusitafsirike kwamba hatuwapendi, lakini tunafanya wajibu wetu kwa mujibu wa taratibu na sheria ambazo sisi ndio watungaji wa sheria zile.

Mimi kama Asha Bakari na mimi sitoupitisha mswada huu mpaka pale marekebisho ambayo tuliyatoa yarekebishwe, kwa maana kwanza haukidhi haja na tulieleza kwa makini na tukakubaliana na wakakubali kwamba tutayachukua marekebisho haya tuyarekebishe lakini matokeo yake hakuna lililokuwa. Hii yote ni kuonesha kwamba Baraza hili yale matakwa ambayo ni ya msingi yanayorekebishwa kama ni mswada wa sheria hayachukuliwi hatua ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, hebu tujiulize kweli tuko *serious* na mambo yetu? Mimi sitorejea vifungu kwa vifungu kwa sababu vimeshazungumzwa nazungumza yale ambayo wenzangu hawajazungumza, hivi kweli tuko *serious*? Nchi ndogo kama hii mimi nasema bado changa, badala ya kutetea maslahi ya wananchi na maendeleo ya wananchi tunajipangia sisi viongozi tufanye kazi tuhakikishe kwamba nchi yetu sasa hivi imefika wakati wa kujipangia viongozi maslahi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni ulitupeleka China na wewe ukiwemo pia, kwa kweli wenzetu wale wamejituma na wako *serious* na mambo yao, umepewa kazi hukutekeleza au siku nyengine huonekani, na sisi kwanza tujiulize tuna matatizo gani katika nchi yetu ambayo yanawakwaza wananchi tuweze kuyatatua japo si yote. Wameeleza wenzangu kwamba kuna skuli hazina madawati, kuna hospitali ndio kabisa vitu kidogo kidogo vinatushinda halafu bado tunapanga mambo kuwatia dosari viongozi wetu. Mimi nasema tuwashauri vizuri viongozi wetu, tukae tuwashauri viongozi mambo ambayo yataleta tija kwa wananchi na sisi ndio dhamana kwa wananchi Mhe. Naibu Spika.

Huko nje yanazungumzwa mengi kwa sababu sisi ndio tunaofuatwa, sisi wengine milango yetu iko wazi tangu enzi, milango yetu iko wazi watu wanakuja saa 24 kuuliza baadhi ya masuala haya. Sasa wakati mwengine unajiuliza kwa nini na sisi ndio tunaowakilisha wananchi Mhe. Naibu Spika?

Mhe. Naibu Spika, wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunatetea nchi hii kwa maslahi ya wananchi wetu kwanza, hatuwezi kwenda kwa utashi wa mtu.

Mhe. Naibu Spika, nilisema na mimi nitilie mkazo kwa sababu ni miongoni ambao nawaongoza asilimia kubwa katika nchi hii na ndio wenye matatizo akinamama. Sitowatendea haki kama na mimi sikuzungumza suala hili ili kutafuta utaratibu wa kuhakikisha serikali yetu inajipangia mipango mizuri kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Narudi tena Mhe. Naibu Spika, mswada huu marekebisho tuliyoyatoa hayakuchukuliwa hatua, haikuleta umakini, ni dharau, nasema urudishwe tena na serikali ipo hatupitishi bajeti hapa tukatoa shilingi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu katika mswada huu ambao kwa kweli unagusa hatima ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuzungumzia mswada huu nataka nimshukuru sana Mhe. Rais Mstaafu Dk. Amani Abeid Karume ambaye kwa kipindi kirefu cha miaka kumi ya uongozi wake hakuwa na wazo la kubadilisha sheria hii ya mafao ya viongozi wakati alijua kwamba kuna siku ama atafariki au atastaafu. Huyu ndie rais makini ambaye Wazanzibari wanamhitaji.

Mhe. Naibu Spika, miaka kumi hii ya uongozi wa Dk. Amani Abeid Karume alikuwa anajua kwamba kuna siku atastaafu na alikuwa anajua kwamba ana watoto, wajukuu na wageni. Lakini hakuzingatia hilo na akaona kwamba mwache amalize kwa sheria hii hii ambayo leo Mhe. Waziri anajenga hoja kwamba eti sheria mbaya kwa mtazamo wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niseme jambo moja la kwanza nianze pale Mhe. Asha Bakari Makame alipomalizia ni kweli kwamba sisi ambao si wanasheria tunapokea taarifa ambazo si sahihi kwamba mswada huu tusipoupitisha maana yake mimi nitarudi Kiwani na Muwambe, lakini anasahau huyu anayesema kwamba na yeye atarudi kwao.

Mhe. Naibu Spika, si wakati wa kutishana, ni wakati wa kujenga hoja kwa maslahi ya umma, wacha sote twende majumbani lakini Wazanzibari wapate salama wapate haki. Kwani sisi nani, sisi Mitume, kama lazima mtu abakie kubakia mimi na waondoke mimi niondoke, lakini Wazanzibari wanyonge Muwambe, Makunduchi na Micheweni lazima wapate haki yao.

Mhe. Naibu Spika, Katiba kifungu cha 91 kiko wazi, kifungu cha 79 kiko wazi, Baraza vipi litavunjwa kwa utaratibu gani, kwa kosa gani, si kuwa kukataa mswada ambao unaimeza Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana wale wenzangu ambao tumejaribu kutishwa tujue wajibu wetu. Tusidhani kwamba tumechaguliwa kwa uzuri au ukubwa, ni shani ya Mwenyezi Mungu na matakwa ya watu, lazima tuwafanyie haki

Wazanzibari wanyonge ambao leo hii mswada huu ukipita watamalizika haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba mimi niliwahi kusoma kidogo hesabu lakini sijamfikia kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa hesabu. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo mtaalam wa hesabu anayedhamiria kutafuta thamani ya x lakini ikawa haina jibu, labda hiyo *formula* mpya imetoka Wizara ya Fedha pengine leo imekuja mpya. Lakini miaka yangu yote niliyokaa Mbweni miaka saba sijaona *formula* hii, seuze *formula* kuifanya sheria. Maana kwenye hesabu sijaiona mimi *formula* kama hii labda kwa wale waganga wa kienyeji.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakaa Muwambe huko ndio waganga wa kienyeji wanatumia *formula* hizi za x, vichoro, mwezi, jua, hatwendi hivyo Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, kama sheria hii ni ya waganga wa kienyeji twendeni, lakini kama sheria hii ni kwa maslahi ya kisheria hii ni mpango mbaya hauna maana.

Mhe. Naibu Spika, nadhani tupige bao, kwani bao lile mlitwambia tu kwamba namba 4 ni asilimia 1, 2, 3 kwanini afiche. Hiyo baadae nasema kwa nia njema niamini.

Mhe. Naibu Spika, mimi huu mwaka wangu wa 6 kauli hiyo Mhe. Waziri naamini kwa nia njema ndio aliyozoea, lakini anambie hapo kwamba mangapi ametufanyia kwa kumuamini. Mhe. Naibu Spika, mimi sioni sababu ya kwamba atuwekee kizungu cha kiganga baadae iwe sheria. Kila mmoja ni mchunga na kuna siku kila mmoja ataulizwa kile alichokichunga.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kwa vyovyote vile hata uwe na lugha nzuri kiasi gani hauna maana kwa maslahi ya Zanzibar. Juzi tu serikali nzima hii imejenga hoja kwamba hatuna uwezo wa kuwasomesha hawa watoto wetu kwa sababu hatuna fedha, leo fedha zinapatikana wapi. Kuna tajiri wapi ambako mlisahau leo mnataka msaada ambao si rahisi, Wazanzibari hatutoelewa. Mimi naamini fedha wawakilishi wanazitaka lakini kwa ujasiri wao wamesema tusamehe fedha hizi zisije.

Mhe. Naibu Spika, nikuombe na wewe usamehe formula hii. Kaa umalize urejee Mfenesini Mwenyezi Mungu atakujaalia mengine, lakini hapa tusameheane.

Mhe. Naibu Spika, leo hii tuna marais wanne wastaafu, tuna Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Mhe. Salmin Amour Juma, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na baada ya miaka 10 tunae Dk. Ali Mohammed Shein. Tutakuwa na marais watano wastaafu, twambieni asilimia 80 ya mara 5

zipo hapa, kama zipo kwa nini hamtaki kujenga *ICU*, kwa nini hamtaki kutatua tatizo letu. Mnashindwa kutwambia kwamba fedha zipo lakini hamna haja Wazanzibari. Maana kama fedha zipo kwa nini hatuwafanyii leo hawa ili kesho na wao wanakuwa marais, ili hii asilimia 80 ya leo aje kuipata mtoto wangu mwakani nimsomeshe leo kwa fedha hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa hakika Wazanzibari walipiga kura asilimia 66 kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mategemeo kwamba wataondokana na matatizo ya shida za maisha. Mwaka mmoja balaa hii Mhe. Naibu Spika, miaka kumi kila mtu atakuwa hapa omba omba. Mhe. Naibu Spika, mimi nasema Mawaziri wasione vibaya watuelewe kwamba sisi ni waumini thabiti wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa tena pengine kuliko wao.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi mara yangu ya mwanzo mwaka juzi niliingia Kisiwandui kwa sababu nawashawishi wenzangu tuunde Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ni muumini kamili wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lakini si muumini wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuua uchumi. Kwa tafsiri yangu mimi inanambia wale asilimia 34 walioikataa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ndio mswada huu wanautaka. Huwezi kuwa muumini wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa baadae ukasaliti kwamba watu wamchukie rais. Hii ni kumchukia rais, mswada huu ukipita Wazanzibari watamchukia rais, rais ambaye sote tumeunga mkono kwamba ni Rais makini, Makamo wa Pili wa Rais ni makini na Makamo wa Kwanza ni makini. Leo hatujampa ushauri kuwa mwanasheria tayari rais anateuliwa kuwa mfalme. Tukiamua leo kwamba sheria hii ipitishwe hapa mshauri huyu atasemaje.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hatima ya Wazanzibari iko ndani ya mikono yetu na endapo mswada huu utapita tusubiri kwa Mwenyezi Mungu tukatiwe motoni kwa sababu tumeua haki na wajibu wa Wazanzibari. Sio siri leo Mzanzibari anayefanya kazi ngumu anapewa shilingi 105,000/= sawa sawa na shilingi 4,000/= kwa siku, mimi nipewe milioni 10 kwa nini, nina roho mbili mimi. Kwa hivyo, maadam Mzanzibari wa chini leo tumeshindwa kumpa mshahara angalau wa shilingi laki nne kisingizio fedha hapana, hii mtaipata wapi.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba zile milioni 19 za akiba kwenye hazina kumbe kuwafanyia viongozi ndio maana yake, inawezekana hii fedha inakaa kwa akiba inasubiri mimi mstaafu nipewe. Mimi nisipewe kwa sababu fedha ninazopata sasa hivi zinanitosha kabisa, napewa shilingi laki nane si kidogo. Siku zote mswada tunaotafuta wadau mimi nashangaa kwani Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame aliambiwa sisi wawakilishi tuna shida ya pesa, kwani sisi asitushauri, angetushauri sisi tungemwambia hatuna haja ya pesa tuachie hizi hizi. Kwa hivyo, usituombee kheri wakati sisi wengine hatutaki kheri.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu Mhe. Waziri hakuja hata kwa wadau tukamshauri akaona wawakilishi nao wanataka waongezewe mafao. Yote yale ambayo tumeyapendekeza kwenye semina hata moja halimo, ina maana ile semina ilikuwa haina maana yoyote kwa kweli inasikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba mswada huu kwa heshima zote ingawa si kawaida ya Mhe. Waziri lakini namuomba aurudishe. Si kawaida yake lakini namuomba leo afanye maajabu ya kwanza kuurudisha mswada. Niwaombe wawakilishi wenzangu kwamba mswada huu jamani hauna haja ya kuondoa serikali lengo letu serikali lazima iheshimike na kuheshimika kwake maana yake wananchi waridhike.

Mhe. Naibu Spika, jengine ukinambia nitoe asilimia 10 ya mshahara wangu mimi naujua, basi unambie asilimia 80 ya rais ni ipi. Kwa sababu kama kweli rais asilimia 80 yake ni ndogo mimi niko tayari apewe asilimia 200, lakini ukitumia kigezo cha udhaifu utwambie asilimia 80 ya mshahara wake ni ngapi. Kwa hivyo, twambie ngapi baadae tukusaidie, kama ndogo basi mimi nitawashawishi wenzangu tuongeze, lakini wasijifungie huko wakati katiba inasema kwamba sehemu ya upangaji baadae wakatwambia tumpe asilimia 80. Asilimia ya ngapi, ya 100, 200 au 2,000.

Mhe. Naibu Spika, mimi ushauri wangu ni kwamba wawakilishi wenzangu tuwe makini, tumejaribiwa katika mswada uliopita wa Utumishi wa Umma tukateleza, hapa tuwajibike vyenginevyo nchi hii na wananchi wake itaumia.

Mhe. Naibu Spika, leo hii Wazanzibari wananunua mchele kilo shilingi 1,600/=. Tumeambiwa asubuhi hapa kwamba serikali inahangaika lakini kwa sababu ni biashara huria hatuna uwezo. Mimi nafikiri na *Cabinet* ingekaa ikabuni namna gani ya kuwatatua Wazanzibari kuhusiana na matatizo ya maisha lakini wanafikiria mafao ya mbele, haya ikiwa kesho kiyama nani atakayelipwa. Kwa hivyo, wewe unaangalia mbele huko huangalii leo wananchi wetu wanafanya nini.

Mhe. Naibu Spika, nasema mawaziri tusaidieni katika hili kwa sababu si sera ya CCM wala si sera ya CUF, watu kujilimbikizia mali si sera ya CCM wala CUF. Sasa itakuwa sera ya nani ikiwa CCM na CUF hawakusema hivyo, itakuwa sera binafsi, hatuwezi kuachia sera binafsi ikatawala ikanyonya uchumi. Nasema kwamba kuna waziri mmoja alinitania akanambia makelele yenu hayo ni kwamba nyinyi mmepagawa, sawa tumepagawa lakini tunapagawa na wenzetu Wazanzibari wanyonge.

Mhe. Naibu Spika, kwa hakika na kwa busara zote mswada huu bado wakati wake tuurudisheni tuwaachie Wazanzibari kwanza wapate maisha yao,

tuwatafutie Wazanzibari elimu, maji, barabara nzuri na hatimaye huko mbele tukifika baadae tutatafuta maslahi mazuri. Lakini haiwi wenzetu leo wanalima ule mpunga haujaiva tayari unaanza kuvuna haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba kuna mwokosi mmoja kule kwetu alilima mpunga na mkewe, Mwenyezi Mungu akaujaalia ule mpunga ukaiva sana ukachanua vizuri sana, lakini kwa sababu amezoea uokosi na ubaya akamwambia mkewe ule mpunga tuugawe. Mpunga limeiva vizuri sana nerika lakini kwa sababu amezoea ukorofi ndani ya roho unamla ubaya akamwambia mkewe mpunga tuugawe, kwa nini mume wangu, leo nimekaa usiku nimeingia ashki ya kuuokota. Maana ile ashki yake ya ubaya ndio haja yake mpunga auokote, wakaugawa mpunga asubuhi yake wakauokota wote ukakauka. Mhe. Naibu Spika, niwaombe mawaziri mpunga wetu tusiiokote ni hatari kubwa, huku chini watu wanafukuzana.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu ulioko mbele yetu. Awali yote kwanza sina budi kumuomba Mwenyezi Mungu aijaalie serikali leo hii iyakubali marekebisho yetu yote katika Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Lakini pia Mwenyezi Mungu awajaalie Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi endapo serikali itakataa mapendekezo yetu basi awape nguvu ya kuukataa moja kwa moja mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, naanza kuzungumzia suala la haya marekebisho ambayo tumeletewa hapa, nina uzoefu kama mara ya tatu sasa marekebisho ya mswada wa sheria tunaletewa wakati mswada tunaanza kuujadili hapa. Hii kwa upande mwengine mimi naona kama ni dharau, serikali imekuwa ikiwadharau Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mswada huu ulirejeshwa zamani sana serikali ilikuwa na muda wa kutosha hasa kuangalia marekebisho gani Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanataka pamoja na wadau wengine.

Mhe. Naibu Spika, jengine mapendekezo yote ambayo yametolewa na wadau mbali mbali wakiwemo wanahabari, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na wananchi kwa jumla hayakuzingatiwa katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar, kifungu hichi ndicho kinachowapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuwa na nguvu ya kutunga sheria. Wao tayari walitoa mapendekezo hayo lakini kwa bahati mbaya mapendekezo hayo yote mpaka sasa hayajakubaliwa. Lakini leo hii kamati yetu imeonesha mapendekezo hayo kwamba sisi hatujayasahau na ndio tuliokubaliana katika semina iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, nikija moja kwa moja katika mswada huu kifungu cha 3 kama wenzangu walivyozungumza ni ile asilimia maalum hili lifutwe moja kwa moja lisiwemo kwa sababu itakuwa sio rahisi haki za watu wengi sana kuweza kukabidhiwa mtu mmoja. Mhe.Naibu Spika, Mhe. Rais azingatie aangalie, mimi nahisi sheria zaidi ndio iwekwe wazi na iseme bayana tusimpe mtu lawama kwa haki za watu, haki za watu zinawekwa kwenye sheria. Tukiangalia Katiba ya Zanzibar wameweka haki za binaadamu zote ziko pale katika katiba. Sasa na hili moja kwa moja liwekwe katika sheria ioneshe ni asilimia ngapi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, vile vile hapa tuangalie suala la Mshauri Maalum wa Rais. Pamoja na uwezo ambao Mhe. Rais anapewa kifungu cha 58 cha Katiba ya Zanzibar kwamba anaweza kumchagua mtu yeyote yule kuwa mshauri wake. Kwa hivyo, hapa katiba yenyewe pia haikuwekwa mipaka kwamba rais anaweza kuchagua washauri wangapi. Rais anaweza akachagua wajumbe wote hapa wawe washauri wake au anaweza akachagua watu wengine huko 300 wawe washauri, hao wote watakuwa viongozi wa kisiasa tutakuja kuwalipa vipi na wakati sheria hii haijabana imeweka uhuru moja kwa moja.

Mtakuja kumlaumu rais kachagua washauri wengi lakini sheria inamruhusu kwa sababu katiba imempa nguvu hizi. Kwa hivyo, hili nalo moja kwa moja lifutwe kabisa hao viongozi waliokuwepo wanatosha. Kwa sababu angalau wangelichagua diwani naona yanaingia akilini kwamba awe kiongozi wa kisiasa.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho tuliyoletewa hapa kifungu cha 20 (1) ambacho kinampa uwezo waziri wa kutunga kanuni. Kifungu hichi kibadilishwe sasa badala yake kanuni ambazo zitatungwa ziridhiwe na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu hizi sheria ni muhimu na nzito hatuwezi tukamuachia waziri tu yeye aangalie haki za watu na yeye aseme huko atakuja kutuletea hapa kila mtu asilimia 5 mia mbili na hiyo kanuni itakuwa imezungumza hivyo.

Nilisema kwamba tunawaamini sana mawaziri wetu lakini sisi tunaamini zaidi sheria kuliko mtu kwa sababu binaadamu anaweza kubadilika saa yoyote na hatujui tutamkosa kiasi gani. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hili nalo lizingatiwe.

Mhe. Naibu Spika, pia tukiangalia katika jadweli la kwanza linalohusu rais anapostaafu, hapa tutaangalia zaidi katika kifungu (c) na kifungu (d). Malipo ya pencheni ya asilimia 80 pengine tungeliyakubali haya na vile vile posho la kila mwezi la asilimia 80. Lakini kwa kuwa kuna utaratibu wa muda mrefu sana wa kuvunjwa Katiba ya Zanzibar na katiba hii inavunjwa pale ambapo hamna hata

mjumbe mmoja Baraza la Wawakilishi humu aliyekiri kwamba yeye aliwahi kukaa hapa akapanga mshahara wa rais na katiba hivi ndio inavyotaka.

Sasa huu utaratibu wa kila siku watu kuvunja katiba, kuvunja sheria za nchi hili ni tatizo kuna siku litafika sehemu mbaya. Kwa hivyo, mimi kwa kuwa hapa hatujaoneshwa wala hakuna historia inayoonesha hivi, moja kwa moja hapa asilimia hii 80 zote mbili katika hilo fungu (c) na (d) tutajadili la kwanza hivi vifutwe kabisa tuangalie utaratibu mwengine kama tutaweka asilimia 40 kwa sababu hatujui ndio hofu yetu. Sasa sisi tutapendekeza asilimia 40 lakini hatujui pengine asilimia 40 yenyewe milioni 500 kwa mwezi. Mhe. Naibu Spika, hapa napo tunataka hichi kibadilishwe haraka.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kwa mfumo wa sasa tulionao kuna uwezekano mkubwa sana kwa kila miaka mitano tukabadilisha rais kwa hivyo hapa tutakuja kuwa na mlolongo wa wastaafu wengi sana. Kwa sababu sasa hivi siasa zetu zimebadilika kabisa tumetoka katika karne za nyuma tumeingia katika karne ya 21 kila kitu kipya, kila mtu anajua haki zake na mambo yake. Kwa hivyo, hapa hii asilimia 80 ni kubwa ibadilishwe, itakapobadilishwa hii kwanza tulikuwa tuone kiasi gani ambacho Mhe. Rais anapata kwa sasa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile suala la Makamo wa Pili wa Rais na Mhe. Spika kushauriana na Rais juu ya mafao ya viongozi wastaafu suala hili haliwezekani si jambo rahisi. Sisi tunawaheshimu sana viongozi wetu Makamo wa Pili wa Rais lakini pia tunamheshimu sana Mhe. Spika, tutakuja kufika pahala hawa watakuja kutukanwa. Kwa sababu hizi haki za watu hapa tutakuja kuambiwa inueni maposho hayapunguzwi, unaweza ukaongezewa milioni moja au shilingi hamsini elfu ikawa imekwisha. Nani wa kulaumiwa hapa, tutakuja kuanza kumlaumu Makamo wa Pili wa Rais, tutakuja kumlaumu Spika.

Kwa sababu hapa sheria itakapobakia hivi hao binaadamu unaweza ukatokea ushawishi wowote na wao wakakubaliana na rais na kikatolewa kitu ambacho pengine ni kinyume kabisa. Kwa hivyo, sheria hapa iweke wazi moja kwa moja waoneshe asilimia ngapi ama kiasi gani kitapatikana.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nimepata marekebisho ya kifungu cha 16 kinachohusu huduma za wategemezi hapa tuna maana wakiwemo watoto. Nimesoma sheria ya mwaka 1988 inaonesha wazi pale kwamba watoto wa kiongozi mstaafu Spika, Rais na wengine endapo watastaafu watapata ile posho ya mshahara wa kima cha chini cha mfanyakazi wa serikali. Hii sheria ipo kwa sababu waziri asingekuja hapa akatwambia kwamba sheria hii ilikuwepo. Hii sheria ilikuwepo lakini kuwepo kwake je, kuna uhalali gani kutokana na mazingira ya sasa ya nchi yetu yalivyo.

Kwa wakati huo mwaka 1988 mpaka sasa hivi hata ukiangalia idadi ya watu wa Zanzibar wamezidi kwa kiasi kikubwa na tuchukulie mfano wetu kwamba sheria ipo lakini je, uhalali wa sheria hii kutokana na mazingira ya nchi yetu inakwenda sambamba.

Mhe. Naibu Spika, samahani kuna wakati Adolph Hitler walitunga sheria ya kuwaua Wayahudi na ilikuwa halali sheria ile kutumika, lakini baadae Mwanasheria Mkuu alishtakiwa na akafungwa jela kwa kitendo kile, sheria ilikuwepo lakini ilikuwa batili. Kwa hivyo, kifungu hichi kutokana na mazingira ya sasa na hali yetu ya uchumi ilivyo basi Mhe. Naibu Spika, tunaomba moja kwa moja kwamba hawa watoto watapata mirathi yao ambayo itatokana na baba yao ama mama yao ambaye alikuwa ni kiongozi hapa. Sasa moja kwa moja hapa kifungu hichi kiondoke kabisa.

Kwa sababu katika historia yetu ilivyo sasa na tunakokwenda hatutegemei kabisa kwamba atakuja pengine tujaalie Rais atoke katika wakulima wa hali ya chini kule kijijini kwangu Chaani, lakini atakuja mtu msomi ambaye ameshafanya kazi katika sehemu nyingi.

Lakini tukiangalia huku vijijini tuna watu wangapi ambao wanataka mahitaji maalum. Watoto kila siku tunawaona, juzi nilimuona Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amekwenda kutoa msaada kwa watoto wenye mahitaji maalum katika jimbo lake. Sasa wale tutawafanya nini.

Niseme kwamba endapo marekebisho ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa serikali itayazingatia basi mimi nitakuwa sina pingamizi na mswada huu, lakini endapo haitayazingatia marekebisho haya basi mimi sitokuwa pamoja na mswada huu na mswada huu kwangu mimi utakuwa batili kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni kuweza kuuchangia mswada ambao unazungumzia marekebisho ya mswada wa sheria ya kufuta sheria ya ulipaji wa mafao na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni, siungi mkono mswada huu. Siungi mkono mswada huu kwa sababu hauna manufaa kwa wananchi wa Zanzibar. Mhe. Spika, tulipokuwa tukiwashawishi wananchi wa Zanzibar kukubali mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tulikuwa tunawaambia kwamba wakubali mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu mfumo huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa utawaletea maendeleo.

Kwa bahati nzuri wananchi wa Zanzibar walitupa majaribio. Lakini Mhe. Spika, kwa bahati mbaya sana wananchi kabla ya kupata yale matarajio ambayo wameyatarajia ya maendeleo, wameshuhudia sasa serikali yao inaanza kujipangia maslahi makubwa ambayo kwa kweli ni maslahi ya kutisha. Wananchi wangetarajia katika kipindi hiki cha miaka mitano serikali yao ingewaletea maendeleo ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Magomeni hawana maji ya kutosha, wanasumbuka na maji usiku na mchana, badala ya serikali kukaa kutafakari namna ya kuondosha tatizo la maji katika Jimbo la Magomeni, leo wanakaa na kutafakari namna ya kuongeza mafao makubwa makubwa ya wastaafu. Hili ni jambo la hatari sana katika nchi kama hii yenye mfumo wa demokrasia na utawala wa sheria. Wananchi wanasumbuka sana, kila shehia utasikia wananchi wanalalamika juu ya suala la maji na tunajua umuhimu wa maji. Tungetegemea serikali itakaa kujipanga namna ya kuondosha tatizo la maji kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi hii tumekuwa tukizungumzia suala la ICU na serikali kusema kwamba haina fedha za kutosha kwa ajili ya kutengeneza ICU, huku tumekuwa tukitengeneza bakuli kuomba fedha kwa wahisani waje watutengenezee ICU. Leo inasikitisha kuona kwamba serikali inakaa kupanga na kujipangia maslahi makubwa makubwa juu ya jambo hilo. Kumekuwa kuna wananchi wengi wanahitaji kupata matibabu ya nje ya nchi kutokana na maradhi yao kuwa makubwa ambayo hapa Zanzibar hayawezi kutibika, kumekuwa na orodha kubwa ya wananchi wanaohitaji fedha kwa ajili ya kwenda kupata matibabu nje, lakini serikali inasema haina fedha. Leo tunajifungia kupanga maslahi makubwa mazito ya kutosha hapo tutakapoondoka, hili ni suala la aibu kubwa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, leo watoto wa wananchi wa Zanzibar wanakaa chini mashuleni, hawana viti vya kukalia, hakuna maabara za kutosha kwa watoto wanasoma sekondari na huku tukilalamika kwamba serikali yetu haina fedha, lakini huku tukijipangia mafao makubwa na ya kutisha. Kuna shule za sekondari kadhaa hazina maabara. Hili ni jambo la kusikitisha Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, hali ya maisha ya wananchi wetu ni ngumu, kipato chao hakilingani na matumizi yalivyo. Leo bei ya mapembe kilo ni Shs. 1,600/= wananchi hawawezi kumudu, bei ya sukari kilo ni Shs. 2,000/= wananchi hawawezi kumudu, huku tukitegemea kwamba serikali itakaa na kutafakari na kuwafikiria wananchi namna ya kufidia masuala haya ya gharama za maisha ya wananchi. Lakini leo tunakaa na kufikiria namna ya kuongeza mafao kwa viongozi wa kisiasa. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ni lazima wenzetu hawa wakae watafakari, na kwa sababu sisi ni viongozi ambao tumechaguliwa na

wananchi na wananchi wametuchagua wakiwa na matumaini kwamba tutawatendea vyema, hivyo sio busara hata kidogo kuona wananchi ambao wametuchagua kuendeleza nchi hii wakiona kwamba tunakaa na kujipangia namna ya kujinufaisha tukiondoka hapa, hili sio jambo zuri.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mswada huu unahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa ili uendane na nchi yetu, nchi yetu bado ni maskini, hatuna uchumi mkubwa, uchumi wetu ni mdogompaka leo. Kwa hivyo, tunahitaji kukaa na kutafakari namna ya kuongeza uchumi wetu. Tunajua kwamba sheria zilizopo zinahitaji kufanyiwa *amendment* na kwa sababu kuna baadhi ya maeneo yalikuwa yamemtaja Waziri Kiongozi na sasa hivi tuna Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais. Lakini ni vyema sheria hii ikaja katika yale maeneo ambayo yalikuwa yanahitaji *amendment* ili yaendane na wakati ulivyo na sio kujiongezea mafao kwa kiasi hiki. Hili jambo lazima lizingatiwe na lionekane kwamba linakwenda vizuri na wananchi wajenge imani na serikali yao na wananchi wajenge imani na Baraza lao la Wawakilishi na waone tuko pamoja katika kujenga nchi hii na kwa maendeleo yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamezungumzwa na wenzangu wameweza kutoa mifano mbali mbali juu ya mswada huu. Nakubaliana na mapendekezo na marekebisho ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, juu ya mswada wa sheria hii, mapendekezo ambayo mengi ni yenye maana na yenye msingi ambayo serikali inahitaji kuyazingatia bila kigugumizi. Ni mapendekezo mazuri ambayo kama serikali itayafuata basi mswada huu utakuwa hauna matatizo unaweza kuwa na manufaa kwa wananchi wetu na kwa taifa letu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, kama wenzangu walivyotangulia kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiwatisha wale wawakilishi wapya, wanawaambia kwamba ikiwa mswada huu wa sheria haukupitishwa maana yake Baraza la Wawakilishi litavunjwa. Nani atavunja Baraza la Wawakilishi, nani mwenye ubavu wa kuvunja Baraza la Wawakilishi, hakuna mwenye ubavu wa kuvunja Baraza la Wawakilishi. Katiba hii ya Zanzibar iko wazi na wala haizungumzii juu ya suala hili la kupitishwa mswada wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, sisi Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa ibara ya 88 kazi yetu ni kutunga sheria, haya ni mapendekezo tu yaliyoletwa kwenye Baraza la Wawakilishi na wala sio sheria. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio wenye mamlaka ya kutunga sheria na katiba hii waisome vizuri haizungumzii juu ya mswada ulioletwa. Katiba hii inazungumzia juu ya mswada uliopelekwa kwa Rais na Rais akakataa kuweka sahihi kwa mara ya kwanza na ukarejeshwa tena na Baraza la Wawakilishi likaupeleka tena mswada huo, Rais akikataa kuweka sahihi hapo anaruhusiwa kuvunja Baraza. Lakini sisi tunakataa hata

kuupeleka huo mswada kwa Rais, sasa hilo Baraza atalivunja nani. Sasa tunawaambia watu wasitishwe, watu wasitishwe na kuwacha kufanya majukumu yao, katiba hii haizungumzii hayo, sisi kazi yetu moja hapa ni kutunga sheria na tutatunga sheria yenye manufaa ya nchi hii, tutatunga sheria yenye manufaa ya wananchi wetu, tutatunga sheria ambayo haimkandamizi mtu na ndio wajibu wetu. Pale mswada wa sheria utakaowasilishwa hapa tukiuhisi una manufaa basi tutaupitisha, lakini tukiona mswada una mizengwe kama huu basi hatutoukubali kamwe.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niwasihi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi msitishwe wala msiogope hakuna mwenye ubavu wa kuvunja Baraza la Wawakilishi hata mmoja hapa. Tufanye wajibu wetu wa wananchi wetu waliotutuma hapa, tutekeleze taratibu zetu tuone miswada inayopitishwa hapa kuwa sheria inakuwa kwa manufaa ya nchi yetu na manufaa ya wananchi wetu kwa ujumla. Mswada huu hauna manufaa kwa wananchi, nchi yetu bado ni masikini mno, hatuwezi kuwarundikia mapesa watu wakawa hawana namna hata ya kuyatumia. Ni lazima tukae tutafakari, sisi sote ni watu wazima na tuna akili timamu, wananchi wetu wanatuangalia, wametuchagua lakini wanatuangalia. Wala tusifikiri kwamba tupo kwenye chombo hiki, tukawa sisi sote tuna akili zaidi kuliko wale waliokuwa nje.

Mhe. Naibu Spika, kuna watu wako nje wananchi wa kawaida wana akili kuliko sisi, lakini kuna utaratibu tu Mwenyezi Mungu ametuwekea kwamba lazima wawepo viongozi na lazima wawepo watu wanaoongozwa, tusije tukajifikiria kwamba tupo humu kwamba sisi tuna akili sana kuliko watu wengine. Wananchi wanatuangalia na wanaangalia busara zetu zilivyo na wanaangalia aah! Hivi hawa watu kweli wana busara za kutuongoza, na kwa sababu wao ndio waliotuleta humu, tusije tukafika pahala wananchi waliotuweka humu wakatuona kwamba sisi hatuna akili. Ni lazima tukae tutafakari, tujuwe jambo gani linahitaji kwa wakati upi, lipi linahitaji kusubiri na lipilinahitaji kufanyika kwa wakati huu tuliokuwa nao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nisingependa kuingia vifungu baada ya vifungu, kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wameviingia vifungu vyote, ambapo marekebisho ambayo tayari Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ameyatolea ufafanuzi. Nazungumza tena kwamba nayakubali, nayaunga mkono na ninawaomba wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi wayakubali na wayaunge mkono ili serikali iende ikarekebishe masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni nasema tena hatuungi mkono mswada huu, ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia machache juu ya mswada huu ulioko mbele yetu unahusu maslahi ya viongozi wa kisiasa pale watakapostaafu.

Mswada huu Mhe. Naibu Spika, lengo lake ni kuwa sheria pale ambapo tutaupitisha na una lengo la kufuta sheria mbili, sheria nambari 4 ya mwaka 1988 na sheria nambari 6 ya mwaka 1999. Sheria hizo ambazo zinataka kufutwa mimi binafsi nimepewa hivi punde, sijui serikali imetuona tuna akili kiasi gani kuwa jambo tunaletewa leo tupitie leo ile itakayofutwa ili tupate kuangalia ile itakayotungwa. Kwa kweli kama alivyosema Mhe. Ussi, hivi serikali inatufanyia nini. Mhe. Naibu Spika, kuna msemo wa Kipemba unasema, 'mengine enhee mengine kinehe'. Kwa hapa serikali inatufanyia kinehe.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki nichangie sana mswada huu kwa kuwa ni mswada ambao kamati yangu ilikaa siku tano sio mfululizo ni kwa awamu kujadili na kutoa mapendekezo yetu. Lakini asilimia kubwa ya yale tuliyopendekeza serikali haikuyajali. Kwa hivyo, kama yale tuliyopendekeza hayakuchukuliwa hatua, mimi sitounga mkono hoja ya mswada huu kwa sababa tutaipa serikali mzigo mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa Pemba karafuu zetu tunakopesha. Ukiuza leo, wala huambiwi kwamba hakuna pesa, mpaka wameshazipima na kuzitia ndani ndio wanakuambia njoo uchukuwe pesa keshokutwa. Hii ina maana pesa haipo tusingekopesha, lakini tunaandaa utaratibu, kwa lugha yenu watu wa sasa, kuboresha maslahi ya viongozi wa kisiasa, kama alivyosema Mhe. Rashid Seif waishi raha mustarehe. Mimi sipingi kuwa waishi kwa raha, lakini ile raha yao isiyokuwa na karaha ndani yake.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu una majadweli manne sitaki niyapitie kifungu baada ya kifungu kwa kuwa sehemu kubwa ya yale ambayo yamo katika jadweli hili kamati yangu imetoa mapendekezo yake ya kutaka ama yafutwe au yafanyiwe marekebisho. Huko nyuma kabla serikali haijafanya marekebisho haya ya mwisho, ilikuwa hao watoto wa viongozi wakuu wastaafu watahudumiwa hadi pale watakapofika miaka 18. Lakini katika marekebisho ya serikali wameona, hapana, kumbe tutawapunja tuwachukuwe hadi miaka 20, maana yake serikali imeona miaka 18 ni kidogo. Sisi tunataka iondolewe kabisa, serikali inatuambia nyinyi kama mnataka tuiondowe basi sisi tunawapa miaka 20. Kwa mwanamke kama ataolewa kabla ya hapo basi, na kwa mwanamme hadi atimie miaka 20 ndio haya yakatike kwa upande wake.

Mhe. Naibu Spika, serikali pamoja na kuwa ina nia ya kuwasaidia viongozi wastaafu, lakini pia itazame vile vile uwezo wa nchi ulivyo. Kuna watu hapa

ambao ni washauri maaluma wa Mhe. Rais na wameingizwa katika mlolongo wa kisiasa kuwa ni viongozi wa kisiasa. Mimi ni mwakilishi wa kuchaguliwa wa Jimbo la Mtambile na nipo katika Baraza hili kwa hivyo ni kiongozi wa kisiasa. Waheshimiwa Wajumbe wengine ama kwa kuteuliwa au kwa kuingia katika nafasi zao, lakini hatimaye wakaapishwa kuwa ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kadhalika na wao ni viongozi wa kisiasa. Lakini huyu mshauri maalum wa Rais huo uwanasiasa kaupata wapi, ni mshauri wa Rais lakini sio mwanasiasa, kwa hivyo hawajibiki kuingizwa katika mlolongo huu wetu sisi hapa. Serikali imtafutie pale anapostahiki umuweke. Rais ana haki ya kumchagua atakaye kumpa kazi, kwa sababu katiba imemruhusu. Halafu katika jadweli moja wapo serikali katika marekebisho yake imesema katika ile asilimia maalum kuwa Mhe. Rais atashauriana na Mhe. Spika wa Baraza na Mhe. Makamu wa Pili, lakini katiba hii ya Zanzibar kuna kifungu hiki cha 52. Mhe. Naibu Spika, naomba nikinukuu.

Kifungu cha 52

> “Rais wa Zanzibar halazimiki kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote katika utekelezaji wa shughuli zake, isipokuwa kama sheria itaagiza vyenginevyo”.

Kwa hivyo, anaweza akashauriwa na Spika na Makamu wa Pili, lakini hatimaye akaamua atakavyo mwenyewe, kwa sababu halazimiki kufuata ushauri wa mtu yeyote. Kwa hivyo, serikali kutuambia kwamba musiwe na wasi wasi kwa sababu Spika yuko, Makamu wa Pili yupo, Rais ndiye mwenye mamlaka ya mwisho.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa leo na kwa mswada huu sitaki niseme mengi, kwa sababu tumeshaongelea sana katika kamati, tushaelekeza sana katika kamati na matokeo yake marekebisho serikali iliyofanya ndio hayo ya kumuondoa mtoto wa miaka 18 na ikamsogeza mpaka miaka 20, ya kuweka pazia baada ya kurudisha kima cha chini cha mshahara sasa wanasema kuwa atahudumiwa na serikali. Ni hayo hayo maji ya futi na nyayo. Kwa vyovyote hapa tunatumia pesa ya serikali bila ya kutazama uwezo wenyewe wa serikali ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, serikali itazame shilingi katika pande zote mbili. Shilingi yetu ina mwenge japo haitumiki hivi sasa upande mmoja na upande wa pili ina uso wa mwalimu nyerere. Kwa hivyo, serikali iangalie shilingi hii katika pande zote mbili, upande wenye mwenge usome kuna nini na upande wenye mwalimu usome kuna nini. Wakiwa upande mmoja tu na hatimaye wakaja kwenye mswada huu kutaka sisi tuupitishwe uwe sheria ni kuvisha serikali kaa la moto kichwani, kwa sababu itafika pahala nusu ya bajeti ya nchi hii iwe inawahudumia viongozi wastaafu. Kwa sababu Alhamdulillah Wazanzibari tu

wazazi sana. Humu waliokuwa hawana watoto labda waliokuwa hawajaoa au hawajaolewa na wengine miongoni mwetu wanaweza wakashika hii nafasi ya Urais na umakamu wa kwanza na wa pili wa Rais na uspika.

Mhe. Naibu Spika, Mtu anafariki ana watoto 18, 12 *under* 20, serikali iwatazame kwa miaka 20 kutakuwa kuna mlolongo wa hawa wastaafu. Kwa hapa serikali imetazama shilingi kwa upande mmoja tu, sina hakika imetazama kwa upande wa mwenge au kwa upande wa mwalimu, lakini wametazama shilingi kwa upande mmoja, hivyo ningeiomba serikali na kwa upande wa pili wa shilingi iutupie macho.

Mhe. Naibu Spika, kama serikali itakubali yale mapendekezo ya kamati yetu, basi itaunga mkono mswada huu, vyenginevyo pamoja na kuwa nimeukalia siku tano siungi mkono hoja hii bila ya marekebisho hayo, ahsante sana. *(Makofi)*.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, na mimi kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Allah kwa kunipa uwezo na afya njema nikatimiza ile azma yangu ya kufika hapa na kufanya kazi niliyotumwa na wananchi waliyonichagua.

Lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipa hii nafasi, kama usingeamua kunipa nisingepata fursa ya kuchangia, lakini nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Naibu Spika, wenzangu waliotangulia takriban wamesema mengi na nataka niseme wamenipunguzia kazi kubwa sana, nikuwa na maneno mengi ya kusema lakini sasa nitasema machache.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tunawaongoza watu ambao wao wenyewe wako *conscious* kweli kweli na mambo yanavyokwenda hapa nchini. Nakumbuka siku za nyuma kidogo tuliwahi kupitisha mswada hapa tukapata tabu kidogo huko uraiani, ule mswada uliokuwa unagusia habari ya mirathi pamoja na mambo mengine ambao ulikuwa umechanganya itikadi zote mbili. Kwa kweli tulijieleza kadri tulivyojieleza na kutetea hapa vya kutosha, lakini hatimaye tulipotoka huko nje tulipata tabu sana.

Sasa ili kuonesha Wazanzibari haya tunayoyaamua hapa wanayasikiliza kwa makini kweli na wao tusijetukashangaa siku nyengine wanao upeo mkubwa zaidi wa kufahamu kuliko sisi tuliomo humu.

Kwa hivyo, tunapoamua mambo lazima tuwe makini sana, vyenginevyo tusijetukakumbwa na ile dua aliyoitahadharisha Mhe. Hija Hassan Hija, yaani tukaja kufanya jambo na halafu ikawa mzigo mkubwa kwa serikali, maana

yake wananchi wanaweza kuichukia serikali kwa mambo ambayo tunayoyapitisha kama hatukuwa makini.

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba Mafao ya Viongozi Wastaafu kama ni wa kisiasa ama wafanyakazi, yaani mafao ni jambo ambalo haliepukii, Kiinua Mgongo pamoja na masuala ya pencheni ni mambo ambayo hayaepukii, kwa sababu ni mambo yapo tena ni haki zetu tunastahiki kuzipata kwa hali yoyote.

Kwa hivyo, nafikiri baadhi ya Mawaziri wanaweza kuwa mashahidi kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi mpaka leo wana malalamiko, kwa sababu walifanyakazi serikalini lakini wakastaafu na wala hawakulipwa haki zao ipasavyo na mpaka leo na kesi hizo ninazo nyingi. Sasa hii ni kuonesha kwamba ni haki.

Lakini na *special* kwa mswada huu wa leo katika kuitekeleza haki hiyo, basi ni vizuri tukaangalia *position* ya uchumi wetu kwanza hapa nchini ulivyo, tukeshajua mwenendo wa uchimu wetu ulivyo ndio tunaweza kuona kwamba hiki ambacho tunakipanga kinastahiki. Je, hakitaleta wivu kwa wenzetu, je hakitatufanya sisi tutukanike, maana kufanya jambo ambalo haliingii akilini mara nyengine unaweza kuwapa watu fursa wakuone wewe si mtu wa maana.

Kwa hivyo, ni vyema tuangalie hayo, yaani tuangalie kipato cha wananchi wetu kikoje, maana tafsiri yangu niliyoileta mimi kwa haya niliyoyakuta kwenye mswada huu.

Kwa kweli ni kama familia moja ambayo inahitaji kula kilo nne za mchele wa Mapembe kwa siku, lakini haitizimi kilo nne ikapata kilo tatu kwa mfano, maana yake nini? Watu wote watakuwa hawashibi mule ndani. Lakini baba akasema aa! Wacha mimi nile mpaka nicheue na chengine niweke uporo kesho, kitakachobakia ndio mule nyinyi watoto. Sasa hii nadhani haitakuwa busara hata kidogo.

Kwa hivyo, ni vyema viongozi kupangiwa mafao na kweli viongozi wetu wanayo kazi kubwa sana katika nchi hii, yaani wanaitumikia jamii kwa kutumia akili zao, muda wao pamoja na kila kitu chao na hivyo tunayo haki ya kuwatunza. Lakini matunzo yawe yale yanayolingana na nchi yetu ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi nachelea kusema siukubali mswada huu, maana yake nikisema hivyo ni sawa na kusema viongozi hawastahiki mafao, kwa hivyo, nachelea kusema hivyo.

Lakini kuna wenzangu walisema mswada huu ni bora urudishwe kwanza, kwa sababu hata ukiangalia ile ripoti ya kamati ina marekebisho mengi sana sasa si

jambo la kusema aha! Basi tuupitishe hivi pamoja na marekebisho yake, kwa kweli haya marekebisho ni mengi kuna haja ya mswada huu kuandikwa upya. *(Makofi)*

Sasa mimi sisemi kama siukubali, isipokuwa nasema kwanza urudishwe na nimejaribu kuangalia mambo kwa haraka na kusema kuwa mswada huu hauko wazi na hata Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitumia neno bubu, yaani tunapitisha mswada bubu. Kwa mfano, yamo maneno humu kama vile "Asilimia Maalum" na watu wengi wameshasema kuwa irekebishwe, maana yake iwekwe wazi ni asilimia ngapi, kwa sababu huu ni wakati wa ukweli na uwazi. *(Makofi)*

Vile vile tumeambiwa katika kifungu cha 19 hayo mafao ambayo Rais ataamua basi yasiwe pungufu ya kiwango kile cha kiongozi, yaani yale mafao yaliyopita yasiwe pungufu. Sasa hiyo bado haijawa wazi na mambo kama hayo lazima yarekebishwe.

Mhe. Naibu Spika, leo nimeshtuka sana na nimefika pahala na kusema basi kuupitisha mswada huu hivi ulivyo ni kwenda kinyume na Katiba yetu ya Zanzibar na hakuna kosa baya kama kwenda kinyume na Katiba.

Nilifika kusema hivyo kwa nini, kwa sababu wenzangu walisoma hapa kifungu cha 35(1) cha Katiba ya Zanzibar kwamba Mshahara wa Rais lazima uthibitishwe na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, hili halijafanyika mimi tokea niwepo katika uhai wa Baraza nina miaka 15 hivi sasa na wala sijaona hata siku moja kuletewa na kuambiwa Mshahara wa Rais ni huu mnaukubali au mnaukataa, yaani hatujafanyiwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, serikali inaendelea kuvunja Katiba muda wote huo. Sasa na sisi kwa sababu wakati hivi sasa umefika, tukilikubali hili bila ya kuidhinisha huo Mshahara wa Rais na sisi tunaisaidia serikali kuvunja Katiba. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sidhani kama kuna haja ya kuendelea kufanya hivyo, kwa sababu hiyo basi hata tukisema kuwa Rais akeshakustaafu Kiinua Mgongo kiwe sawa na asilimia 50 mara hiyo miezi aliyotumikia. Sasa hii asilimia 50 ya kiasi gani? Hatujui. Kwa maana hiyo, bado naendelea ku-*prove* kwamba huu mswada bado ni bubu hauko wazi.

Vile vile tukisema Rais au Kiongozi yeyote wa Kisiasa apewe pencheni ya asilimia 80 ya Mshahara wa Rais ambaye yupo hivi sasa lakini hatuujui. Mhe. Naibu Spika, tukienda kwenye Jaduweli Nam. 4 kuna X *percentage*, yaani

haijulikani. Sasa mambo haya hayakowazi na kama hayakowazi tukaendelea kupitisha mswada huu, ndio yale aliyosema Mhe Ismail Jussa Ladhu kama tunapitisha mswada bubu**.**

Kwa kweli mambo haya yanaweza kusababishwa *violence* huko usoni, kwani mtu anaweza kufanya anavyotaka, kwa sababu sheria hii itakuwa haibani afanye vipi. Kwa kuwa mambo ni mengi ya kufanya, basi ni vyema mswada huu tunaukubali, lakini kwanza urudi na si hivi sasa, yaani serikali ikauandike upya na halafu ndipo watuletee.

Mhe. Naibu Spika, nataka niipongeze sana Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, wamefanyakazi kubwa tena nzuri. Kwa kweli wameyaainisha mambo mengi ambayo walisema wao yatolewe, sasa ukiyachukua haya yote karibu mambo sita nimeyaandika hapa kwamba haya yafutwe katika mswada huu pamoja na haya ambayo nimeyaeleza hivi punde hayakowazi, ndipo inapokuja ile mantiki kwamba huu mswada ni afadhali wende ukaandikwe upya.

Vile vile niliangalia kidogo Jaduweli Nam. 1. Mhe. Spika, najua kwamba tulisema viongozi wetu lazima tuwatunze, lakini matunzo yawe yale ya kumfanya mtu asihangaike kimaisha. Sasa haya yaliopo hapa ukiyakusanya yote, basi sikumfanya asihangaike kimaisha tu, lakini ni kumfanya awe tajiri kuliko mtu mwengine yeyote hapa nchini.

Kwa hivyo, kwenye jaduweli hili kuna marekebisho mengi sana ambayo yanahitaji kufanywa. Kwa mfano, mimi nili-*propose* na kusema na wala sikugusa kiinua mgongo, kwa sababu kiinua mgongo ni jambo la mara moja mtu akeshakupokea ndio basi kimekwisha wala posho la kumalizia muda, lakini pencheni ni suala la kuendelea asilimia 80 ni kubwa sana na huyu ni Rais wa pili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, utakuwa na Rais wa Kwanza ambaye yupo kwenye Madaraka na Mamlaka ya Maamuzi, lakini kutakuwa na marais wengine kadri wakati utakavyokuwa, kwa sababu ni vipindi vya miaka 10, basi siku moja tunaweza kuwa na marais 10 katika nchi hii na hiyo ni hatari kubwa.

Mhe. Naibu Spika, pia nikasema hata posho la matunzo asilimia 80 ni kubwa ipunguzwe angalau ibaki asilimia 50.

Kuhusu suala la nyumba, mimi nyumba ninayo je rais. Kwa kweli mimi ninahakika kila Rais wetu ambaye atakaa katika kiti cha urais mpaka akamaliza

muda wake, basi huyo anayo nyumba nzuri sana ya kuishi. Sasa hili litolewe kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nilipata *challenge* hapa kuna Mhe. Mjumbe mmoja ameninong'oneza hapa kwamba kuna Rais Mstaafu X amestaafu hata nyumba ya kuishi hana akenda kubakia kwenye nyumba yake ya zamani. Sasa suala hilo liangaliwe kama Mhe. Rais amestaafu ikaonekana hana nyumba si tatizo na apewe nyumba, lakini ikionekana anayo nyumba basi hiyo nyumba yake iwe inatosha katika kubana matumizi, kwani huu ni wakati wa kubana matumizi, nchi yetu uchumi wake ni mbaya.

Kwa kweli haya nisingekuwa na pingamizi nayo hata siku moja Mhe. Naibu Spika, kama ingekuwa tayari nchi hii tunachimba mafuta na kiwango chetu cha uchumi kiko juu na wala sina *problem*. *(Makofi)*

Lakini kila kukicha tunasikia wenzetu wanaomba hivi sasa na sijui ile jawabu itakuja wakati gani, yaani watu wanataka huu ukanda wetu wenye mafuta wauchukue wao na halafu sisi tunajipangia mambo haya, nadhani hayawi haya. Mhe. Naibu Spika, huwezi kupanga bajeti kama huna fedha, kwa sababu matumzi yaoane na hali ya uchumi ilivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nafikiri haya marekebisho ni vizuri Mhe. Waziri akayachukua kwa ajili ya kwenda kuuandika tena mswada huu vizuri. Vile vile nadhani ikiwa Mhe. Waziri atafanya haya, basi Waheshimiwa Wajumbe hawana tatizo kama tulivyosema kuwa na sisi maslahi yetu yamo humo. Sasa kama yakipangwa vizuri basi nafikiri kupitisha mswada huo utakaokuwa na marekebisho haya mbona litakuwa jambo rahisi sana.

Kwa hivyo, ni vyema kufanya hivyo na wala tusisababishe matatizo, kwa sababu najua tumo katika nia njema sana na tokea tuanze Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa tutaona kwamba tumekuwa na ushirikiano mkubwa sana, kwani tumepitisha pamoja na kuamua mambo mengi ambayo ni mazuri tena ni mazito kwa sababu ya umoja wetu. Sasa tusitie ufa hapa katikati ikaja ikaonekana kati ya serikali na *backbenchers* kuna *tag of war* hapa katikati kuna jambo baya lisiwepo.

Kwa maana hiyo, nadhani serikali ikubali kwenda kurekebisha na halafu watuletee kitu ambacho tukikifanya na wale ambao tunawaongoza watakubaliana nacho, ili tuendelee kwenda vizuri katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kwa ninavyomjua Mhe. Waziri, maana kwanza anakuwa mbishi, lakini akiona kweli watu wame-*determine* basi

anakubali upesi, hivyo ninahakika atakubaliana na haya kwa ajili ya kwenda kufanya marekebisho na baadaye kuuleta tena. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii ya leo kunipa na mimi fursa ya kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu kuhusu Maslahi ya Viongozi mwaka 2012.

Vile vile na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukadiriki kuingia katika mwaka huu wa 2012. Kwa hivyo, Inshaallah nawatakia heri wote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wananchi wa Zanzibar pamoja na viongozi wetu.

Kwa kweli naomba niungane na wenzangu niseme kabisa kwamba mswada huu siungi mkono kwa sababu zangu maalum. Mhe. Naibu Spika, mimi siku zote humu Barazani nikizungumza mnaniona kama huwa ninafanya mas-hara wakati mwengine, lakini huwa sifanyi mas-hara, isipokuwa huwa ninasema kitu nikiwa *serious*.

Kwa mfano, kuna kipindi nilizungumza hapa na kusema jamani serikali yetu tusiifanye Babu Mkongwe Miujiza. Mhe. Naibu Spika, Babu Mkongwe Miuzija achukua chanja haliwezi anachukua na gogo ajiegemeza. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa ninayo maana yangu maalum kusema hivyo. Mhe. Naibu Spika, kipindi hiki tulichonacho wananchi wa Zanzibar walikuwa na matumaini makubwa ya Serikali yao ya Umoja wa Kitaifa hii. Lakini katika kipindi tulichonacho bado tunakabiliwa na matatizo mengi katika nchi yetu tena wananchi wanayo matatizo makubwa.

Wakati tunapozungumza tunasema kwamba serikali yetu haina fedha. Kwa mfano, kuna matatizo mengi kama vile hospitalini, skuli na baadhi ya sehemu nyengine ambayo yanatushinda kuyatatua.

Kwa hivyo, leo hii tunafanya kitu ambacho hata hao wananchi wetu hawatuelewi tunafanya nini, kwa sababu hao wananchi wakitusikiliza tunachokizungumza, basi inasikitisha na kuhuzunisha. Wakati huku hospitali hazina dawa na skuli watoto tunashindwa kuwasomesha, leo hii Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba kuna mabanda yaliyojengwa kipindi hiki basi yote hayakuezekwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Sasa leo tunakaa hapa tunapitisha mafao ya viongozi ambapo tukitizama hatuwezi hata kuyahudumia hayo mafao yenyewe, hivi tunataka kufanya miujiza, yaani hii serikali yetu inataka kufanya miujiza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kumbe serikali yetu inayo fedha lakini haitaki kuzitumia kwa ajili ya wananchi, kwa sababu kama hatuna fedha tusingepanga mipango hii. Lakini naamini kwamba serikali inazo fedha, isipokuwa inawafanyia kusudi wananchi wake wadhalilike. *(Makofi)*

Kwa kweli sisi hatukatai kuwahudumia viongozi wetu wastaafu, yaani tunataka viongozi wetu wastaafu wahudumiwe tena waenziwe, lakini si kwamba wapewe ufalme au utajiri, kwa sababu huu ni utajiri tunaowapangia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hakuna Rais hata mmoja anayekaa madarakani mpaka akamaliza muda wake ikawa hana nyumba, gari. Lakini leo tunapanga tena tumpe pencheni ya asilimia 80 ya Mshahara wa Rais ambaye yuko madarakani, halafu walipiwe watumishi wanne, apewe walinzi wanne, apewe gari mbili walipwe watoto wake wote. Sasa hawa wananchi wakitusikia tukizungumza, basi wao wanasikitika na wanaona kama sisi tunawafanyia mas-hara. *(Kicheko/Makofi)*

Nadhani tunafanya mambo tusifanye mas-hara tutakwenda kuulizwa na Mwenyezi Mungu, kwa sababu Mwenyezi Mungu ametuweka sisi kama viongozi na sote tunakwenda kuulizwa kutokana na uongozi wetu tulionao, mbona tunakwenda hivi jamani. Tusifanye mas-hara twende kwa kuwainua wananchi hali zao, kwa sababu watu hivi sasa wataabani Mchele wa Mapembe shilingi 1,600/= na wala watu hawadiriki kuyapata hata mara moja. *(Makofi)*

Sasa leo wakisikia tunawapangia viongozi ambao tayari wameshakuwa na mali huku nyuma tunawapangia tena wakuongeza utajiri, hivi tunaelekea wapi? Tusifanye mas-hara. *(Makofi)*

Jambo la kusikitisha zaidi kuna Kamati ambazo ni za Baraza la Wawakilishi zinakaa kwa ajili ya kushauriana na serikali, wametoa mapendekezo basi mapendekezo yao yote waliyotoa ni mabaya hakuna hata moja ambalo ni zuri. Kwa kweli yote yameachwa na serikali imeona kama hawana maana hata kidogo, basi hatuna maana ya kwenda kwenye Kamati na badala yake serikali ikae tu na kuamua mambo yake. Lakini Kamati imekaa na kutoa mapendekezo basi yote ni mabaya hakuna hata moja ambalo ni zuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba wanasheria hawakuwashauri vizuri viongozi wetu, kama wangewashauri vizuri basi mswada huu usingeletwa kwa hivi ulivyo, kwa sababu hivi sasa serikali iko katika hali ngumu na tunalenga

kuwanasua wananchi, ili yale matumaini waliyonayo yarudi kidogo, kwani sisi kila tunapopita tunaulizwa jamani serikali hii tulikuwa na matumaini, lakini mbona hivi? Sasa lini tutapata uokozi.

Kwa mfano, juzi tulipata ajali ya meli kuzama ya *MV. Spice Islander I* na tulisema inunuliwe meli na serikali imesema haina fedha za kununulia meli, wakati wananchi wetu wanapata shida. Sasa leo hii tunapanga sisi tugaiane fedha nyingi na mimi fedha hizo nisipewe. *(Makofi)*

Vile vile nawashawishi wenzangu kuhusu mswada huu tusiupitishe na tukiupitisha wananchi wetu huko vijijini tutakakorudi na wala hatutakaa humu Barazani tu, isipokuwa tutarudi vijijini na tutaulizwa na wananchi tumewafanyia nini na wao wametutuma nini. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ninawashawishi mswada huu kwanza tusiupitishe mpaka utakaporudi kwa ajili ya kwenda kufanyiwa marekebisho na wala sio siku hizi isipokuwa ni baadaye ndizo siku za kuleta mafao ya viongozi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu pamoja na viongozi napenda kusema hivi, tunapolifanya jambo basi ni vyema tulifikirini kwanza, kwa sababu mambo kama haya ni aibu na wananchi wakitusikia ni aibu na wala tusifanye mas-hara jamani. Kwa maana hiyo, kama fedha zipo basi tuzitoe kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

Kwa mfano, Mhe. Mjumbe mmoja aliuliza swali hapa kwamba jamani wakati huu mchele ni ghali duniani, serikali haioni kama iko haja ya kusaidia wananchi. Sasa jibu ni kwamba wafanyabiashara ni watu binafsi na wala hawawezi kusaidiwa. Mhe. Naibu Spika, hivi unapomuona mwananchi wako anateseka huwezi kumsaidia, nadhani serikali itoe rai ya kuwasaidia wananchi.

Sasa ikiwa Rais Mstaafu ameshapewa nyumba, magari, matibabu, huduma ya umeme, tena hizi fedha zote anazopangiwa za asilimia 80 anakwenda kuzitumia nini. Kwa kweli matumizi yote tayari ameshapangiwa, kama vile chakula, matibabu, fedha za simu, nyumba ya kulala, hivyo tunapanga tena tumpe ofisi na baadaye tumpe na fedha kila pahala asilimia 80 anakwenda kuzifanyia nini au akaweke mabenki ya nje kwa ajili ya kuwa tajiri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hatukatai viongozi wetu kuwaenzi, kuwatunza pamoja na kuwalea, lakini tuwatunze viongozi wetu kwa vile inavyostahiki kuwatunza na wala tusifanye kitu ikawa tena ni ria na Mwenyezi Mungu anatukataza kufanya ria. Kwa maana hiyo, haiwezekani tumpe mtu fedha mpaka zizidi, kwani wananchi wanashida na vyema ni kuwasaidia hao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sitaki niseme sana naona bora yanatoka hayo namalizia. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami kupata fursa hii ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa.

Mhe. Naibu Spika, kama wenzangu walivyotangulia kusema basi kwanza kabisa na mimi siungi mkono mswada huu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama tutakumbuka viongozi waliochaguliwa wamechaguliwa kwa njia ya demokrasia, yaani wamechaguliwa na wananchi wetu wakiwa na imani nao kubwa kwamba wanapochaguliwa wataleta maendeleo makubwa kwa wananchi wao, lakini ukizingatia mswada huu tunaanza kupoteza mwelekeo.

Kwa kweli kama alivyozungumza Mhe. Mjumbe mwenzangu aliyeondoka hivi punde kwamba hatukatai kuwa mtoto yeyote akeshafanyakazi kupewa mafao yake ni haki yake, lakini isiwe israfu. Sasa hapa imeshapangwa na wenzangu wengi wamenukuu mambo hayo mpaka watoto wa viongozi wenye chini ya umri wa miaka 18 walipwe mshahara wakati wazee wao wako madarakani hawana mshahara, sasa na wao wanapatiwa ajira na hili ni tatizo. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wanayo matumaini sana na Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa, lakini sasa tunaanza kuwapoteza mwelekeo na matumaini yao ni kuona kwanza tumeingia ndani ya mwaka huu tukiona Zao la Karafuu limepanda bei na kweli wamepata matumaini makubwa sana.

Kwa hivyo, pamoja na matumaini makubwa sana, lakini asubuhi ya leo hii Waheshimiwa Wajumbe walioiuliza maswali waliuliza bei ya zao la mwani. Sasa zao hili halina bei, nadhani ni vyema kutatufa masoko kwa ajili ya kuwajenga wananchi wetu, badala yake tunajipangia mafao sisi viongozi na hili ni tatizo tena ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jimbo langu lina historia, yaani kila kiongozi wa kisiasa ambaye anayeondoka madarakani basi hana chochote cha kutumia na wala mimi sitoona tatizo hapa kuondoka nikarudi kwenye uvuvi tena, lakini wananchi tuone wamefaidika. Sisi tumeletwa hapa na wananchi na tunazo sababu za kuwatetea kwa hali na mali bila ya kufanya hivyo itakuwa hatujawatendea haki wananchi wetu. *(Makofi)*

Nadhani niseme tu kwamba tumeanza vizuri na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kama tumeshaanza vizuri, basi tusirudi nyuma kwani tukirudi nyuma tutawakatisha tamaa wananchi wetu, kwa sababu mazuri yote tuliyoyafanya

hapa kama Mchele wa Mapembe haujapungua bei, basi bure hata tukafanya nini hatuna zuri. *(Makofi)*

Tunashukuru kwamba serikali yetu imejipanga vizuri, imekipa kipaumbele kilimo kwa ajili ya kujikwamua na matatizo hayo. Lakini bado hatujafika hatua viongozi tunajipangia maslahi ambayo ni makubwa sana. Kwa kweli suala hili halipendezi kwa nchi ya demokrasia na iliyochaguliwa na wananchi, nafikiri ni vyema kuwafanyia wananchi wema na wewe ukaondoka madarakani unasemwa kwa wema, yaani ni utajiri usio malizika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, niseme katika hili mswada huu tunamuomba Mhe. Waziri arudi akafanye marekebisho tena makubwa, pia tunaomba kwa mwaka 2012/2013 usiletwe mpaka mwaka 2014, kwa sababu bado ni mapema. Kwa kweli hatuoni tabu viongozi wetu kupata asilimia 100, lakini kwanza wananchi, yaani wananchi wakeshafaidika basi na sisi hatuna matatizo na yote watayasahau, isipokuwa kujilimbikizia mali sisi viongozi tu haipendezi.

Sasa kama haipendezi basi jambo hili Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tusiliunge mkono na wala tusilipitishe, kwa sababu tukipitisha mswada huu itakuwa hatujawatendea haki hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tunayo matumaini makubwa sana na kama tunayo matumaini makubwa basi wananchi wetu tusiwarudishe nyuma tulikotoka, kwa sababu hivi sasa wananchi wametulia na tumepata utulivu katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni jambo jema sana. Lakini hili tutaanza kufanya makundi ya hapa na pale. Tutarudi kule kule tulikotoka, kwamba mwananchi kama hajafarijika basi hakuna utulivu, hata wewe binafsi kama hujatulia hujapata utulivu basi kutakuwa na makundi.

Mheshimiwa tunaomba tena na nasema tena Mswada huu urudi ufanyiwe marekebisho makubwa wala sio marekebisho ya kupitisha vifungu pamoja na marekebisho yake hayafai. Urudi hasa ufanyiwe marekebisho makubwa.
Mhe. Naibu Spika, mengi yamezungumzwa sina haja ya kuogelea sana kwa sababu watu wameshazungumza mengi na ni hayo kwa hayo. Ishallah Mwenyezi Mungu amjaalie Waziri wetu awe na hekma na busara, arudi kuja kufanya marekebisho. Kwa haya machache nasema ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, napenda kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuzungumza juu ya Mswada huu. Lakini kabla sijasema hivyo napenda nichukue nafasi hii ya kuwatakia kheri ya 2012 kwa sisi wajumbe sote tuliokuwepo hapa, pamoja na wafanyakazi wa Baraza hili na wananchi wetu kwa ujumla. Mwenyezi Mungu

aujaalie mwaka huu uwe na kheri na sisi na utupe maendeleo na faida kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika Mswada huu napenda kwanza niseme mambo mawili na pengine hayo mambo yangu mawili ndiyo yatakuwa mchango wangu kwa Mswada huu.

Kwanza ni suala la ujumla ambalo waheshimiwa wengi walizungumza. Mswada huu ambao upo ni Mswada ambao unarekebisha au unafuta Sheria Nam. 6 ya mwaka 1999 na Sheria Nam. 4 ya mwaka 1988. Sheria hizi mbili ambazo zinafutwa na Mswada huu ni sheria ambazo ziliweka mafao kwa viongozi wa kisiasa. Sheria hii mpya tunayoijadili hivi sasa ni sheria ambayo inataka kufuta sheria zile mbili na kuiweka hii kwa niaba ya zile sheria mbili ambazo zilikuwepo.

Mhe. Naibu Spika, tunapofanya masuala yoyote katika sheria tunapofuta, ni vyema na hapa nawaomba waheshimiwa Wawakilishi wasende katika Mswada ule ambao umeletwa tu katika Baraza. Ni wajibu wao na ni jukumu lao kwenda na kutizama katika ule Mswada ambaoumefutwa au unataka kufutwa.

Mhe. Naibu Spika, hapo mwanzo kulikuwa kuna matatizo kidogo. Lakini tutakumbuka Waheshimiwa Wawakilishi walitaka kupewa sheria zote zilizotungwa katika Baraza lako kuanzia ya 1964 mpaka leo. Kazi hiyo tuliifanya, kwa hivyo kila mtu anacho kitabu hichi. Kwa hivyo ni jukumu la Mwakilishi kutizama sheria ile ipo mwaka gani na ipo mahala gani, ili aweze kupitia na kujua ni kitu gani ambacho kinafutwa.

Mbali na hivyo Afisi yetu hii ya Baraza la Wawakilishi kuna washauri wa kisheria, kuna na *library*. Kwa hivyo mwakilishi anaposema kwamba hana sheria inayotaka kufutwa hiyo ni kuonesha dhahiri kwamba mwakilishi huyo hafanyi kazi zake alizopewa. Kwa sababu ni jukumu lake kwenda kwenye *library* na kutizama sheria ambayo ipo au inataka kufutwa.

Mhe. Naibu Spika, hata ukiacha hayo unapozisoma sheria tatu hizi kwa pamoja, sheria hii mpya kwa kweli imechukua mambo yote takriban katika sheria mbili zile nilizozitaja. Hapa nimefanya *analysis*. Sheria hii

Kifungu cha 3 au Mswada huu mpya ni sawa sawa na kifungu cha 3 cha sheria ambayo tunaifuta ya mwaka 1999, ni sawa sawa na kifungu cha 3 cha Sheria Nam. 4 ya mwaka 1988 ambayo tunaifuta.

Kifungu cha 4 vile vile ni sawa sawa na kifungu cha 4 na kifungu cha 8 cha sheria hizo.

Kifungu cha 5 ni sawa sawa na kifungu cha 11.
Kifungu cha 12 ni sawa sawa na kifungu cha 18.
Kifungu cha 15 ni sawa sawa na kifungu cha 19.
Kifungu cha 20 ni sawa sawa na kifungu cha 18
Kifungu cha 22 ni sawa na kifungu 9.

Halafu jaduweli zilizomo katika sheria hii ni sawa na jaduweli zilizomo katika sheria zile ambao tunazifuta. Kwa hivyo sheria hii Mhe. Naibu Spika, ilichofanya ni kuboresha au ni kuweka sheria hii kuwa nzuri zaidi. Na uzuri wake ni namna gani? Kwa mfano ukiitizama sheria ya zamani ambazo tunazotaka kuzifuta, sheria zile zinatoa marupurupu mengi zaidi kuliko sheria hii.

Mhe. Naibu Spika naomba kila mwakilishi atizame kifungu cha 4, kifungu cha 5, kifungu cha 8 na kifungu cha 12 cha sheria hii, imeweka hasa na imesema na ukisoma utaona kwamba vifungu hivi vinapunguza yale maposho na marupurupu yaliyomo katika Sheria Nam. 6 ya mwaka 1999 na Sheria Nam. 4 ya mwaka 1988.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo sheria hii tunayoijadili sasa ni sheria ambayo ni nzuri zaidi kuliko hizi. Sasa unaposema kwamba sheria hii inatoa marupurupu mengi si kweli, si kweli hata kidogo. Ni suala la mwakilishi kwamba hakufanya kazi yake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, katika hoja ambayo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati, alisema kwamba ile asilimia X na hii iliungwa mkono na Wawakilishi wengine. Alisema kwamba asilimia X isiwe X lakini yeye alipendekeza asilimia 100.
Mhe. Naibu Spika, kwa nini tukaitoa, ni katika misingi hiyo hiyo waliyoielezea waheshimiwa wawakilishi, kwamba ukiweka asilimia 100 unawapa viongozi wa kisiasa fedha nyingi sana na hilo serikali imeliona. Baada ya kuona hivyo ndio ikasema isitoe asilimia 100 kama sheria hizi zilivyo.

Sasa mwakilishi anapokuja akasema serikali imetoa fedha nyingi sana kwa sababu tumeweka X ambayo x ni chini ya 100, mimi shangaa. Na hii ni upotoshaji wa makusudi kwa wananchi kuonesha kwamba serikali haijafanya *home work* yake. Si kweli.

Mhe. Naibu Spika, unaposema kwamba 100% kwamba ile X iwe asilimia 100, athari yake ni hii inayofuata. Mtakumbuka Mhe. Naibu Spika, kwamba Mhe. Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika hotuba zake nyingi tu katika kuwapenda wananchi wake na wafanyakazi wake alisema, na hii hajasema mara moja na wala hajasema mara mbili. Alisema kwamba kila mwaka atajitahidi au serikali yake itajitahidi kuongeza maslahi ya wafanyakazi.

Kwa hivyo hiyo ni uhakika kwamba Mhe. Rais kila mwaka ana nia ya kuongeza mishahara.

Athari ya kuweka 100% mpaka kwa viongozi wa siasa ni kwamba pale inapoongezwa mishahara huyu kiongozi wa kisiasa, akiwemo mwakilishi marupurupu yake yatakuwa makubwa sana sana sana na hili serikali imeliona. Ndio maana ikakataa kusema kwamba kiongozi wa siasa alipwe marupurupu yake asilimia 100 ya mshahara wake kwa miezi au kwa siku alizofanya kazi. Hivyo itakuwa sivyo.

Lakini la pili ni suala la fedha. Kuna wengine walisema kwamba Mswada huu uje katika mwaka 2014. Mhe. Naibu Spika, wewe ni shahidi na wengi ni mashahidi kwamba suala hili likiletwa katika mwaka 2014 halitojulikana suala hili isipokuwa kila mwananchi atasema kwa sababu 2015 ndio mwisho, wanasiasa wanajiongezea marupurupu. Hiyo haiwezekani. Lazima suala hili lijadiliwe na likubalike. Halafu tujue masuala haya tunayoyazungumza hayalipwi kila mwaka. Masuala haya yanalipwa kila baada ya miaka mitano au pale ambapo mtu anakufa.

Sasa kama kila baada ya miaka 5, lazima sheria iwepo mapema ili fedha zile ziwekwe katika kitu kinachoita S*inking Fund*. *Sinking Fund* ni *Fund* ya kiserikali iliyokuwepo makusudi ili kukidhi haja hii. Lakini 2014 fedha hizi utaziweka katika s*inking fund* ya mwaka mmoja kweli utazipata. Lakini ukishakujua utaratibu huu, kwa hivyo fedha hizi zinawekwa katika *sinking fund* ili inapofika 2015 kila mtu anapata haki yake.

Lakini kuna suala ambalo liliulizwa kwamba kuna mambo mengi, kuna ICU, kuna Skuli, kuna maji ya Magomeni na Mgogoni. Haya Mhe. Naibu Spika, ni kweli lakini tutofautishe baina ya matumizi haya na matumizi ya *recurrent*. Matumizi haya ya ICU, maji na mambo mengine ni matumizi ambayo yanatoka katika mfuko wa *recurrent* ambao kila mwaka unatolewa fedha kwa ajili hiyo. Naomba tutofautishe sana baina ya fedha hizi ambazo zinatolewa katika *sinking fund* na fedha ambazo zinatumiwa kwa mafumizi ya *recurrent*.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wajumbe wamesema kwamba mwaka mmoja kufanya sheria hii haielekei kwa sababu hatujapata nafasi ya kumjaji mtu. Suala hili halimjaji mtu, suala hili linasema mtu anayefanya kazi katika nafasi ile ikiwa ame- *qualify* basi atalipwa posho lake na marupurupu yake ambayo yanakusudiwa. Sasa si suala la ku-*qualify* au sio suala la kusema kwamba mtu huyu atizamwe. Mtu huyu atatizamwa akiwa hastahiki atatolewa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Lakini madhali ameshakuwa ni mfanyakazi wa kisiasa au hata aliyekuwa sio wa kisiasa kwa sababu yapo

maposho yake na marupurupu yake. Kwa hivyo hiyo itakuwa *determine* na sheria nyengine.

Mhe. Naibu Spika, hata ukitizama katika sheria hii kifungu cha 5 kinasema kiongozi wa kisiasa hatostahiki kulipwa mafao chini ya sheria hii ikiwa utumishi wake utasita kwa vitendo vya aibu na fedheha kwa Zanzibar, vilivyothibitishwa bila ya kuwa na shaka chini ya Katiba au sheria nyengine yoyote. Kwa hivyo utaratibu huu upo ikiwa kiongozi yule kasimamishwa au kaondolewa kwa aibu ina maana hapati marupurupu haya. Kwa hivyo hili sio suala la kusema kwamba tusubiri halafu tumtizame mtu mpaka katika mwaka wa 2014 ndio tufanye sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo. lilizungumzwa la *Separation of Powers*, nakubali kwamba kuna *Separation of Powers*. Lakini kikazungumzwa kifungu cha 58. Kwamba Raisi anaweza akamteuwa mshauri wake wakati wowote. Lakini hivyo hivyo kukazungumzwa kifungu cha 62 nafikiri au kifungu cha 52 kinachosema kwamba Raisi hatolazimika kufuata ushauri wa mtu yeyote. Sasa hapa kuna mambo mawili. Kwanza Raisi ana uwezo wa kumteuwa mtu yeyote kuwa mshauri wake.

Tutizame Raisi ni mtu gani? Raisi kazi yake ni ya kisiasa, basi hiyo ndio kazi yake. Kwa hivyo mtu yeyote anayemshauri Raisi atakuwa anamshauri kisiasa. Kwa hivyo na wale *automatically* watakuwa wanasiasa, hawatokuwa wafanyakazi wa kawaida. Na utaratibu huu upo tokea enzi za Mzee Karume na umeanzishwa na Mzee Karume na wanasiasa wale waliokuwa wanaitwa makamisaa. Sote tunajua kulikuwa kuna Makamisaa kwa Mzee Karume. Alipoondoka Mzee Karume kaja Mzee Jumbe pia kulikuwa kuna makamisaa, halafu akaja Mzee Mwinyi kukawa na makamisaa halafu wakabadilishwa wakawa ni washauri na tunaendelea nao mpaka sasa. Kwa hivyo washauri hawa ni washauri wa kisiasa, hendi kule mshauri kumshauri Rais kuhusu utendaji wa kitu fulani, lakini anamshauri Rais ambaye yeye ni mtu wa siasa. Kwa hivyo *definitely* washauri hawa ni washauri wa kisiasa.

Kifungu 52 kinasema hivi, Kwa bahati Mwakilishi alikisoma na mimi naomba nikisome.

> “Rais wa Zanzibar hatolazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote katika utekelezaji wa shughuli zake, isipokuwa kama sheria inaagiza vyenginevyo.”

Yeye akaogopa akasema kwamba Raisi tulisema ashauriane na Spika, ashauriane na Makamo wa Pili wa Raisi. Lakini akasema kifungu hichi

anaweza Rais akasema hasikilizi ushauri wa Spika na ushauri wa Makamo wa Pili.

Si kweli, kwa sababu hapa tunatunga sheria na sheria inaagiza kwamba Rais ashauriane na wakubaliane na Spika, na Makamo wa Pili wa Rais. Sasa katiba itamfunga kwamba anaweza Raisi kwamba hatolazimika kufuata ushauri wowote isipokuwa kama sheria imeagiza hivyo na sheria ikishakuagiza hivyo kwa hivyo Raisi ameshafungika. Kwa hivyo kifungu hichi kitamfunga Raisi. Kwa hivyo ni lazima Raisi ashauriane na Spika, ashauriane na Makamo wa Pili wa Rais katika utekelezaji wa Sheria hii ambayo itatumika.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa kuhusu Waziri kutunga kanuni. Akasema Waziri anaweza akatunga kanuni zikawa zinamatatizo. Napenda niseme mbele ya Baraza lako tukufu kwamba katika utaratibu wa kutunga kanuni kuna taratibu aina mbili.

- Taratibu ya kwanza Waziri anapewa uwezo chini ya sheria kutunga kanuni na akishakutunga kanuni akataja tu kwamba kanuni hizi zitatumika tarehe kadhaa na tarehe kadhaa.

- Utaratibu wa pilli ni kwamba Waziri anapotunga kanuni basi anaweza kuzipeleka Baraza la Wawakilishi kupata taarifa ya kanuni zile.

Kwa sababu huu ni utaratibu wa kawaida sioni tatizo la kusema kwamba Waziri atatunga kanuni halafu azilete katika Baraza la Wawakilishi. Hiyo haina matatizo kisheria.

Mhe. Naibu Spika, ukitizama katika masuala haya sasa kama nilivyosema mwanzo naomba sasa tuje katika Mswada wenyewe. Hii ndio sehemu yangu ya pili ambayo nataka kuzungumza.

Kama nilivyosema kwamba katika Mswada huu, eneo kubwa la Mswada huu umechukua maeneo yaliyopo katika Sheria mbili ambazo tuna lengo la kuzifuta. Unaposoma kifungu cha 1, kwa mfano na kifungu cha 2 na kifungu cha 3 katika Mswada huu. Vifungu hivi ni sawa sawa na vifungu vilivyowekwa katika Sheria Nam. 6 ya mwaka 1999 na Sheria Nam. 4 ya mwaka 1988.

Halkadhalika kifungu cha 4 ambacho kinazungumzia stahiki za kulipwa mafao. Kifungu hichi kimechukuliwa sawa sawa na Sheria Nam. 4 mwaka 1999 na kifungu cha 4 mwaka 1988. Kifungu cha 5 cha Mswada huu ambacho kinazungumzia kukosa sifa za kulipwa mafao. Hichi ni kifungu kipya ambacho kimewekwa kwa ajili ya kuwadhibiti wale wanasiasa ili kuonesha kwamba Mswada huu ni mzuri zaidi. Kwa sababu umemdhibiti mwanasiasa kwamba

anaweza kafanya mambo yaliyokuwa hayana maana. Pale anapofanya mambo yaliyokuwa hayana maana Sheria hii itamkosesha haki zake. Wakati katika sheria mbili za nyuma ambazo tunazifuta, masuala hayo yalikuwa hayapo sana. Mhe. Naibu Spika, katika mafao vile vile Mswada huu umebana kidogo mafao ya viongozi wakuu wa kisiasa, yaani Raisi, Makamo wa Raisi wakati zamani alikuwa ni Waziri Kiongozi. Kwa nini?

Ukisoma kifungu cha 12(2) kinasema kwamba

> "Endapo Makamo wa Raisi Mstaafu atafariki mjane wake atastahiki kulipwa na mamlaka husika pencheni ya kila mwezi kwa miaka mitatu itakayokuwa sawa.."

Lakini ukisoma sheria hizi mbili zinasema iwapo Raisi kwa wakati ule ni Waziri Kiongozi ikiwa watakufa basi wale wajane pamoja na watoto watalipwa mpaka kuendelea, haikutoa kikomo. Kwa hivyo kama haikutoa kikomo ina maana matumizi yanakuwa ni makubwa.

Lakini hapa katika Mswada huu umetoa kikomo yaani kikifika kikomo fulani angalau kile kipindi cha kuondokana na majonzi basi watakuwa hawalipwi tena. Ndio Mswada huu unavyosema. Lakini sheria hizi mbili zinazungumzia suala la kusema kwamba ikiwa Raisi au Makamo wa Raisi au Waziri Kiongozi wakati ule akifa basi wale wajane pamoja na watoto wataendelea wala haikusemwa kwamba ni mtoto aliyekuwa chini ya umri wa miaka 18 au laa, wamesema ni watoto tu wa Raisi au wa Waziri kiongozi.

Sasa kama hivyo ndivyo tunaona kwamba Mswada huu umepunguza hayo. Huu umesema kwa miaka mitatu lakini pia umesema ni watoto ambao ni chini ya miaka 20, ama pale atakapoolewa au akifika miaka 20 itakuwa ni basi. Kwa hivyo hiyo ni afueni kubwa. Wakati zamani serikali ilikuwa inawalipa tu hawa kwa kipindi chote, lakini sasa hivi serikali imeona kwamba ipunguze matumizi hayo na ndio maana ikafanywa hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 15 pia kinasitisha kutoa pencheni kwa watu au watoto wa viongozi kwa muda wote ni tofauti na sheria hii, ambayo sheria hii inasema kwamba kifungu cha 19 naomba nikisome ili nifahamike vizuri cha sheria ya zamani.

Kifungu cha 19 *"Every legitimate child of the distaste leader born or conceived during period of folding specified state office of amount equal to the minimum salary for civil service a prove by the government"*

Kwa hivyo hapa ni *avery legitimate child* ya marehemu yule na haikusema kwa muda gani, madhali yule ni mtoto wa marehemu kwa hivyo ataendelea kulipwa tu kwa kipindi chote. Hii ndio sheria ya zamani. Sheria hii inasema hivyo, serikali itatumia pesa nyingi. Kama serikali itatumia pesa nyingi hebu tuwapunguze hawa tuwape kipindi cha miaka mitatu angalau kupata *consolidation* kidogo ya majonzi ambayo wamepata kutokana na kifo cha mzee wao. Ndio maana ikasema bila ya kujali masharti yaliyotungwa na sheria hii. Raisi mstaafu au Makamo wa Raisi mstaafu au Spika Mstaafu, hawatolipwa mafao yao kama yalivyoelekezwa kwenye majuweli ya sheria hii, isipokuwa kwa kiinua mgongo na posho la kumaliza muda ikiwa ataacha kutumikia nafasi moja ya kisiasa na kwenda kumiliki nafasi nyengine.

Katika sheria hii kwa mfano mtu alikuwa ni Makamo wa Raisi au Waziri Kiongozi. Mfano mzuri sioni vibaya kusema Mhe. Shamsi. Mhe. Shamsi alikuwa Waziri Kiongozi, alioondoka Waziri Kiongozi ikawa anapata mafao yake yote, jensheni na kila kitu. Hivi sasa ni Waziri wa Mambo ya Ndani, ni kiongozi vile vile. Kwa hivyo kwa mujibu wa sheria hii itakuwa anapata mapensheni haya pamoja na mambo mengine ya kule. Lakini sheria hii inasema hivyo ni kutumia fedha vibaya ikiwa wewe utakuwa Waziri Kiongozi halafu unakwenda katika nafasi nyengine ya kisiasa hii pensheni yako hii itasimamishwa utatumia ile kule mpaka umalize.

Sasa jamano hapo serikali si imesaidia kupunguza fedha za wananchi. Hii ndio sheria inavyosema ya wananchi. Kwa hivyo hili ni suala ambalo mimi nahisi tungelisoma vizuri sheria hii tunayotaka kuipitisha na sheria hizi ambazo zilikuwepo. Kitu kikubwa hapa, tofauti iliyokuwemo baina ya sheria hizi mbili ambazo tunaomba zifutwe na huu mswada ni kwamba zamani Spika alikuwa hayumo katika hii, humu yumo. Na hii kwa nini tukafanya hivyo? Tulifanya kwa sababu tunaheshimu mihimili mitatu ya nchi hivyo kwa nini Spika aachwe? Lakini leo Waheshimiwa Wawakilishi wanasema turejee kule kule tuongeze gharama na Spika wetu mpendwa tumuache. Hiyo haiwezekani kwa sababu tupo katika suala la mihimili mitatu. Kwa hivyo, ndio maana tukamuongeza Spika, lakini ukitizama yale matumizi yote yamepunguzwa kwa kiwango kikubwa, ukija katika *schedule* katika jadweli ya kwanza, ya pili na ya tatu ambazo zinazungumzia Rais, zinazungumzia Makamo wa Rais na zinazungumzia Spika hizo zote ni sawa sawa na jadweli zilizokuwemo katika sheria hizi.

Mhe. Naibu Spika, hapa nina jadweli hiyo na imeandikwa *hapa terminal benefit to former president* mambo yote yaliyomo yale ya *fifty percent, winding up allowance equal to the amount that to received the salary in twenty months* na humu imo halafu. Kila kitu kimo isipokuwa yale mambo ambayo nimeyasema mwanzo kwa mfano mtoto anapofika miaka 20 ndio basi, wakati

kule ilikuwa mtoto aendelee kulipwa. Kwa hivyo, hayo itakuwa si barabara na ndio maana serikali ikasema haya mambo mengine tuyapunguzeni, tuyatumie lakini tuyapunguze kwa kipindi kile ambacho tunahisi inatosha na ndio maana tukasema miaka 3 wakati zamani ilikuwa mtoto anaendelea kulipwa wakati wote. Kwa hiyo hivyo sivyo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, ukenda katika jadweli hili na hii sheria ya zamani kifungu cha ® humu katika mswada huu kimeongezwa ili kukinga yale ambayo humu Rais au Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais wangelifaidika kama ni sheria ile ya zamani. Kwa hivyo, humu tumepunguza matumizi ukilinganisha na humu.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba ukiusoma mswada huu na ukisoma sheria hizi ambazo tunaomba zifutwe ni dhahiri kwamba serikali imezingatia yote hayo, imezingatia hali halisi, imezingatia namna gani hawa viongozi wapate heshima zao. Lakini pia kwa kutizama namna au njia yakufanya kwamba yule kiongozi aweze kuishi katika hali ambayo ni nzuri. Kwa hivyo, ninachopenda kusema Mhe. Naibu Spika, ni kwamba humu katika mswada huu ambao tunaomba Waheshimiwa Wawakilishi waukubali ukitizama na sheria hizi mbili ni kwamba maslahi ya viongozi yamepunguzwa kwa asilimia kubwa. Kubwa hapa linalojadiliwa ni kusema kwamba kwa nini suala (x) likawemo isiwe ni asilimia 100.

Kama nilivyosema mwanzo Mhe. Naibu Spika, suala la (x) kama (x) ni kitu kibaya unaweza hata ukatia (y) sio lazima (x). Lakini hilo suala la (y) linaonesha Mhe. Naibu Spika, kwamba zile fedha ambazo kiongozi alikuwa apate ukitia asilimia 100 zitakuwa ni nyingi sana itakuwa tunawaumiza wananchi wetu. Kwa hivyo, hatuwezi katika mazingira haya kuwaumiza wananchi wetu kwa hivyo Rais kwa kutizama hali ilivyo, kwa kutizama uchumi ulivyo yeye ndio ata-*determine*. Lakini pia imesema katika sheria kwamba *determination* yake haitopungua kiinua mgongo ambacho zamani mtu alikuwa anapata. Kwa mfano kwa mujibu wa sheria hii ikiwa Mwakilishi 2010 alikuwa anapata (x) ndio marupurupu yake sasa kwa mujibu wa sheria hii 2015 mwakilishi atapata (x) jumlisha na zile ambazo zitakuwa *dermine* na Rais, Makamo wa Pili wa Rais na Spika na lazima wakubaliane kwa mujibu wa sheria hii na kwa mujibu wa Katiba. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Katiba inasema Rais anaweza au halazimiki kuchukua ushauri kwa mtu yeyote, lakini ikiwa sheria inasema kwamba Rais na mtu mwengine lazima wakubaliane kwa pamoja kwa hivyo hiyo ndio sheria. Kwa hivyo, hiyo nyongeza itakuwa *determine* na Mhe. Rais, Makamo wa Rais na Spika kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia mimi napenda niseme kwamba nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wausome huu mswada, wasome sheria zile

ambazo tunataka kuzifuta, mswada huu umepunguza sana mafao ya viongozi na kwa maana hiyo naamini kwamba mswada huu ni mzuri kwani ni kwa maslahi ya wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba mimi binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni tunaunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika mswada huu. Mhe. Naibu Spika, mimi naungana mkono na wenzangu waliotangulia ukiondoa mjumbe aliyepita sasa hivi kwamba siungi mkono huu mswada. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba siungi mkono kwa sababu nyingi sana nina mambo mengi ambayo nimeyaona na tuliwahi kuyazungumza katika semina kule, lakini Mhe. Waziri inaonekana hakuataka kabisa kutusikia, sisi tuliitana kwenye semina kule kuujadili huu mswada na kutoa mapendekezo yetu kabla ya kuuleta kwenye Baraza. Mhe. Naibu Spika, tulijadili pale tukatoa mapendekezo mengi sana kama ambavyo Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilivyotoa mapendekezo yao.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana upande wa serikali umeshindwa kabisa kuchukua yale mapendekezo yetu. Kwa hivyo, mimi nina mambo humu nimeyaona napendekeza kama yatakuwa yameondoshwa au kama nitakavyotoa mapendekezo yangu yakakubaliwa na Mhe. Waziri basi hapo naweza nikabadilisha maamuzi yangu. Mhe. Naibu Spika, kwanza nikianza na sehemu ya tatu ya mafao kwa Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu na Spika Mstaafu, hapa nimeona kuna vipengele ambavyo wenzangu walishavizungumza na mimi nataka nivirejee baadhi ya vipengele hapa. Mhe. Naibu Spika, endapo Rais Mstaafu atafariki basi mjane wake atastahiki kulipwa na mamlaka husika pencheni ya kila mwezi itakayokuwa sawa na asilimia maalum ya mshahara wa Rais aliyepo madarakani.

Mhe. Naibu Spika, mimi hoja yangu ya mwanzo kabisa ni huu mshahara, huu mshahara wa Rais aliyekuwepo madarakani sisi hatuujui. Kwa hivyo, kama hatuutambui hivyo hatufahamu kiasi gani analipwa hivyo hizi asilimia zilizowekwa humu sisi tutazithibitisha vipi kwa kujua kiwango gani anacholipwa huyo muhusika. Mwanzo kabisa nafikiria Mhe. Waziri walikuwa wakubaliane na sisi angetuletea kile kiwango cha mshahara ambacho Rais aliyekuwepo kwenye madaraka anastahili kulipwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiria tungekuwa tunakijua basi mimi nafikiria hapa kusingekuwa na matatizo sana, kwani ni rahisi sana mswada huu tungeweza kuujadili kwa wepesi na tukaweza kufikia muafaka. Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 35 huu mshahara na maposho ya Rais yanapangwa na Baraza la Wawakilishi. Lakini hakuna kikao hata kimoja ambacho kimepanga maposho haya na mshahara huu, hivyo leo

tuje tuidhinishe hii ni sheria tunataka kuiweka naomba tukumbuke hilo. Hivyo tunaenda kuweka sheria na wala hatujui huyo mtu atakuwa anapokea kiasi gani. Mhe. Naibu Spika, mimi nafikiria hili litakuwa ni tatizo tena kubwa sana. Kwa hivyo, mimi niungane na wale wenzangu waliotaka mswada huu urudi ukafanyiwe haya marekebisho ambayo tunayasema, ni ya msingi sana haya halafu ndio uletwe tena tuje tuujadili hapa.

Mhe. Naibu Spika, tukienda kwenye jadweli la kwanza la mafao atakayolipwa Rais Mstaafu kiinua mgongo sawa na asilimia 50 ya mshahara wa juu aliopokea wakati anasita kuwa Rais zidisha kwa miezi iliyotumikia nafasi hiyo. Mhe. Naibu Spika, tatizo ndio liko pale pale hatujui kitu hivyo mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri kwenye hili tukajuulishana kwanza ndio ndipo tukaendelea kuuchangia mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mengi sana hapa ya asilimia, mimi katika asilimia hizi siko tayari kupitisha hata fungu moja katika hili bila ya kujua ni kiasi gani atachoenda kulipa huyo muhusika. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wamesema hapa inawezekana tunapitisha asilimia 80, lakini kwa mtazamo au kwa maisha yalivyo hivi sasa tulikuwa tunampelekea kidogo tukaamua tumpe mia moja kabisa, au tukaona tunampa nyingi tukaamua kumpunguzia kumuwekea asilimia iliyokuwa chini ya kiasi. Kwa hivyo, ni lazima kwanza tuelewe ni kipi anachokipata ili tukimpitishia hiki atapata ngapi sasa. Mimi nafikiria Mhe. Waziri hili kwanza ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, nije tena katika jadweli hilo hilo kwenye vifungu vinavyoanzia (i), (j) na (k) kuhusu ofisi, wasaidizi, Katibu Muhtasi. Mimi nafikiria kwa sababu huyu mtu amestaafu hakuna haja ya kumuwekea ofisi, tuwaache hawa viongozi wetu wanapostaafu wakapumzike tukiwaekea ofisi maana yake tunawataka wafanye kazi. Kwa hivyo, hawa ni wastaafu wameshaitumikia nchi hapa pengine miaka kumi katika Urais ni kazi kubwa sana hii, hivyo ameamua kupumzika mimi nafikiria tuwape nafasi vizuri ili waweze kupumzika. Kwa hivyo, vifungu hivi mimi ningeshauri viondoshwe kabisa na katika kiwango cha shilingi lake kama posho la kila mwezi la simu pia mimi hili naliona hili ni kubwa mno, tusimpe mazonge sana ya kumuingizia fedha hizo ili aweze kupiga simu sana.

Mhe. Naibu Spika, sisi huku katika majimbo posho yetu ya simu tunaiona hapa na tuna watu karibu 16,000 au 15,000 kutwa watu wanatupigia *missed calls* hapa tukiingiza 20,000 kwa siku basi hazitoshi. Lakini huyu tunamuwekea shilingi 500,000 hizo ni shingi mno hizi tupunguze tuweke angalau 300,000 hivi zitaweza kumsaidia katika matumizi yake ya simu za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, niende katika jadweli hilo hilo la kwanza, kwamba malipo ya daraja la kwanza kwa safari binafsi ambazo hazitopindukia nne kwa mwaka mmoja ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na moja kwa nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itajumuisha wake, watu wa familia na mambo kama yaliyoanishwa. Mimi hii safari ya nje moja kwa mwaka haina tatizo nakubaliana nayo, lakini hizi za ndani ya Tanzania nne kwa huduma ambazo zilipiwe na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hizi ni nyingi sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda wa kuchangia jioni tumemaliza kwa hivyo utamaliza dakika zako 10 kesho tukijaaliwa.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 19/01/2012 saa 3:00 asubuhi)